# Nipashe

Jumatatu Machi 16, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580180

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





RIPOTI MAALUM

## Chupa za chai zatumika kuuza pombe za viroba

UKURASA 4




UKURASA 13

# Freeman Mbowe: Hatulipi kisasi



• **Polisi** wasema upelelezi vigogo, wanachama waliokamatwa Ijumaa waiva...*Uk. 2*



**BAA LA CORONA**

**WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameagiza mahafali ya kidato cha sita yanayofanyika nchini kutohusisha wageni kutoka nje ya shule husika ili kujiepusha na ugonjwa wa corona.**

- **Epuka mikusanyiko ya watu isiyo ya lazima**
- **Nawa mikono kwa maji yanayotiririka na sabuni kila mara**
- **Ukipiga chafya au kukohoa ziba mdomo**



Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, katika picha ya pamoja na Makamu Mwenyekiti Bara, Dorothy Semu (katikati) na Mwenyekiti mpya wa chama hicho, Maalim Seif Shariff Hamad, baada ya kutangazwa washindi wa uchaguzi mkuu jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Wadaiwa kuua mtoto wa miezi 9 kuimarisha penzi lao

UKURASA 3



TISHIO CORONA

## Serikali yatenga hospitali maalumu

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **SPORTPESA YAMWAGA VIFAA VYA MICHEZO** UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

## TISHIO CORONA

# Serikali yatenga hospitali maalumu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetenga hospitali maalumu katika kanda zote nchini kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa watakaobainika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, alisema kuna hospitali zilizotengwa kanda zote nchini kwa ajili ya kuhudumiwa washukiwa wa corona kwa kuwa hawatakiwi kulazwa kwenye wodi za kawaida. "Kuna vitu lazima Watanzania tujifunze, nilishangaa juzi mtu anasema Regency kuna mgonjwa haiwezi kutokea mgonjwa wa corona akawekwa Regency, huu ugonjwa mbaya sana," alisema.

Alisema serikali imechukua hatua kama ilivyo nchi nyingine na imejiandaa kama itatokea mgonjwa wa virusi hivyo akabainika nchini.

"Pale Dar es Salaam kuna hospitali imetengwa maalumu kwa sababu hatuna mgonjwa, hatuwezi kusema ipo wapi, ila ikitokea kuna mgonjwa hawezi kwenda kwenye wodi au hospitali ya kawaida," alisisitiza.

Dk. Abbas alisema, hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwamo kusitisha safari za ndege za Tanzania. "Serikali imeunda vikosi kazi mbalimbali vya kitaifa na mikoa ili kuchukua hatua, nipongeze vyombo vya habari vimeanza kutoa elimu kwa umma kuhusu hatua za kuchukua, endeleeni kutoa elimu hili ni suala la kitaalamu ili kutotia hofu watu," alisema.

Vile vile, alisema Tanzania ipo salama licha ya nchi zaidi ya 100 duniani kukumbwa na ugonjwa huo. "Nchi yetu imechukua hatua mbalimbali kwa kila taasisi na hatua za kitaifa zipo, Watanzania waendelee kuchukua hatua, Wizara ya Afya itaendelea kutoa taarifa kitaalamu, kwenye maeneo yote ambayo wageni wanatumia kuingia nchini kuna wataalamu kwa ajili ya kupima hatua za kwanza za mshukiwa wa ugonjwa huo," alisema.

Alisema uwanja wa ndege kinachopimwa ni joto na sio corona.

"Hatua ya pili baada ya mtu kuhisiwa, nchi yetu imeweka vituo maalumu vya kuwatenga washukiwa wa ugonjwa, wanapimwa kupitia maabara ya taifa na ukibainika una corona hatua ya tatu unapelekwa kwenye hospitali maalumu," alisema.

Kadhalika alisema, kama Tanzania ikifanikiwa katika hatua za kujikinga kuna uwezekano wa kujiepusha na gharama za kuhudumia wagonjwa.

"Msiwe na wasiwasi tusipaniki tuamini serikali inafanya kazi na kama kutakuwa na viashiria fulani serikali itatoa taarifa," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameagiza mahafali ya kidato cha sita yanayofanyika nchini kutohusisha wageni kutoka nje ya shule husika ili kujiepusha na ugonjwa wa corona. Jafo alisema ili kujiepusha na ugonjwa huo ni vyema Watanzania wakaepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

"Kwa mfano mahafali tumezoea wazazi kutoka mikoa mbalimbali wanashiriki, naelekeza kuwa sherehe hizo za mahafali zisihusishe wageni kutoka nje ya shule kama kuna ulazima wa kufanya mahafali, na yafanyike kwa kuwahusisha wanafunzi pamoja na jamii ya shule tu na sio wageni kutoka sehemu mbalimbali za nchi yetu," alisisitiza.

Aliongeza: "Hii ni kwa nia njema ya kuendelea na mikakati na maelekezo ya Wizara ya Afya na msisitizo mkubwa uliotolewa na Dk. John Magufuli kuhusu kupuka misongamano isiyokuwa na lazima katika kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona." Alisema ugonjwa huo ni hatari na unaua kwa haraka licha ya kuwa hadi sasa Tanzania haina mgonjwa kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11

(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)
Katika mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI

Usimamizi wa Mirathi No. 12/2020.

Ombi la 1 ASMINI CHAIMA 2. JOHARI CHAIMA
kuteuliwa kuwa
Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu CHAIMA ALLY CHIAPO

KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 2/3/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

115669702



PASSPORT IMEPOTEA



15669302

**LEAH HOSEA KIMARO** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 313222** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam tarehe 3/3/2020. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/202032/2020.**




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama ambaye ni Mbunge wa Peramiho, akishirikiana na wananchi wa kijiji cha Ngahokola wilayani Songea kung'oa visiki kwa ajili ya kutengeneza barabara yenye urefu wa kilomita sita kuelekea hospitali ya wilaya. **PICHA: GIDEONI MWAKANOSYA**

# Mbowe: Hatulipi kisasi

**Na Gwamaka Alipipi**

ZIKIWA zimepita siku nne tangu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, atoke gerezani, amesema chama chake hakitalipa kisasi.

Amesema wataendelea kuomba umoja na mshikamano wa kitaifa na kwamba wanataka kuona Watanzania wote wanakuwa salama, nchi inakuwa sehemu nzuri ya kuishi.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati alipoenda kuwajulia hali baadhi ya viongozi wa chama hicho waliolazwa hospitali baada ya kudaiwa kupigwa na maofisa wa Magereza walipokuwa wakienda kumpokea (Mbowe) kwenye Gereza la Segerea.

Viongozi wa Chadema waliolazwa hospitalini ni Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

Viongozi hao wanadaiwa kupigwa na kuvunjwa mikono na miguu na maofisa wa Magereza siku hiyo.

Akiwa hospitalini hapo, Mbowe alisema: "Tuliahidi na tunaahidi, tutasimama na taifa na Watanzania wote, tunataka kuona Watanzania wote wanakuwa salama na nchi inakuwa salama na mahala pazuri pa kuishi."

"Maadili yetu tutayasimamia na kuyapigania kwa nguvu zote, na hata salamu zetu wakati wa mkutano mkuu tuliyoianzisha tulisema 'No hate no fear' (hakuna chuki, hakuna hofu), hatutajenga kisasi wala hatutalipa kisasi," alisema Mbowe.

Alisema mwenye jukumu la kuhukumu ni Mungu na kwamba wao hawawezi kuingilia majukumu hayo.

"Tuna mengi ya kufanya kwa ajili ya nchi yetu, kufikiri ya jana na kuanza kuwaza kulipa ni ujinga, sisi sote tu wadhambi, lakini lazima tuangalie zaidi katika kuijenga kesho yenye matumaini kwa nchi yetu kuliko kuitafuta jana yenye chuki na kisasi kwa yaliyopita," alisema Mbowe.

Hata hivyo, Mbowe aliahidi kuzungumza zaidi leo na waandishi wa habari kwa kutoa salamu rasmi za chama kwa taifa.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam limesema upelelezi wa kesi inayowakabili viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), umeshakamilika na kwamba leo litawasilisha jalada kwa Mwanasheria wa Serikali ili taratibu zingine ziendelee.

Viongozi hao ni Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, Meya wa Ubungo, Boniface Jacob, Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya, pamoja na wanachama 27 wa chama hicho ambao wanatuhumiwa kuvamia Gereza la Segerea na kufanya fujo, kuwavamia maofisa wa Magereza na kuwazuia kufanya kazi zao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi kanda hiyo, Lazaro Mambosasa alisema: "Upelelezi wa kesi umekamilika na kesho jalada litapelekwa kwa mwanasheria wa serikali alipitie kisha ataamua kama kuna kesi kwa namna itakavyomfaa atapeleka mahakamani wakajibu tuhuma hizo."

Kamanda Mambosasa alisema siku ya tukio watuhumiwa hao waliambatana na wafuasi wengi kwenda katika Gereza la Segerea kwa lengo la kumpokea mwenyekiti wao, Freeman Mbowe.

Alisema lakini walipofika katika eneo hilo walitumia nguvu eneo la geti pamoja na kumchania nguo askari wa magereza aliyekuwa kwenye lindo.

"Tulipigiwa simu na Magereza kuwa kuna watu wanataka kuvamia eneo la magereza na wanafanya fujo, tuliondoka mara moja kwenda eneo la tukio kwa kupeleka askari wa kanda pamoja na askari wa kutuliza ghasia," alisema Kamanda Mambosasa na kuongeza:

"Tulipofika tulikuta maofisa wa Magereza walishawakamata baadhi ya watuhumiwa na kuwaweka chini ya ulinzi, hivyo Jeshi la Polisi lilipofika liliwakamatwa upya na kuwapeleka kituo cha polisi cha Stakishari, hata hivyo baadaye walipata dhamana," alisema Kamanda Mambosasa.

Kamanda Mambosasa alisema Magereza ni eneo nyeti linalotumiwa kuhifadhi wafungwa na mahabusi hivyo mfungwa ama mtu yoyote anatoka gerezani kwa kufuata utaratibu wa mahakama na kwamba kitendo kilichofanywa na viongozi wa Chadema ni cha kihuni.

HABARI KITAIFA

# Wapenzi wadaiwa kuua mtoto kuimarisha penzi

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

MWANAMKE mmoja kwa kushirikiana na mpenzi wake mpya, wanadaiwa kumuua mtoto wa miezi tisa kwa kumnyonga ili kuimarisha mahusiano yao, na mama huyo kuamini ataolewa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, alisema jana tukio hilo lilitokea Februari 25, na watuhumiwa walikamatwa Machi 12, mwaka huu, katika kitongoji cha Mwashega Kijiji cha Bugembe Kata ya Nyamilama wilayani Kwimba.

Alisema mtoto huyo anajulikana kwa jina la Abdallah Simon ambaye aliuawa kwa kunyongwa kwa kutumia kamba na mama yake mzazi, Helena Washera (19).

Alisema mama huyo alitenda jambo hilo kwa kushirikiana na mpenzi wake, Lucas Jackson maarufu 'Kajanja (24)' kisha kuutupa mwili wa mtoto huyo vichakani.

Kwa mujibu wa Kamanda Muliro, baada ya mama wa mtoto kuelezwa na mpenzi wake wa sasa aitwaye Lucas Jackson kuwa amuue mtoto huyo ili amuoe.

Alisema baada ya mwanamke huyo kuelezwa kuwa ataolewa na ndipo kwa pamoja walifanya uhalifu huo na kuendelea na mahusiano yao ya kimapenzi.

Kamanda Muliro alisema baada ya muda kupita, baba mzazi wa mtoto huyo, James Simoni, alikwenda kumsalimia mwanawe na kuambiwa na mzazi mwenzake kuwa mtoto yupo kwa bibi yake, na alipofuatilia alimkosa na kuamua kutoa taarifa Polisi.

"Jeshi la Polisi lilifuatilia na uchunguzi ulibaini kuwa wapenzi hao wamehusika kwa kuwa katika mahojiano ya kina, walikiri kuhusika na mauaji hayo na kwenda kuonyesha sehemu walipoutupa mwili wa mtoto huyo," alisema Kamanda huyo.

Aidha, alisema katika eneo la tukio ilikutwa mifupa inayosadikiwa kuwa mabaki ya mwili wa mtoto mdogo, na kwamba yamepelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Wakati huo huo, mtu mmoja ameuawa na polisi kwa kupigwa risasi wakati akijaribu kuwatoroka baada ya kuwarushia kichwa cha mtoto wa mtaani anayedaiwa kuchinjwa na mtu huyo, kwa lengo la kuwatisha.

Kamanda Muliro alisema tukio hilo lilitokea Machi 9, mwaka huu katika msitu wa Machemba Kata ya Isamilo wilayani Nyamagana jijini hapa.

Alisema mtoto wa mtaani asiyefahamika utambulisho wake, jinsia ya kiume anayekadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 15-20, alikutwa ameuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali hadi kutenganishwa kichwa na kiwiliwili na mtu ambaye baada ya uchunguzi alifahamika kwa jina la Abdul Abdalah mwenye umri kati ya miaka 25-30, mkazi wa Mabatini wilayani Nyamagana.

Alisema baada ya ufuatiliaji wa polisi walimkamata Machi 12 mwaka huu, na alipohojiwa alikiri kutenda kosa hilo kisha kuondoka na kichwa cha marehemu ambacho alitaka kukipeleka kwa mganga wa kienyeji.

# Maalim Seif, Zitto kuiongoza ACT

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kitaingia kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu kikiwa chini ya uongozi wa wanasiasa wawili wazoefu; Zitto Kabwe na Maalim Seif Shariff Hamad. Maalim Seif aliyewahi kuwa Waziri Kiongozi na baadaye Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Zitto ambaye ni Mbunge wa Kigoma Mjini, walitangazwa kuwa washindi wa nafasi za mwenyekiti na kiongozi wa chama katika uchaguzi uliofanyika juzi na jana jijini Dar es Salaam. Juma Duni Haji, mkongwe mwingine wa siasa za upinzani Zanzibar, alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo (Zanzibar), huku Dorothy Semu, akishinda nafasi hiyo kwa upande wa Tanzania Bara.

Semu anakuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa juu zaidi miongoni mwa vyama vikuu vya siasa nchini tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi.

Akitangaza matokeo hayo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya ACT-Wazalendo, Wakili Omar Said Shaabani, alisema Maalim Seif alishinda nafasi ya mwenyekiti kwa kura 337, sawa na asilimia 93.35 ya kura zote zilizopigwa.

Zitto aliyechuana na Ismail Jussa Ladhu katika nafasi ya Kiongozi wa Chama, alishinda kwa kupigiwa kura 276, sawa na asilimia 73.6 ya kura zote zilizopigwa. Jussa alipata kura 91, sawa na asilimia 24.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Maalim Seif alisema ushindi wake ni salamu tosha kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), akidai Watanzania sasa wako tayari kwa mabadiliko ya kiutawala na maisha yao.

Alisema atazungumza kwa kina na wanachama na wafuasi wake wa ACT-Wazalendo mara atakapokalia rasmi kiti chake hicho, akiwashukuru kwa imani yao kubwa kwake.

Zitto pia aliwashukuru wajumbe wa Mkutano Mkuu wa ACT-Wazalendo kwa kuwapa kura za kutosha karibu wagombea wote na akasema wameshinda mtihani mkubwa kupitia uchaguzi huo.

Alisema kitendo cha Maalim Seif kushinda kwa zaidi ya asilimia 90,huku yeye na Dorothy wakishinda kwa zaidi ya asilimia 70, kinaonyesha kwamba chama hicho ni kimoja; kisicho na ubaguzi wa wageni na wakuja, wa Bara na Wazanzibar, wanaume na wanawake au wazee kwa vijana.




# Chupa za chai zatumika kuuza pombe za viroba

## ■Wateja waibuka na msamiati
## ■Viongozi wa dini walia na usiri

Na Mary Geofrey

IKIWA ni miaka mitatu tangu kuanza kwa utekelezaji wa amri ya serikali kupiga marufuku biashara ya uuzaji wa pombe kali kwenye mifuko midogo ya plastiki, maarufu viroba, imebainika bado kuna baadhi ya maeneo, yakiwamo ya Jiji la Dar es Salaam, vilevi hivyo vingali vinauzwa.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe kwa miezi minne kuanzia Oktoba mwaka jana katika jiji hilo lenye idadi kubwa ya watu, umebaini biashara ya aina hiyo ya pombe imeendelea kupamba moto, tofauti pekee ikiwa ni namna ya ufanyikaji wake na pia usiri uliotawala miongoni mwa wauzaji na wateja wao.

Serikali kupitia agizo lililotolewa Februari 2017 na Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, ilitangaza kupiga marufuku biashara ya pombe za viroba kuanzia Machi Mosi, mwaka huo, na hivyo yeyote anayekiuka amri hiyo halali kujiweka katika hatari ya kuchukuliwa hatua za kisheria.

Tangu wakati huo, operesheni kadhaa zimekuwa zikifanywa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazosimamia biashara na uhifadhi wa mazingira nchini kama vile Shirika la Viwango (TBS), Tume ya Ushindani (FCC) na Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Mazingira (NEMC).

Licha ya kuwapo kwa amri hiyo, uchunguzi wa Nipashe jijini Dar es Salaam umebaini mbinu mpya ya unywaji wa pombe hizo mitaani, baadhi ya wauzaji wakitumia chupa za chai na glasi ndogo zilizobatizwa majina mbalimbali na wauzaji na wateja wao.

Nipashe imebaini biashara ya pombe aina ya Konyagi, K-Vant na gongo imeshamiri kwenye vijiwe na stendi za daladala za jiji hilo la kibiashara na vilevi hivyo vinauzwa kwa bei ya chini kuanzia Sh. 500.

Gazeti hili limebaini baadhi ya wafanyabiashara wanaofahamika kwa kuuza uji, chai na kahawa, wamekuwa wakibeba vilevi hivyo kwenye chupa za chai na kuwauzia wateja bila mtu mgeni kutambua.

Uchunguzi wa Nipashe kwenye maeneo ya Ubungo, Kigogo, Mwananyamala, Mburahati, Manzese, Tabata na Kimara, ulibainisha wapigadebe, madereva, makondakta, wamebeba mizigo, waendesha maguta na wafanyabiashara ndogondogo, maarufu machinga, ndiyo wateja wakubwa wa pombe hizo na wanauziwa kwa kupimiwa kwenye glasi ndogo, ambazo wahusika wamezibatiza jina la 'kiduchu'.

"Sisi watumiaji wa pombe hizi tuna majina yetu ambayo kwa mtu mgeni si rahisi kuelewa, nikifika kwa muuzaji namwambia 'nipe panado' (jina la kibiashara la dawa za kutuliza maumivu), wewe utadhani ni kidonge, lakini kumbe ni hii kitu," alisema mmoja wa wapigadebe wa daladala eneo la Kimara huku akimwonyesha mwandishi glasi ndogo yenye pombe kali.

Jumanne Nasoro, mkazi wa Mabibo jijini, alisema amekuwa akiuziwa pombe aina ya Konyagi na gongo kwenye vibanda vya kahawa na maduka ya mitaa mbalimbali ya eneo hilo.

"Pombe hizi mbona bado tunauziwa, sema kwa sababu wewe ni 'mwana' (si mtu hatari kwao), acha tukwambie tu, usione watu wanauza uji ukajua huo ni uji katika chupa zote, wanabeba na chupa za gongo na Konyagi. Mjini hapa usishangae," Nasoro alibainisha.

Alisema pombe kali zinauzwa kwa mtindo huo ili kuendelea kulipata soko la vijana ambao walizoea kunywa pombe aina ya viroba kabla ya amri ya serikali ya kupiga marufuku biashara hiyo.

Mfanyabiashara katika Stendi ya Manzese jijini, Frank Maziku, alisema wapigadebe na vijana wa mtaani wamekuwa wakiendelea kunywa pombe hizo za bei rahisi zinazouzwa kinyemela mitaani.

Alisema pombe huuzwa kwa usiri mkubwa kwenye vichochoro vya maeneo ya Manzese, lakini kwa watu waliozoeleka tu, ikiwa ni mbinu ya kuvikwepa vyombo vya dola. Alisema baadhi ya wauzaji huwa wanatembeza kwenye maeneo ya wazi wakiwa wamechanganya na biashara ya uji au kahawa, hivyo kuwa ngumu kwa mamlaka za udhibiti kutambua kinachoendelea.

"Serikali imepiga marufuku matumizi ya viroba, lakini huku mtaani bado zinauzwa sana. Inakuwa ngumu kutambua kwa sababu wanachanganya na biashara nyingine kama uji na kahawa," alisema.

Alisema wafanyabiashara wa pombe kali wamekuwa wakibuni mbinu mbalimbali za kuendesha biashara hiyo, baada ya serikali kupiga marufuku pombe za viroba.

Katika uchunguzi wake maeneo ya Tabata jijini, Nipashe ilibaini watumiaji wa aina hizo za pombe wamezibatiza jina la 'dawa ya kichwa'.

"Vijana wengi wanaingia kwenye vibanda wanakouza pombe aina ya gongo, Konyagi na K-Vant na wanauziwa kuanzia Sh. 500 hadi 1,000 kwenye glasi ndogo na wewe mtu mgeni huwezi kufahamu kwa sababu wanaagiza kwa majina wanayoyajua wao na wauzaji wao," Mariam Kapama, mkazi wa Tabata alisema.

Gabriel Kisanga, muuzaji wa moja ya baa za Kimara jijini, alisema wamekuwa wakipima pombe aina ya Konyagi na K-Vant kwenye glasi ndogo na kuuza kwa bei ya kuanzia Sh. 500.

"Hili siyo jambo la kushangaza, watu wengi sana tunawapimia na wala siyo tu ambao hawana fedha, wengine wana fedha, lakini wanataka kunywa kidogo, hivyo tunawapimia," alisema.

Alisema pombe hizo za kupimwa wakati mwingine huchanganywa na vinywaji vingine kama soda ili kupunguza makali.

Kisanga alidai watu wanapendelea utaratibu huo wa kupimiwa pombe kutokana na urahisi wa bei na hali ya ugumu wa maisha ya sasa.

"Hii Konyagi ukimpimia mtu anakunywa na analewa kwa gharama nafuu, lakini bia inamgharimu mnywaji kununua nyingi ili kulewa, na hali yetu ya maisha kama unavyojua," alisema.



Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

### MCHUNGAJI AONYA

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Richard Hananja, alisema suala la unywaji wa pombe za kienyeji na pombe kali mitaani limechukuliwa la kawaida ilhali lina madhara makubwa kwa jamii.

Mchungaji Hananja ambaye ni mlezi wa vijana walioacha kutumia dawa za kulevya na pombe, alisema jamii haipo tayari kuripoti wauzaji na wanywaji, ambao wanachukuliwa kuwa watu wa kawaida wakati wanafanya vitendo ambavyo ni janga kwa taifa.

Alisema jitihada za serikali kudhibiti biashara hiyo kwa kupiga marufuku utengenezaji na uuzaji wa aina hizo za pombe, hazitazaa matunda kwa jamii iliyoharibika na isiyo na maadili.

"Jamii ipo bize kuwaza uchawi wa kulogwa ilhali uchawi wa wazi ni wauzaji wa pombe hizi zinazokatisha na kuharibu maisha ya vijana wengi nchini," alilalamika.

Mchungaji Hananja alisema kumekuwapo na mmomonyoko wa maadili unaochagizwa na watu kuuza na kuvuta bangi na pombe kali hadharani, huku jamii ikiwaona bila kuchukua hatua za kuwadhibiti na kuvipa taarifa vyombo vya dola.

"Nafikiri mifumo ya kuilinda jamii inayopaswa kutoa taarifa haijawekwa sawa, ndiyo sababu imekaa kimya, inashuhudia haya lakini ipo kimya," alisema.

**■Usikose kufuatilia kesho madaktari bingwa wakibainisha madhara yatokanayo na unywaji wa pombe za aina hiyo.**

# Polisi yaendelea uchunguzi tukio kulishwa sumu Mangula

**Na Mwandishi Wetu**

KAMANDA wa Polisi wa Kanda Maalumu, Lazaro Mambosasa, amesema wanaendelea na uchunguzi wa tukio la Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Philip Mangula, kulishwa sumu.

Alikuwa akijibu swali la waandishi wa habari jana, jijini Dar es Salaam kuhusiana kama kuna aliyekamatwa au kinachoendelea kwenye tukio hilo la kulishwa sumu kwa kiongozi huyo.

"Upelelezi unaendelea na tutakapokamilisha tutawaeleza, masuala ya upelelezi tunakusanya kwa ajili ya kutoa ushahidi mahakamani, yakikamilika tutaeleza na watu waliokamatwa tutawaeleza," alisema.

Machi 9, mwaka huu, Kamanda Mambosasa alisema, taarifa walizozipata Februari 28, mwaka huu, baada ya Mangula kudondoka ghafla katika ofisi ndogo zilizopo Lumumba baada ya kumaliza kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu Taifa, ni kuwa aliwekewa sumu ingawa haijajulikana aliwekewa wapi.

Alisema polisi wanaendelea na upelelezi kuhusu namna ambavyo sumu hiyo iliingia mwilini na kwamba watachukua hatua kali kwa yeyote atakayebainika kuhusika.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu kuhusu maendeleo ya afya ya kiongozi huyo, Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM, Hamphrey Polepole, alisema

"Ninachofahamu mzee (Mangula) anahitaji mapumziko zaidi na sasa anaendelea na mapumziko," alisema bila kufafanua zaidi.



Magugu maji yakiwa yamezingira sehemu maalumu za kuondokea boti za watalii wa ndani jana, huku jitihada za kuyaondoa zilisimamiwa na Mhifadhi Mkuu, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa Hifadhi ya Taifa ya Saanane, Eva Mallya. Magugu hayo yaliyotapakaa kwenye Ziwa Victoria huletwa na upepo pamoja vichaka na baada ya muda hupelekwa sehemu nyingine. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Serikali kujenga maeneo maalum ya viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZA), imepanga kujenga maeneo maalum ya viwanda kama sehemu ya kufungamanisha kilimo na viwanda, sekta ambazo ni chanzo kikubwa cha kuzalisha ajira.

Akiongea na wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, iliyotembelea eneo la Kurasini lililopangwa kujengwa kituo kikubwa cha biashara mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema serikali inalenga kujenga na kuendeleza eneo maalumu la viwanda (industrial park) kila mkoa ikiwa ni fursa ya kuvutia uwekezaji na kutengeneza ajira mpya kwa wingi.

"Napenda kuwahakikishia wanakamati wote mliokuja kutembelea eneo hili la mradi kuwa serikali imejipanga vizuri na imeshaanza hatua mbalimbali ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa kituo hiki kikubwa cha biashara nchini na katika eneo la Afrika Mashariki unaanza mara moja," alisema na kuongeza kuwa mradi huo unaotekelezwa na EPZA utafungamanisha kilimo na viwanda ili kuongeza kipato cha wakulima.

Akizungumza katika ziara hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Suleiman Saddiq, alisema ni muhimu mradi huo kuanza kwa wakati ili uweze kuchangia na kuongeza kipato cha wakulima na uchumi wa nchi.

"Mradi huu ni vizuri utekelezwe kwa haraka ili kuwapa wakulima wetu uhakika wa soko na ongezeko la kipato na pia kufanya mchango wa sekta hii inayoajiri asilimia zaidi ya 70 ya Watanzania na asilimia 26 ya pato la taifa liweze kuongezeka zaidi," alisema.

Waziri Bashungwa aliihakikishia kamati hiyo kuwa baada ya kupata hati ya eneo la kujengwa mradi wa Kurasini, Hazina itatoa fedha kwa ajili ya kuanza maandalizi ya mradi na hasa ujenzi wa ukuta kuzunga eneo hilo.

Miradi mingine ya ujenzi na uendelezaji wa maeneo maalum ya viwanda ni pamoja na Kahama mkoani Shinyanga, Mtwara na Songwe.

Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Kanali mstaafu Joseph Simbakalia, alisema kuna umuhimu wa kujenga na kuendeleza maeneo maalumu ya viwanda mengi zaidi nchini kwa vile nchi ya Tanzania ni kubwa na pia kutosheleza soko la ndani na la ukanda wa Afrika Mashariki.

Katika kituo kikubwa cha biashara cha Kurasini, tayari bodi nne za mazao ikiwa ni pamoja na chai, kahawa, mazao mchanganyiko na matunda wameonyesha nia ya kushiriki katika mradi huo.

Maandalizi ya kuanzishwa kwa kituo cha kukusanya na kufanya mauzo ya kahawa kwa mnada badala ya kupeleka Mombasa tayari yameanza na kufikia hatua nzuri.


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent& Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK (TZ) LTD** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa MNADA WA HADHARA.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na | JINA LA MDAIWA | JINA LA MMILIKI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **KILIMOTIVE(T) COMPANY LIMITED** | **KILIMOTIVE(T)COMPANY LIMITED** | Shamba la mpunga lililopo Ilula wilayani Kwimba Mwanza- lenye ukubwa wa **HEKTA 1577.95** | **4/04/2020** |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537

AU

Mkurugezi Mtendaji
Equity Bank (Tz)Limited
Head Office,
Ohio street-Golden Jubilee Towers,
P.O. BOX 110183,
DAR ES SALAAM
MOBILE; + 255 768985500
Email: info@equitybank.co.ke

156695



UNHCR
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**REQUEST FOR PROPOSAL: No. RFP/2020/SUP/001**

**FOR THE ESTABLISHMENT OF FRAME AGREEMENTS FOR PROVISION OF ROAD CARGO AND PASSENGERS TRANSPORT SERVICE IN TANZANIA.**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Tanzania, invites qualified suppliers to make a firm offer for the establishment of Frame Agreement(s) for the provision of Road Cargo and Passengers transportation services (referred to hereinafter as services).

UNHCR may award Frame Agreement(s) with initial duration of 2 (two) years, potentially extendable for a further period of 1 (one) year. The successful bidder(s) will be requested to maintain their quoted price proposal for the duration of the Frame Agreement(s).

**2. Eligibility:**

Service providers or traders duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's needs are invited to participate in the bidding process.

The tender documents can be collected from the following UNHCR Offices:

UNHCR Representation Office Tanzania
Plot 1658 Masaki, Rufiji Street
P.O Box 2666 - **Dar es Salaam, Tanzania**

UNHCR Sub- Office Kibondo
Kabigwa (Near TANESCO)
P.O. Box 49
**Kibondo**

UNHCR Field Office Kasulu
Kimobwa (Mlimani Area)
P.O. Box 332 - Kasulu,
**Kigoma**

UNHCR Field Unit Mwanza
Mwanza Airport
P.O. Box 2273 – **Mwanza**

215661402

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

| | |
|---|---|
| Deadline for receiving requests for clarification | Tuesday 22nd March 2020 at 23.59 hours EAT |
| Suppliers' conference meeting | Wednesday 25th March 2020 at 11.00hours EAT |
| Deadline for submission of offers | Tuesday 14th April 2020 at 16.00 hours EAT |

*UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mashabiki chukueni tahadhari maambukizi corona viwanjani

**SHIRIKA** la Afya Duniani (WHO) limetangaza virusi vya corona 'coronavirus' vinavyojulikana kama CONVID-19 kuwa janga la kimataifa 'global pandemic'. Hatua hiyo ni kutokana na virusi hivyo vinavyosababisha mafua, kukohoa na homa kali ya mapafu kutokuwa na kinga, huku vikienea kwa kasi kubwa.

Tayari zaidi ya mataifa 123 duniani kote yametangazwa kuwa na maambukizi ya virusi hivyo vilivyoanzia mjini Wuhan nchini China huku vifo vilivyoripotiwa kutokana na janga hilo vikiwa ni takriban 5,800 na wagonjwa wakiwa zaidi ya 156,000 .

Kutokana na janga hilo, Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), lile la Ulaya (Uefa), Amerika Kusini (CONMEBOL) na Afrika (Caf), yameahirisha michuano mbalimbali iliyokuwa ifanyike mwezi huu kwa kuhofia usalama wa afya za wachezaji na mashabiki.

Awali mashirikisho ya soka katika nchi mbalimbali zilizoanza kuripotiwa kuwa na mlipuko wa virusi hivyo, ikiwamo China, Italia na kwingineko, yalianza kuchukua hatua kwa mechi kuchezwa bila mashabiki kabla ya kuamua kusimamisha kabisa ligi zao.

Hatua hiyo ikapokelewa na nchi nyingi za Ulaya ikiwamo ligi pendwa duniani, Ligi Kuu England pamoja na Hispania, Ujerumani na kwingineko.

Kwa Caf imezuia mechi zote za shirikisho hilo zikiwamo za kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021 ambapo Machi 27 timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars ingesafiri kwenda kuivaa Tunisia kabla ya siku tatu baadaye kurudiana hapa nchini.

Lakini Caf inaendelea kufanya uchunguzi ili kujiridhisha zaidi endapo michuano ya fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zinazotarajiwa kufanyika nchini Cameroon Aprili 4-25, mwaka huu, zifanyike ama laa.

Hiyo ni kutokana na maambukizi ya virusi vya corona kuripotiwa kuingia nchini Cameroon kwa sasa, wakati huu vikiripotiwa pia kubisha hodi kwa baadhi ya nchi za Afrika Mashariki ikiwamo Kenya, Burundi.

Hata hivyo, Tanzania ina kila sababu ya kumshukuru Mungu kwani hadi sasa hakujaripotiwa kuwa na mgonjwa yeyote aliyepata maambukizi hayo wakati huu ambao Rais John Magufuli akiwataka Watanzania kuchukua tahadhari mapema.

Nipashe tunaungana na Rais Magufuli katika kutoa msisitizo huo kwa kila mtu kuchukua tahadhari hususan katika mikusanyiko mikubwa kama viwanjani.


Ni wazi Caf inaweza pia kusogeza mbele michuano ya CHAN, hivyo kutoa fursa kwa wachezaji wa Taifa Stars waliopo kambini kujiandaa na fainali hizo kurejea katika klabu zao kuendelea na mechi za Ligi Kuu na mashindano mengine kwa ngazi ya klabu.

Na kwa sababu Tanzania corona haijabisha hodi, tunahitaji kuona mashabiki viwanjani wakichukua tahadhari zote stahiki mapema hususan kutosalimiana kwa kupeana mikono, kukumbatiana, huku wakivaa vikinga pua na mdomo.

Tunasema hivyo kutokana na kutambua kinga ni bora kuliko tiba, hivyo kuchukua tahadhari mapema kutasaidia, hasa kutokana na wimbi la wahamiaji haramu ambao wanaweza kuingia nchini wakiwa na maambukizi hayo bila kubainika.

Tunaamini kila mmoja atachukua hatua huku wote tukishirikiana kutoa elimu na kumuomba Mungu atuepushe na janga hili linaloitikisa dunia, lakini ni wakati wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuandaa utaratibu wa kutoa elimu namna ya kujikinga na kuchukua tahadhari wakati na kabla ya kila mechi kuanza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Gwambina karibuni Ligi Kuu, ila mjipange

**INAHITAJI** pointi sita tu kati ya mechi tano ilizobakiza ili kupanda moja kwa moja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hiyo ni timu ya Gwambina ambayo inaongoza kwenye Kundi B na kuwa ni timu iliyo karibu zaidi kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa imeziacha timu zingine kwa mbali.

Gwambina FC timu yenye maskani yake Misungwi mkoani Mwanza, awali ilikuwa inajulikana kama JKT Oljoro ya Arusha ambayo imeshawahi kucheza Ligi Kuu, lakini ikashuka.

Baadaye ikabadilishwa jina na kuitwa Arusha United ambayo nayo iliuzwa mjini Mwanza mwanzoni mwa mwaka jana na kubadilishwa jina na kuwa Gwambina FC.

Moja kati ya vitu vya kuvutia kwa klabu hii ni kwamba ni timu ambayo ina uwanja wake, hivyo haitoiwia tabu kwa mechi za Ligi Kuu kuchezwa hapo.

Ilishangaza mashabiki wengi wa soka nchini ilipoialika Simba Juni mwaka jana kwenda kufungua uwanja huo ambao unaonekana kabisa unakidhi vigezo vyote, si vya Shirikisho la Soka nchini (TFF) tu, lakini hata vya Shirikisho la Soka Afrika (Caf) na hata duniani (Fifa).

Hivi majuzi, wengi waliishuhudia ikicheza dhidi ya Yanga kwenye Kombe la FA. Yanga ilishinda bao 1-0, lakini Gwambina iliipa wakati mgumu Yanga na ilibaki kidogo tu ngoma iende kwenye matuta.

Inaonekana ni timu iliyojipanga na yenye dhamira ya dhati. Klabu zinazoonekana kujipanga kisawasawa kama Gwambia FC, ndiyo kwa kiasi kikubwa zinatakiwa kwenye Ligi Kuu kwa ajili ya kutoa ushindani wa nguvu na wa kweli kwa ajili ya kuifanya ligi yetu kuwa bora, tofauti na baadhi ya klabu ambazo zinaonekana zipo tu kwenye ligi.

Kwenye ligi hii zinahitajika timu kama Gwambina na Namungo kwa ajili ya kupambana kuutafuta ubingwa wa Tanzania Bara tangu mwanzo wa ligi hadi mwisho na si kucheza ligi kwa ajili ya kutafuta pointi za kubaki, ili kuwapo tena msimu ujao.

Pamoja na yote haya, natoa angalizo kwa Gwambina FC kuwa inapokuja kwenye Ligi Kuu ijipange na ibadilike kwani itakachokikuta kwenye Ligi Kuu, si kile kilicho kwenye Ligi Daraja la Kwanza.

Nimeiangalia mechi dhidi ya Yanga na kubaini kuwa pamoja na kuwa na wachezaji wazuri na baadhi wazoefu, bado inacheza mpira wa 'kishule-shule' sana, hivyo isitarajie kuwa unaweza kuisaidia kwenye Ligi Kuu.

Gwambina inabidi itafute baadhi ya wachezaji wazoefu na wenye uwezo wa kusaka matokeo zaidi na si kupaka sana rangi mipira.

Ikija na aina ile ya mfumo basi kazi itakuwa ngumu, lakini inahitaji marekebisho kidogo kupata baadhi ya wachezaji wa kazi, wenye kujituma, nguvu na kupambana ili wakiungana na waliopo waweze kuifanya kuwa timu bora.

Sina shaka sana na pesa za usajili wa wachezaji wazuri kwenye klabu hiyo, hivyo nategemea kutakuwa na mabadiliko.


Viongozi wa klabu hiyo nao wanatakiwa wawe na nia ya kweli ya kuendeleza soka na si kwamba wanafanya hivyo kwa sababu za kisiasa, labda wanataka kugombea ubunge kwenye uchaguzi huu mkuu.

Tumeona timu nyingi za daraja la kwanza zikilazimishwa kupanda Ligi Kuu kwa sababu ya watu kutaka ubunge, lakini walipofanikiwa walizitelekeza timu na kuanza kuhaha zikiwa hazina tena wafadhili hadi zinaanza kuombaomba kwa wananchi.

Nia iwe ya dhati kutaka kuufanya mkoa wa Mwanza uwe juu kisoka na kulisaidia taifa hili kuwa na klabu bora. Hili ndilo litakaloifanya Gwambina FC iingie Ligi Kuu na kuwa tishio, lakini kama kuna watu wanaipandisha kwa maslahi yao na wakishayapata wanaitelekeza, basi tutashuhudia mlango ilioingilia ndiyo itakaotokea.

MJADALA

# Mbeya City na Ndanda FC zinapokumbuka shuka asubuhi




**Na Adam Fungamwango**

**KUNA** baadhi ya klabu kwenye Ligi Kuu zinashangaza sana. Zinapoanza ligi huwa hazikomai na zinaonekana kucheza kilelemama. Lakini hali ikishakuwa mbaya, basi ndiyo utaona zinatumika nguvu kubwa kuhakikisha zinashinda mechi zilizobaki ili ziendelee kubaki Ligi Kuu.

Mfano wa timu hizo ni Ndanda FC ya Mtwara. Timu hii ilipanda daraja na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2014/15. Msimu wake mzuri zaidi ulikuwa ni 2015/16 ilipomaliza ligi ikiwa nafasi ya tisa kwa pointi 35.

Lakini misimu yake yote imekuwa ikisubiri mechi za mwisho ili kujua kama imebaki au imeshuka daraja.

Na kwa bahati nzuri, Ndanda FC imekuwa ni timu yenye ngekewa, kwani mara zote imekuwa ikifanikiwa kubaki Ligi Kuu, baada ya mechi za mwisho kumalizika na kupigwa mahesabu timu ipi ina pointi chache kuliko zingine au mabao machache. Ndanda imeonekana kama imezoea aina hii ya maisha, kwani hata msimu huu haikuanza vizuri mzunguko wote wa kwanza.

Kama kawaida ya viongozi wa mkoa wa Mtwara, walipoona timu iko hatarini wakaanzisha mkakati wa kuwaweka pamoja wananchi wote wa mkoa huo, pamoja na kuisaidia kwa hali na mali ili ibaki Ligi Kuu.

Hilo limeanza kuisaidia timu hiyo kwa kiasi fulani, kwani imeweza kushinda mechi kadhaa mfululizo, licha ya kwanza Jumamosi iliyopita ilikutana na kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania ugenini.

Kwa vyovyote vile, aina hii ya kuendesha timu haiwezi kuisaidia Ndanda, kwani ipo siku inaweza kujikuta inashuka daraja.

Nadhani Ndanda ijifunze kutoka kwa majirani zao Namungo FC ambayo yenyewe tangu mwanzo imeanza na moto na inamaliza hivyo hivyo na pamoja na ugeni wao, lakini si moja kati ya timu ambayo inasubiri mechi za mwisho ili kufanyike juhudi za kuinusuru.

Mbeya City ni timu iliyopanda Ligi Kuu na kuanza kucheza msimu wa 2013/14. Ilipanda na kuanza kwa mbwembwe mno. Lakini pia ilikuwa ni moja kati ya timu tishio kwenye ligi kwa timu zote kubwa na ndogo zinazoshiriki, ikisaidiwa na mashabiki wake waliokuwa na hamasa kubwa, wakisafiri na timu yao popote pale inapokwenda kucheza nchini Tanzania.

Ni timu ambayo imekuwa ni mfano kwa timu nyingi ambazo zilipanda baadaye kwenye Ligi Kuu kutaka kuiga inavyofanya Mbeya City. Hata hivyo, ikawa kama ni mgonjwa wa muda mrefu anavyoanza kupungua mwili taratibu. Taratibu nayo ikaanza kuwa dhaifu. Msimu huu ndiyo umekuwa mbaya zaidi kwani Mbeya City kwa mara ya kwanza nayo inapigania isishuke daraja.

Cha kushangaza ni kwamba hali hii ilionekana tangu mwanzo, lakini baadhi ya viongozi wa mkoa walikuwa kimya, lakini sasa ndiyo wameibuka na kupanga mikakati.

Moja ya mikakati mimgi ni kuruhusu wanafunzi wa shule za msingi mbalimbali Mbeya Mjini kuingia Uwanja wa Sokoine bure kwa ajili kuipa hamasa timu yao.

Halafu inaonekana kama vile hakuna maandalizi au semina kwa wanafunzi hao, kwani nilishuhudia mechi yao dhidi ya Mbao FC wanafunzi hao wakishangilia chochote kile kinachotokea, kiwe kizuri kwa timu yao au kibaya.

Walikuwa wakishangilia hata mchezaji wa Mbeya City anapopiga mpira juu, au anapokosea au kuurudisha mpira nyuma, walishangilia timu yao ilipokuwa inashambulia na hata wakati mwingine kushambuliwa. Walikuwa wakishangilia baadhi ya vitu ambavyo vingine vilikuwa ni hatari kwa timu yao. Ina maana wengi au baadhi yao hawajui chochote kuhusu soka. Wameletwa tu hapo kisiasa, bila hata kuwekwa chini na kufundishwa vitu mbalimbali kuhusu soka.

Hawakufanana kabisa na wanafunzi wa Alliance FC ambao wakiwa uwanjani kwao unaona kabisa kuwa hawa wanaufahamu mkubwa kuhusu soka, wa kike na wa kiume. Wanahamasisha timu yao. Wachezaji wao wakiwa na mpira wanapiga kelele na kushangilia. Wanawazomea wapinzani wanapokuwa na mpira au wanapokosa goli. Kusema kweli wanawasaidia sana Alliance wakiwa nyumbani, tofauti na wale wa Mbeya City.

Hii yote ni hali ya kukurupuka wakati maji yameshazidi unga. Ni kweli kuwa kwenye ligi ni lazima ziwapo timu ambazo zitashuka daraja, lakini zingine zinaonekana kuwa zinataka kushuka kizembe.

Ndanda haijajifunza tu miaka yote jinsi gani ya kucheza Ligi Kuu na kupata pointi nyingi za mwanzoni na kuepuka presha za mwishoni?

Mbeya City ambayo imeathiriwa zaidi na siasa, imekuwa ikionywa mara kwa mara kujirekebisha kuhusu mwenendo wao huo, na kweli sasa yamewakuta.

Kwa sasa timu zao zinakumbuka shuka kumekucha. Hali ni mbaya. Inawezekana zikapona, lakini kwa machozi, jasho na damu ambayo hayakuwa na ulazima. Zikishuka basi viongozi wa klabu hizo hawatokuwa na wakumlilia, kwani wameyataka wenyewe. Kwa sababu timu hizi hazishuki kwa sababu ya udhaifu wa wachezaji ndani ya uwanja, ila ni matatizo yaliyopo kwa viongozi wao.


## NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.

MAENDELEO BANK PLC Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa wadaiwa wanaotajwa hapa chini, walipe madeni wanayodaiwa.

Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) zao kwa mnada wa hadhara.

Mnada utafanyika tarehe husika kuanzia saa 4 asubuhi na kuendelea.

| S/N | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA | KAMPUNI YA UDALALI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Michael Silvan Assey. | Nyumba ya makazi yenye leseni no ILA/KTD/KTK31/15 iliyopo eneo la kitunda Manispaa ya Ilala. | 05/04/2020 | Msolopa Investment Co.Limited |
| 2 | Elice Entreprises Ltd. | Nyumba ya makazi yenye leseni no.KND029120 iliyopo eneo la Makuburi Manispaa ya Ubungo. | 04/04/2020 | Msolopa Investment Co.Limited |
| 3 | Omary Augustino Zacharia | Nyumba ya makazi yenye hati iliyopo eneo la Yombo Manispaa ya Temeke. | 04/04/2020 | Msolopa Investment Co.Limited |
| 4 | Sia Stophery Kinjoph | Nyumba ya makazi yenye leseni no.KND028220 iliyopo eneo la Mwananyamala Manispaa ya Kinondoni. | 03/04/2020 | Msolopa Investment Co.Limited |
| 5 | Magdalena Cletus Mgombere | Nyumba ya makazi yenye hati no. 74730,kiwanja no.35 ,kitalu no.1, eneo la Bunju Manispaa ya Kinondoni. | 31/03/2020 | Msolopa Investment Co.Limited |
| 6 | Mark SamwelRhombo | Nyumba ya makazi yenye hati ya mauzianoiliyopo eneo la Msigani Manispaa ya Ubungo. | 04/04/2020 | Best group(T) Limited |
| 7 | Enea Godfrye Basaya | Nyumba ya makazi yenye hati ya mauzianoiliyopo eneo la kwanyoka Manispaa ya Temeke | 11/04/2020 | Best group(T) Limited |
| 8 | Sakina Hassan Mshihiri | Nyumba ya makazi yenye leseni iliyopo eneo la Ubungo msewe Manispaa ya Ubungo. | 09/04/2020 | Best group(T) Limited |
| 9 | Anania Anyimike Kasisi | Nyumba ya makazi yenye hati no.143884 iliyopo eneo la Tabata kinyerezi Manispaa ya Ilala. | 21/03/2020 | Best group(T) Limited |
| 10 | Mponjoli William Mwakabana | Nyumba ya biashara yenye hati ya makazi no.TMK/TDK/KLH4/151 eneo la Tandika Manispaa ya Temeke. | 11/04/2020 | Best group(T) Limited |
| 11 | Prisca J. Mushi | Nyumba ya makazi yenye hati ya mauzianoiliyopo eneo la Malambamawili Manispaa ya Ubungo. | 09/04/2020 | Best group(T) Limited |
| 12 | Yusuph Hamis Kitumbo | Gari aina ya YUTONG zenye namba za usajiri T 435 CVL na T 433 CVL | 31/04/2020 | Best group(T) Limited |
| 13 | In the rise canteen/Milton Loth Shango | Nyumba yenye hati no 70135,kiwanja no.53,kitalu no.9 iliyopo eneo la Bunju manispaa ya Kinondoni | 31/04/2020 | Best group(T) Limited |

### MASHARTI YA MNADA

1. Nyumba zitauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakaeshinda atalipa malipo ya awali ya 25% ya bei itakayofikia siku ya mnada na 75% katika muda ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote zakubadilisha hatimiliki, Kutwaa Nyumba/ Kumtoa mmilikiwa awali (ikiwa bado hajatoka hadi wakati wa mnada) na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuonana kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**

**MAENDELEO BANK PLC**
**HQ LUTHER HOUSE**
**P.O BOX 216**
**DAR ES SALAAM.**
**MOBILE 0688699289**

**BEST GROUP(T) LIMITED**
**P.O. BOX 1088 DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/+ 255 766-309913**

**MSOLOPA INVESTMENT COMPANY LIMITED**
**P.O.BOX 40561-DAR ES SALAAM**
**MOB:0688 332233, 0767 666767, 0657363933**

2156669102

# Tabora kumenoga, maji Ziwa Victoria yafika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HATIMAYE mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria umefika mkoani Tabora na tayari wananchi wameanza kunufaika na huduma hiyo.

Mradi huo wa Sh. bilioni 600, utanufanisha wakazi milioni 1.8 katika vijiji zaidi ya 90 maeneo yote ya mradi kuanzia Kanda ya Ziwa hadi Tabora mjini, Igunga na Nzega.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, alisema mradi huo unapita zaidi ya kilometa 300.

"Leo hii tunapozungumza kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu wananchi wa eneo la nchi kavu la Tabora wanaoga, wanakunywa wananufaika na maji kutoka Ziwa Victoria, ambao unatoka zaidi ya kilometa 300 ni mradi mkubwa sana," alisema.

Alisema kazi inayofanyika kwa sasa ni kupeleka maji hayo kwenye vijiji hivyo.

"Huu mradi baada ya miaka mingi hatimaye maji yamefika Tabora, Igunga hadi Nzega sasa hii ni habari njema, maji yamefika Tabora naambiwa kuna shughuli kubwa imeandaliwa watatualika tutaenda kuona kuna fiesta ya aina yake," alisema.

Dk. Abbas alisema tangu nchi iumbwe, wananchi wa Tabora hawajawahi kupata maji kutoka ziwa hilo, lakini sasa yamewafikia.

"Wananchi wa maeneo hayo waanze kuomba kuunganishiwa maji kwa kuwa tayari yameyafikia kwenye eneo husika," alisisitiza.

Alisema serikali imeendelea kuboresha huduma ya majisafi na salama vijijini na mijini na utekelezaji wa miradi 875 unaendelea ukijumuisha miradi 802 ya maji vijijini na miradi 73 ya maji mijini.

"Tunatarajia hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu tutakuwa tumefikia azma ya kufikia lengo la asilimia 85 vijijini na mijini asilimia 95," alisema.

Ujenzi miundombinu

Dk. Abbas alisema Serikali ya Tanzania na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), zimesaini mikataba mitano inayohusu utekelezaji wa mradi mitatu ya kimkakati kwa mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 495.59 ambayo ni sawa na Sh. trilioni 1.14.

Alisema fedha hizo zitatekeleza ujenzi wa mradi ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato jijini Dodoma kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 271.63, ujenzi wa barabara ya Bagamoyo - Horohoro - Lungalunga - Malindi kwa kiwango cha lami (kilomita 120.8) kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 168.76.

"Pia kiasi cha Dola za Marekani milioni 55.2 kwa ajili ya programu ya utawala bora na kuendeleza sekta binafsi," alisema.

Ripoti ya IMF

Ripoti ya IMF iliyotolewa Machi 5, mwaka huu, Dk. Abbas alisema Shirika la Fedha Duniani (IMF), lilikamilisha taarifa yake ya tathmini kuhusu uchumi wa Tanzania na kusisitiza kuwa uchumi wa Tanzania uko imara.

"IMF wanafurahishwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, mfumuko wa bei kuwa chini ya asilimia tano, mauzo ya bidhaa nje ya nchi kuongezeka, na kuongezeka kwa kasi ya benki kutoa mikopo kwa sekta binafsi na kuwa na deni la taifa ambalo ni himilivu," alisema.

Vile vile, alisema IMF imevutiwa na vita dhidi ya rushwa na juhudi za serikali kukusanya kodi.

"Shirika hilo lilitoa mapendekezo kwa Tanzania ikiwamo kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji, kuzingatia mipango inayolenga kupunguza au kuondoa malimbikizo ya matumizi na kuendelea kuweka vipaumbele kwenye sekta za elimu, afya na miundombinu ili kupata maendeleo ya kijamii na kuchangia ukuaji wa uchumi," alisema.

Migogoro ya ardhi

Dk. Abbas ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, alisema serikali imeendelea kutatua migogoro ya ardhi na hadi, kufikia Machi 2020, jumla ya migogoro 10,000 imetatuliwa.

Kuhamia Dodoma

Msemaji huyo alisema watumishi 15,361 wa wizara na taasisi za serikali wamehamia Dodoma na ujenzi wa awali wa ofisi za serikali katika mji wa serikali, Mtumba umekamilika.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Kemilembe Lwota, akitoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Geofrey Mwangulumbi (aliyevaa kaunda suti), wakati kamati yake ilipokwenda kukagua mradi wa upangaji na upimaji ardhi katika manispaa hiyo, jana mkoani Shinyanga. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

## TBS yatoa elimu viwango wilaya 3

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limemaliza kampeni ya kutoa elimu kwa umma katika wilaya za Mpanda, Rungwe na Ludewa na kufanikiwa kuwafikia wananchi zaidi ya 8,000.

Kampeni hyo ilihusu usajili wa majengo ya chakula na vipodozi, umuhimu wa kusoma taarifa zilizopo kwenye vifungashio vya bidhaa ikiwamo muda wa mwisho wa matumizi wa bidhaa.

Akizungumza wakati wa kampeni hiyo Mkaguzi wa TBS, Ernest Simon, aliwahimiza wananchi kujenga utamaduni wa kununua bidhaa zilizothibitishwa ubora na TBS, ili kuepuka hasara kwa kupoteza fedha na kuwa hatarini kupata athari za kiafya.

"Kampeni hii imeweza kuwafikia walengwa zaidi ya 8,000 kati yao wajasiriamali wakiwa ni 64, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 4,381 na wananchi 3, 658," alisema Simon.

Simon aliwataka wafanyabiashara kuhusiana na umuhimu wa kusajili majengo yao kupitia mfumo unaopatikana kwenye tovuti ya shirika hilo na wananchi waendelea kutoa taarifa kupitia mawasiliano waliyopewa pale wanapogundua uwapo wa bidhaa hafifu katika soko.

Wakati wa kampeni hiyo maofisa wa shirika hilo walipata fursa ya kutoa semina kwa wajasiriamali wanaojihusisha na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwamo za nafaka, sabuni, mikate, maziwa, pilipili, siagi ya karanga, korosho, mvinyo, mafuta ya kula, asali, batiki, vikoi na unga lishe.

Kampeni hiyo ambayo ni endelevu imefanyika katika wilaya hizo kuanzia mwanzoni mwa wiki iliyopita kwenye masoko, stendi, minadani na maeneo mengine ya wazi ikihusisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na wananchi kwa ujumla.

# Waumini wapewa elimu kujikinga corona

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAUMINI wa Kanisa la Neema ya Ukombozi kwa Mataifa yote, lililopo maeneo ya Lubaga, Shinyanga mjini, wamepewa elimu ya tahadhari ya kujikinga na virusi vya corona, ili wasiambukizwe na kuleta madhara.

Elimu hiyo ilitolewa jana na Mganga Mkuu wa Manispaa ya Shinyanga, Dk. Lusajo Mwakajoka.

Alisema elimu hiyo wameanza kuitoa kwenye makundi mbalimbali yenye mikusanyiko ya watu zikiwamo sehemu za ibada, ili wapate kuwa salama na kutoathiriwa na virusi hivyo na visiingie Tanzania.

Aliwataka waumini wa kanisa hilo waepukane na tabia ya kushikana mikono wakati wa kusalimiana, wanawe mikono mara kwa mara kwa kutumia sabuni na maji yanayotiririka, wasipige chafya bila ya kuziba pua kwa kitambaa, waepuke safari za nje ya nchi zisizo za lazima, pamoja na kubusiana.

"Nawaomba waumini wa kanisa hili mkawe mabalozi kwa wenzenu, na elimu tunayoitoa hapa muizingatie sana, janga la virusi hivi vya corona ni la taifa zima, hivyo mkichukua tahadhari mapema, virusi vya corona havitaweza kuingia hapa nchini Tanzania tutavisikia kwa nchi za wenzetu kwa sababu vimeshafika Kenya na Rwanda," aliongeza.

Naye Mratibu wa elimu ya afya kwa umma Manispaa ya Shinyanga, Mwita Thomas, alitaja dalili za ugonjwa huo kuwa ni kukohoa, kuumwa homa kali, mwili kuchoka, maumivu ya misuli, kupumua kwa shida, mafua makali, pamoja na kichwa kuuma.

Kwa upande wake nabiii wa kanisa hilo, David Nangale, alipongeza utolewaji wa elimu hiyo, huku akiongoza maombi ya kuliombea taifa lisiweze kupatwa na virusi hivyo na kuwataka viongozi wa kidini kutoka madhehebu mbalimbali waungane kuiombea nchi ibaki salama.

# Wasakwa kisa mkopo fedha za NSSF

**Ndalike Sonda,** KAHAMA

WILAYA ya Kahama mkoani Shinyanga imesema itawasaka popote walipo wanachama wawili wa Chama cha Ushirika Ibuka kinachojihusisha na shughuli mbalimbali katika mgodi wa Bulyahulu, kwa tuhuma za kuutumia ushirika huo kukopa Sh. milioni 80 kwenye Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) mwaka 2015.

Watu hao wanadaiwa pia kuwa baada ya hapo walikimbia na kuuza nyumba walizoweka dhamana.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Anamringi Macha, wakati akizungumza kwenye mkutano mkuu wa chama hicho katika Kata ya Bugarama Halmashauri ya Msalala.

Macha aliwataka wanachama hao ni Erasto Malugu ambaye alikopa Sh. milioni 50 na alipaswa kurejesha Sh. milioni 58, na Clement Ndilana aliyekopa Sh. milioni 30 na alitakiwa kurejesha zaidi ya Sh. milioni 32, na kwamba muda wa kurejesha ulikuwa ni miaka mitatu, lakini imeshapita.

Aidha, Macha alisema serikali inaendelea kuchunguza ili kuwabaini viongozi wa serikali ya kijiji waliohusika kushiriki kuhalalisha nyumba zilizokuwa zimewekewa dhamana ili nao wachukuliwe hatua za kisheria, huku akiwaonya waanachama wengine ambao hawajarejesha mikopo NSSF baada ya kukopa waanze kurejesha ndani ya mwezi mmoja.

Mkopo uliochukuliwa NSSF na wanachama takribani 74, ni shilingi milioni 750 wenye riba ya shilingi 123, 487,500, na mpaka sasa zinazodaiwa ni shilingi 679,399,166.61, na kwamba wapo waananchama watano waliomaliza mkopo wao.

Nao baadhi ya wanachama wa Ushirika wa Ibuka wameipongeza serikali kwa hatua za kisheria dhidi ya wale wanaotumia ushirika huo kwa manufaa yao binafsi.

Chama cha ushirika Ibuka kinaundwa na wananchama zaidi ya 400 wanaotoka katika vijiji 14 vinavyozunguka mgodi wa Bulyahulu ambacho ndio msimamizi wa shughuli mbalimbali ndani ya godi huo zinazofanywa na wananchi wanaozungukwa



Wafanyakazi wanaojenga daraja la Kiyegeya lililopo mkoani Morogoro, wakiwa katika maandalizi ya ujenzi wa daraja hilo, lililokuwa limezolewa na maji ya mvua. **PICHA: WUU**

# Wafanyabiashara wadogo wa kemikali wapata nafuu

**Na Mary Geofrey**

MAABARA ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) imeshusha gharama ya ada ya usajili wa kemikali kwa wafanyabishara wadogo wanaonunua bidhaa hiyo kwa matumizi yao ya uzalishaji mali kutoka Sh. 40,000 hadi Sh. 10,000. Lengo la punguzo hilo ni kuhamasisha wajasiriamali wadogo waliosajiliwa na Shirika la Viwanda Vidogo (Sido) na wanaotumia kemikali nchini kujisajili ili kutambulika na kuepusha uchepushaji wa matumizi ya kemikali yanayosababisha madhara mbalimbali kwa jamii.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam, wakati akitoa vyeti kwa wajasiriamali 176 waliofuzu mafunzo ya matumizi sahihi ya kemikali yaliyotolewa na mamlaka hiyo.

"Tumetangaza kushusha gharama za usajili wa kemikali kwa watumiaji ambao ni wafanyabiashara wadogo mliosajiliwa na Sido na mnaotumia kemikali kuzalisha bidhaa zenu lengo ni kuwahamasisha watumiaji wa kemikali kutambulika ili kupunguza matumizi yasiyo sahihi ya kemikali," alisema Dk. Mafumiko. Alisema wanaendelea kushirikiana na wajasiriamali kuhakikisha wanapunguza madhara ya kemikali katika jamii kwa kuendelea kuwahimiza kujisajili.

Kadhalika aliwataka wajasiriamali hao kujisajili kwa ajili ya kupata kibali cha kutumia kemikali ambacho ada yake ni Sh. 50,000 na kusajili maeneo yao ya kuzalishia bidhaa zao kwa kutumia kemikali kwa Sh. 50,000 ili kufanya kazi kwa majibu wa sheria zilizopo. Dk. Mafumiko pia aliwakumbusha wajasiriamali hao kuwa, matumizi ya mabaya ya kemikali yanaweza kusababisha majanga kwa jamii kama watu kumwagiwa tindikali na vilevi.

Alisema madhara ya kemikali zikitumiwa isivyokusudiwa ni kuwa sumu, silaha, kusababisha ajali, ulemavu, matatizo ya uzazi na saratani.

## Kesi za ndoa, kifamilia zapaa

**Na Romana Mallya**

KITUO cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake (WLAC), kimesema kesi za ndoa na za kifamilia zimeongoza ambapo kwa mwaka huu zilizoripotiwa kwao ni 602.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho, Theodosia Nshala, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati WLAC kikiungana na wanawake wanaowasaidia msaada wa kisheria kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani.

Alisema kauli mbiu za maadhimisho hayo mwaka huu inasema, "Kizazi chenye usawa kwa maendeleo ya sasa na baadaye."

Nshala alisema wameamua kusherehekea siku hiyo kwa kuungana na wanawake wenye uhitaji wa kisheria ambao hufika kituoni hapo kupata msaada ikiwa ni sehemu ya mafanikio waliyoyapata tangu kuanzishwa kituo.

"Takwimu za mwaka huu kuanzia Januari hadi sasa, zinaonyesha tumepokea kesi 602, za ndoa na za kifamilia ndizo zinazoongoza, zinahusiana na matunzo, talaka, mgawanyo wa mali, utengano na ulinzi wa mtoto au watoto," alisema.

Alisema tangu kituo hicho kianze kazi, wanawake waliosaidiwa ni takribani 60,000.

"Tunasherehekea kwa sababu mwanamke ni shujaa na mshindi na anaposhinda kesi ile mali akiipata husaidia watoto wake au jamii tofauti na upande wa pili.

Nshala alisema moja ya mafanikio yao ni kwamba wanawake ambao wamewasaidia wanaporudi kituoni huwa kama wanasheria kwa sababu ya kufahamu baadhi ya vifungu vya sheria hivyo kuweza kujisimamia.

"Siku hii ni muhimu kuitumia kutafakari usawa wa jinsia katika kuleta maendeleo ya jamii na taifa, hii ni pamoja kuleta uwiano wa usawa katika nyaja zote za kiuchumi, kisiasa na kijamii," alisema. Nshala alisema mara nyingi sherehe hizo zimekuwa zikiwaangalia wanawake wenye majina makubwa.

"WLAC tumeamua kusherehekea na wanawake ambao hawana majina makubwa, ambao hawajasoma na walikuwa hawajui haki na wajibu wao kisheria, lakini sasa wanajisimamia wenyewe mahakamani kuanzia Mahakama ya Mwanzo hadi Mahakama ya Rufani," alisema.

Rukia Lila (65), mkazi wa Magomeni jijini Dar es Salaam ni miongoni mwa wanufaika wa kisheria katika kituo hicho ambaye alisema alifika hapo baada ya kutokea mgogoro wa kifamilia wa mgawanyo wa nyumba ya urithi iliyoachwa na wazazi.

"Kituo hiki kimenisaidia sana kwenye masuala ya kisheria, wanawake hata kama umri wako ni mkubwa kiasi gani inapofikia hatua ya kudai haki angaikia, msijifungie ndani ukisema umri wangu umekwenda sasa mali ya nini, ni haki yako," alisema.

## Bosi TGNP awapa angalizo vijana mitandao kujamii

**Na Sabato Kasika**

VIJANA wametakiwa kutumia vizuri mitandao ya kijamii ili waweze kujiendeleza kielimu, kupata ajira na hata kufanyabiashara kwa ajili ya maendeleo yao.

Aidha, wamekumbushwa kuwa wao ni kizazi cha millenia, ambacho kinatakiwa kuwa makini katika matumizi ya mitandao hiyo kwa kutojiingiza kwenye mambo yasiyofaa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, ndiye aliyesema hayo jijini Dar es Salaam alipokuwa akizungumza katika maadhimisho ya Wanawake Duniani.

Maadhimisho hayo yaliandaliwa na Jukwaa la Wanaharakati Vijana linalohusisha wanafunzi wa vyuo mbalimbali nchini.

"Tumieni mitandao ya kijamii vizuri kwani kuna fursa nyingi zikiwamo za ajira, biashara na kujiendeleza kielimu siyo vinginevyo," alisema Liundi.

"Vilevile nimekuwa nikiingia mara kwa mara katika mitandao hiyo, lakini bahati mbaya wasichana ni wachache kuliko wavulana, ambao wanajitokeza kwa wingi kuchangamikia fursa mbalimbali mtandaoni," alisema.

Alisema, vijana ndiyo wenye kuamua baadaye yao, hivyo estudie utandawazi vizuri ili iweze kuwasaidia kwa kupata fursa mbalimbali.

Naye mmoja wa viongozi wa jukwaa hilo, Fatuma Ngamba, aliwataka vijana kushiriki katika harakati mbalimbali za kudai haki na usawa wa kijinsia.

"Tusione hili ni jukumu la watu fulani au kundi fulani bali tukiwamo sisi vijana, hivyo tuungane," alisema Fatuma.

Aliwataka vijana wa kike kutobaki nyuma katika harakati mbalimbali zenye lengo la kuwafanya vijana wa kike na wanawake kwa ujumla kushiriki kwenye nafasi za uongozi.

# Kampeni kulinda wasichana dhidi ya rushwa ngono yaja

**Na Yasmine Protace**

KAMPENI ya safari salama kwa wasichana na wanafunzi bila rushwa ya ngono inawezeka, imezinduliwa jijini Dar es Salaam.

Kampeni hiyo imewashirikisha madereva wa daladala, bodaboda, kwa kupatiwa stika ambazo zina ujumbe ambao utasomwa na utasaidia jamii kuachana na matamanio kwa watoto wadogo.

Hayo yalizungumzwa na Janeth Mavinza, Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Wanawake katika Jitihada za Maendeleo (WAJIKI) ikiwa sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambapo asasi hiyo ilifanua maadhimisho hayo Gongo la Mboto.

Alisema kutokana na madereva wa daladala na pikipiki kubeba abiria mara kwa mara, wanatarajia stika hizo zitasomwa na watu mbalimbali ujumbe uliomo, hiyo itasaidia kuondokana na changamoto kwa watoto wa kike. "Tunajua watu wengi wanatumia usafiri wa bodaboda na daladala, hivyo kuwekwa kwa stika katika vyombo hivyo vya usafiri, ujumbe utasomwa na watu mbalimbali na hali hiyo itasaidia kuwapo kwa ulinzi kwa mtoto wa kike," alisema.

Aliongeza kuwa wasichana na wanafunzi wanakutana na rushwa ya ngono na wamekuwa wakishindwa kutimiza ndoto zao. Alisema rushwa ya ngono imewaathiri wasichana wasio shuleni, wasichana wa kazi na wanafunzi wanajikuta wakipitia changamoto nyingi kutokana na kuombwa rushwa ya ngono.

Alisema rushwa ya ngono ni ukatili endelevu na unarudisha nyuma maendeleo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa WAJIKI, wamefanya kampeni katika wilaya tatu za Mkoa wa Dar es Salaam ambazo ni Kinondoni, Temeke na Ilala, na kuwa wanatarajia kufanya Kigamboni na Ubungo.



Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi Biashara Ndogo na Kati wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, akizungumza wakati wa halfa ya NMB Business Club iliyowakutanisha wafanyabiashara 300 jijini Dar es Salaam, ili kupata mafunzo ya kibiashara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara watakiwa kukata bima

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA wameshauriwa kuona umuhimu wa kukata bima ya biashara zao ili ziwe endelevu kwa kuzilinda dhidi ya hatari zinazoweza kujitokeza.

Ushauri huo umetolewa na Benki ya NMB kupitia kwa Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi, Biashara Ndogo na za kati, Filbert Mponzi, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kwa kusema kuwa biashara hukabiliwa na hatari mbalimbali ambazo kinga yake ni kuzikatia bima.

"Kupata mkopo wa kuongeza mtaji kutoka taasisi ya fedha ni jambo muhimu ila ukuaji endelevu wa biashara hutegemea zaidi kinga [ya biashara yenyewe] dhidi ya hatari zinazoweza kujitokeza," alisema Mponzi.

Majanga kama moto, wizi na mafuriko ni baadhi ya hatari zinazozikabili biashara na kudumaza ukuaji endelevu wake.

Benki ya NMB inatoa huduma za bima (Bancassurance) katika matawi yake yote 225 nchini kote kupitia ushirikiano wake na kampuni za bima za Sanlam, UAP, Shirika la Bima la Taifa (National Insurance Corporation - NIC), Jubilee, Shirika la Bima la Zanzibar (Zanzibar Insurance Corporation – ZIC) na Reliance.

Kwa ushirikiano na kampuni tajwa, matawi ya Benki ya NMB hutoa huduma za bima za magari, afya, mali za thamani, maisha, hatifungani na kilimo.

Mponzi alikuwa akizungumza katika semina iliyohudhuriwa na wajasiriamali wapatao 300 wanaounda Klabu ya Biashara ya Mkoa wa Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Alisema kwa kupitia huduma ya bima kupitia benki [Bancassurance], Watanzania wanaweza kukata bima na kuomba malipo ya bima pindi hatari zinapojitokeza kupitia matawi yote na NMB nchini kote.

Vilabu vya Biashara vya NMB huwakutanisha pamoja wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa ambao hupata nafasi ya kuelimishwa juu ya masuala mbalimbali kuhusu biashara zao.

Meneja mwandamizi wa huduma ya bima kupitia benki ya NMB, Martin Massawe, aliwaambia washiriki kuwa uwepo wa matawi ya NMB karibu na maeneo yao kunatoa fursa ya wao kupata huduma za bima kwa karibu zaidi.

Mjasiriamali na mshiriki wa semina hiyo ambaye biashara yake iliathiriwa na moto uliounguza sehemu ya Soko la Tegeta Nyuki jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Godwin Rwechungura, alitoa ushuhuda wa jinsi Benki ya NMB ilivyomhakikishia kupata fidia ya hasara aliyoipata.

"Biashara yangu imekuzwa na mikopo kutoka NMB kwa muda wa miaka 10 hivi sasa. Mikopo yetu hukatiwa bima na janga lilipotokea ndipo tunaona umuhimu wa ile bima kwani hivi sasa nina uhakika wa kurudi kufanya biashara kutokana na fidia ya bima," alisema.

Naye meneja mwandamizi wa huduma za benki kwa njia ya kidijitali wa Benki ya NMB, Tito Mangesho, alisema mbali na huduma za bima kupitia benki, taasisi hiyo ya fedha pia hutoa huduma za NMB Mkononi, Mastercard QR Code na nyingine nyingi kupitia kadi ambazo kwa pamoja husaidia kuboresha ufanisi katika biashara.



# Longido waweka mashine maalumu kupima corona

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, amesema ili kudhibiti ugonjwa wa corona usiingie nchini, wamechukuwa tahadhari mbalimbali ikiwamo kuweka mashine maalum ya kupima ugonjwa huo katika mpaka wa Kenya na Tanzania wa Namanga.

Lengo la hatua hiyo alisema ni mwenyeji na mgeni kupimwa atakapopita katika mpaka huo. Pia wameweka maji maalum yenye dawa ili wafanyakazi wa eneo hilo, kuyatumia kwa kunawa mikono sambamba na kupewa vifaa maalum vya kujikinga. Akizungumza kwenye mpaka wa Namanga na Kenya, Mwaisumbe, alisema hadi sasa Tanzania hakuna mgonjwa wa corona, lakini wanachukuwa tahadhari maeneo ya mipaka kwa kuwa ni muhimu ndio sababu katika eneo hilo wameweka tahadhari ya kutosha kwa watu wanaoingia na kutoka nje ya nchi. Alisema mpaka huo hutumiwa pia na watalii, hivyo wameweka vifaa maalum vya kupima ugonjwa huo, mita 30 kabla ya kufika eneo la upekuzi wa chumba cha dharura, mashine maalum ya kupimia ugonjwa huo.

Alisema endapo mtu atabainika kuwa na dalili za ugonjwa huo, atapelekwa kituo cha afya cha Eworendeke kilichotengwa kwa ajili ya wagonjwa kulazwa.

"Tumejipanga vema hapa mpakani na mgonjwa akigundulika anapumzishwa kwa muda wa saa mbili hapa mpakani kisha atapelekwa kituo cha afya cha Eworendeke kilichotengwa kwa ajili ya wagonjwa, lakini tumezuia mikusanyiko yoyote kwa muda ili kudhibiti ugonjwa huu ikiwamo kuzuia vibali vya promosheni," alisema.

"Tunaishukuru serikali kwa kutupa vifaa mbalimbali vya kudhibiti ugonjwa huu, ili kuhakikisha wilaya hii tunadhibiti ugonjwa huo, kwa kuwa ipo karibu na mpaka wa Tanzania na Kenya," alisema Mwaisumbe.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Dk. Jumaa Mhina, alisisitiza kuwa halmashauri hiyo imezuia mikusanyiko ya watu, ikiwamo kutoa promosheni za vitu mbalimbali, lakini wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia viongozi wa vijiji na watendaji wa kata.

Ameishukuru timu ya wataalamu wa afya kwa kutoa vifaa mbalimbali vya kudhibiti ugonjwa huo, na ametoa tahadhari kwa watu kutumia maji yenye malimao pamoja na kuacha kugusana au kusalimiana ili kuepukana na ugonjwa huo.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya ya Longido, Dk. Justice Munisi, alitumia fursa hiyo, kuishukuru timu ya afya Mkoa wa Arusha, kwa kutoa vifaa vya kudhibiti ugonjwa huo, huku akisisitiza kuwa madaktari wapo tayari kutibu ugonjwa huo endapo utaingia nchini sambamba na kutoa elimu kwa watumishi wa afya na wananchi namna ya kujikinga na ugonjwa huo. Baadhi ya wasafiri wanaotumia mpaka huo, Juma Ismail na Lucas Raphael raia wa Kenya, walishangaa kuona hatua zinazochukuliwa za kudhibiti ugonjwa huo nchini, kwa kuwa nchini Kenya wamechukua tahadhari, lakini kwa upande wa Tanzania tahadhari ni kubwa zaidi.



Mkuu wa mauzo wa kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania PLC Kanda ya Kaskazini, Brigita Stephen (kushoto), akimkabidhi zawadi ya simu mkazi wa Longido, Sketa Mollel, wiki iliyopita wakati wafanyakazi wa Vodacom wa kanda hiyo, walipotembelea kijiji hicho kwenye shamrashamra ya Wiki ya Wanawake Duniani na kutoa zawadi mbalimbali kwa wakazi wa Longido. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yakarabati magari mawili ya polisi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Singida, limeishukuru Kampuni za Sunny Autoworks LTD na Sunny Adventure Safaris kwa kuwasaidia kukarabati magari mawili ya jeshi hilo, kati ya matatu yalitolewa na jeshi kwa ajili ya matengenezo.

Akizungumza jijini Arusha wakati akipokea magari hayo kutoka kwa Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Ayub Ali Haji Suleman, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Sweetbert Njewike, alisema kutengemaa kwa magari hayo kutaongeza utendaji kazi wa jeshi hilo katika kudhibiti uhalifu wakati wa kufanya doria.

Njewike alisema kazi kubwa ya Polisi ni kufanya doria fupi na za masafa marefu ili kuhakikisha amani, usalama na utulivu unakuwapo kwa wananchi.

Aidha, alisema ili wafanikiwe kufanya doria hizo, ni lazima wawe na vyombo vya usafiri kama pikipiki na magari.

Alisema Mkoa wa Singida hali ya usalama ipo vizuri tofauti na miaka ya nyuma, ambapo kulikuwapo na matukio ya utekaji wa magari. Mkurugenzi wa Sunny Works LTD na Sunny Adventure Safaris LTD, Ayub Alihaji Suleman, alisema kampuni yake kwa zaidi ya miaka 30 wanajitolea kukarabati magari ya polisi na Kikosi cha Zimamoto mkoani humo ili kuimarisha ulinzi. "Kwa kipindi cha miaka 30, tungekuwa tukikarabati bure magari ya Jeshi la Polisi na kama tungekuwa tumetoa fedha yangegharimu zaidi ya Sh. milioni 20, lakini thamani ya mchango wetu kwa askari ni tuwatengenezea magari bure," alisema.

Alimshukuru Rais John Magufuli kwa kuendelea kusisitiza amani na usalama nchini.

## Shirika sasa lakamilisha mradi wa choo

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SHIRIKA lisilo la kiserikali la SNV, limekamikisha mradi wake wa ujenzi wa vyoo bora katika Halmashauri ya Arusha DC wilayani Arumeru.

Licha ya kukamilisha ujenzi wa mradi huo, shirika hilo limefanikiwa kuweziwesha kata 14 za Halmashauri ya Arusha kwa kufikia asilimia 95 ya kaya kwa kujenga vyoo bora.

Akizungumza wakati wa kikao maalumu cha kufunga mradi huo, Meneja wa Shirika la SNV Tanzania, Jackson Wandera, alithibitisha kumalizika kwa muda wa utekelezaji wa mradi huo, kwa kufikia mafanikio makubwa, yaliyoziwezesha kata 14, kufikia asilimia 95 ya kaya kuwa na vyoo bora, ukilinganisha na awali walipoanza mradi huo mwaka 2017.

Aidha, alisema kazi zilizozitekeleza katika mradi huo, ni pamoja na kuhamasisha na kutoe elimu ya ujenzi wa vyoo bora kwenye kaya, kuhamasisha tabia chanya za afya kwa watu kunawa mikono nyakati tano muhimu, na kutoa elimu ya afya shuleni na kuunda klabu za afya shuleni.

"Tumepata mafanikio makubwa kwa kuziwezesha kata 14, kwenye Halmashauri ya Arusha DC, kwa wastani wa asilimia 95 ya kaya kwenye kata 14, kujenga vyoo bora kwenye sehemu za kunawia mikono, kuhamasisha unawaji mikono nyakati tano muhimu," alisema Wandera.

Hata hivyo, Wandera alisema licha ya mafanikio hayo, bado jamii inakabiliwa na tatizo la unawaji mikono nyakati tano muhimu kwa kuwa mradi huo, umefanikiwa kufikia asilimia tano.

Ameitaka halmashauri hiyo kuendeleza kampeni hiyo, ya unawaji mikono kwa kuwa na wataalamu wa kuwajengea uwezo wananchi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Baraka Simoni, alipongeza SNV kwa ushirikiano na kazi nzuri waliyofanya kwa wananchi wa Halmashauri ya Arusha, kwa utekelezaji wa mradi huo na ameahidi kuendelea kusimamia mradi huo, ili uwe endelevu kwa manufaa ya wananchi wa halmashauri hiyo.

Amewataka wataalamu wa halmashauri kuendelea kutoa elimu kwa jamii ya matumizi sahihi ya vyoo.

Pia amewataka kuwekeza nguvu katika kampeni ya tabia chanya ya kunawa mikono kwa maji na sabuni, nyakati tano muhimu.

"Kunawa mikono ni jambo linalofanywa na mtu mwenyewe binafsi, niwatake wananchi kubadili tabia na kuanza kunawa mikono kwa maji na sabuni, katika nyakati tano muhimu," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Angela Mvaa, kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, alisema halmashauri imeweka mpango mikakati ya kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya vyoo bora na unawaji mikono kwa sabuni na kuhakikisha jamii inakuwa na tabia chanya za kiafya.



## Mbwa wazururaji 260 wauawa Hai

**Na Godfrey Mushi,** HAI

ZAIDI ya mbwa 260 wanaozurura ovyo mitaani katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai, wameuawa kwa kupigwa risasi na maofisa mifugo ili kuepusha madhara ya kiafya kwa binadamu.

Taarifa ya Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo (TEO), Noel Nnko, aliyoitoa inaeleza kuwa hadi kufikia jana jioni mbwa hao walikuwa wameuawa na kwenda kufukiwa eneo la Muungano.

Alisema mbwa hao wanaohofiwa kuwa na magonjwa kutokana na kukosa chanjo na uangalizi wa wamiliki wa mifugo hiyo, waliuawa kuanzia Machi 9 hadi 14 mwaka huu.

"Kama mlivyosikia awali, tulihofu kuzuka kwa ugonjwa wa kichaa cha mbwa na tukatangaza wapewe chanjo na wasiachiwe wazurure mitaani. Sasa wamiliki wakakaidi amri hiyo na hadi kufikia jana tulikuwa tumewapiga risasi mbwa 263," alisema Nnko.

"Ni ajabu sana, kwa sababu kuna wamiliki wa mifugo hiyo hawajui hata hali ya afya ya mbwa wao. Nilishagawa barua kwa kila mwenyekiti na mtendaji, nimewaelekeza kutangaza zoezi hilo na sisi kama mamlaka tayari tumeshatangaza misikitini na makanisani, kwenye mbao za matangazao na kwenye mikutano ya vitongoji. Kimsingi zoezi hili ni endelevu."

Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, akizungumzia zaidi zoezi hilo, alieleza kufurahishwa kwake na juhudi zilizoanza kuchukuliwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai katika kutimiza majukumu yake.

"Hii ndio kazi ya serikali na nimpongeze ofisa huyu kwa kuua mbwa hao wanaozurura ovyo mitaani na hata ukiangalia suala la usafi wa mazingira hapa katika mji wa Bomang'ombe linaridhisha sana, tumeona kuna mapipa mengi ya kutupa taka na kuondoa gereji bubu katikati ya mji, tunawasihi wenyeviti wote muungane naye kwa pamoja mji huu uwe safi," alisisitiza Ole Sabaya.

# Mawasiliano barabara yarejeshwa Mwanga

**Godfrey Mushi,** MWANGA

HATIMAYE serikali imefanikiwa kufungua mawasiliano ya barabara iliyokuwa haipitiki kwa zaidi ya siku nne, kati ya ukanda wa milimani na tambarare, Wilaya ya Mwanga.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Thomas Apson, alisema hadi kufikia jana, Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) alikuwa ameshafungua baadhi ya sehemu katika vijiji vilivyoathirika na maporomoko ya mawe, miamba na vifusi vya udongo.

"Tunamshukuru Mungu sasa barabara inayounganisha maeneo ya ukanda wa milimani na tambarare imefunguka na wananchi wanaendelea na shughuli za kiuchumi kama kawaida, ingawa bado tunaendelea kuondoa vifusi katika baadhi ya maeneo," alisema.

Wiki iliyopita, wananchi wanaotoka ukanda wa milimani hasa kata za Kilomeni na Lembeni hawakuweza kutoka wala kuingia kutokana na mvua kusababisha vifusi vya udongo, mawe na miamba iliyokatika kujaa barabarani.

Hali ya usafiri katika maeneo hayo ilikuwa mbaya, hasa kwa wagonjwa kushindwa kufuata matibabu katika Hospitali ya Wilaya hiyo pamoja na mahitaji mengine muhimu ya binadamu.

Uharibifu huo wa miundombinu ya barabara ulitokana na mvua kubwa za msimu wa masika zinazoendelea kunyesha mkoani Kilimanjaro.

Barabara ambayo ina urefu wa kilomita 17 ambayo inategemewa na wakazi wa Wilaya ya Mwanga kutokana na kupitisha kwa wingi mazao ya chakula hasa viungo.

Kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakazi Kata ya Kilomeni akiwamo Ephraim Mlacha na Amina Mmbwambo, walieleza hisia zao namna hali hiyo ilivyoacha majanga kwa wananchi wa ukanda wa milimani, wakihofia kuadimika kwa bidhaa zilizopo madukani na kwenye masoko ya walaji.

"Endapo bidhaa zilizopo madukani kwa sasa zitaisha, itakuwa vigumu kupata bidhaa nyingine, kwa kuwa barabara hii haipitiki kabisa na imezibwa na vifusi vya mawe, miamba na udongo.

Mbwambo aliongeza: "Wanaoteseka zaidi hapa ni wanawake wajawazito ambao wamepewa rufani kwenda kutibiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC."

Hata hivyo, akizungumzia adha hiyo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kilomeni, Sadat Kweka, alisema athari ambazo zimesababishwa na mvua hizo ni kubwa ikiwamo baadhi ya familia kukosa makazi.



Wanachama wa Taasisi isiyo ya Kiserikali inayojihusisha na masuala ya Ulinzi wa Kisheria kwa Jamii (Smart Community on Legal Protection Organization) wakishiriki upandaji wa miti juzi kwenye chanzo cha maji cha Mto Naurei kilichopo Shule ya Msingi Sekei, kama sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Upandaji Miti. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# TIC: Parachichi lisafirishwe kwa reli

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI mkoa wa Kilimanjaro ukiwa miongoni mwa mikoa inayosifika kwa uzalishaji wa parachichi nchini, serikali imeshauri wafanyabiashara wa zao hilo na wawekezaji kutumia usafiri wa reli kama njia kuu ya kusafirisha mazao ya biashara kwenda bandarini.

Meneja wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) Kanda ya Kaskazini, Daudi Riganda, alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki, wakati akizungumzia uboreshaji wa mifumo na miundombinu iliyowekezwa na serikali katika kanda hiyo.

"Tumeboresha mifumo na miundombinu ya usafirishaji kwa ajili ya kusaidia wawekezaji wetu na hata wafanyabiashara ya mazao kwa serikali kufufua reli ya kaskazini. Hiyo ni fursa ya pekee, itumieni sasa kupunguza gharama za usafirishaji kwenda bandarini.

Kwa upande wake, Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini ambaye ni Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fedrick Shoo, alisema kwa kuwa watu wanaowaunga mkono kulima zao wametaka wachangamkie fursa zilizopo ikiwamo kuanzisha kilimo chenye soko duniani, kilimo cha parachichi yaani Green Gold, watazingatia ushauri huo wa kituo cha uwekezaji.

Kampuni ya uzalishaji wa parachichi ya Africado iliyopo Kilimanjaro, mwaka juzi peke yake waliuza kwa wingi parachichi katika masoko ya Ulaya, matunda zaidi ya tani 2,580.

Africado inauza kwa wingi parachichi inayolimwa mkoa wa Kilimanjaro kwenye masoko ya Ufaransa, Denmark, Holland na Sainsbury Waitrose ya UK (Uingereza).

Parachichi kutoka Kilimanjaro ambalo linauzwa katika masoko hayo ni bora zaidi na linauzika zaidi kuliko lile linalochukuliwa katika masoko ya nchi ya Afrika Kusini na Peru.

Pia, parachichi linalozalishwa katika mkoa wa Kilimanjaro linalifuata kwa kasi sokoni tunda kama hilo linalozalishwa nchini Israel.

Nipashe

# Spotika



MAMBO MA5 MUHIMU MBIO ZA 4-BORA EPL UK. 16 & 17



## ISIKUPITE

BRUNO Fernandes amehusika katika mabao mengi (10) kuliko mchezaji yeyote kwenye michuano ya Europa League msimu huu, Mreno huyo amefunga sita na kutoa pasi za mwisho nne akiwa na Manchester United na Sporting.

# CORONA INAVYODIDIMIZA UCHUMI SOKA LA ULAYA, DUNIA

Madaktari wakimtibu mgonjwa mwenye maambukizi ya virusi vya corona, COVID-19 ambavyo hadi jana vimeripotiwa kuwakumba watu 156,000, huku vifo vilivyotokana na janga hilo vikiwa zaidi ya 5,800. **HABARI UK. 19**




# WANAPOSHIKANA MESSI, RONALDO

**BARCELONA,** Hispania

CRISTIANO Ronaldo na Lionel Messi wanaishi katika maisha ya ushindani zaidi kwenye soka katika maisha yao. Wachezaji hao wawili wamekuwa wakiwagawa mashabiki tangu walipoingiza mguu kwenye soka la ushindani duniani.

**Ni wachezaji hao wawiili wamekuwa wapinzani kwa zaidi ya muongo mmoja na hakuna mchezaji yeyote aliyejaribu kuwakaribia.**

Makala haya yanachambua rekodi nne ambazo wameziweka kwa pamoja Ronaldo na Messi, shuka nazo...

### 4. HAT-TRICK NYINGI LALIGA KWA MSIMU

Messi aliweka rekodi ya kuwa na hat-trick kwenye msimu mmoja wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, msimu wa 2011/12, ambapo raia huyo wa Argentina alifunga mabao 50 katika mechi 37 za ligi. Mshambuliaji huyo wa Barcelona anayevaa jezi namba 10, alifunga hat-trick ya kwanza ya ligi dhidi ya Osasuna Septemba. Akawa tena kwenye moto huo huo wiki moja baadaye, akifunga hat-trick ya pili wakati wakiwafumua Atletico Madrid 5-0.

Alifunga hat-trick mbili zaidi dhidi ya Mallorca na Malaga kabla ya mwisho wa mwaka. Messi akafunga hat-trick nne zaidi katika kipindi cha pili cha msimu dhidi ya Valencia, Granada, Malaga na Espanyol, akamaliza hat-trick ya nane, akiwa mchezaji wa kwanza kuweza kufanya hivyo kwenye Ligi Kuu ya Hispania.

Mreno Ronald aliweza kufikia rekodi ya Messi msimu wa 2014/15, akifunga hat-trick nane kwa Real Madrid kwenye LaLiga. Ronaldo alianza msimu kwa mabao matatu dhidi ya Deportivo La Coruna na Elche Septemba. Mreno huyo alifunga hat-trick ya tatu na nne dhidi ya Atletic Bilbao na Celta Vigo Oktoba na Desemba mwaka huo.

Hata hivyo, ilimchukua hadi Aprili kufunga hat-trick ya tano, na wakati huu ilikuwa dhidi ya Granada. Ronaldo alimaliza msimu kwa kufunga hat-trick tatu Mei dhidi ya Sevilla, Espanyol na Getafe na kuifikia rekodi ya Messi.

### 3. KIKOSI CHA FIFPRO MARA NYINGI

Shirikisho la Wachezaji wa Kulipwa wa Kimataifa au FIFPro, limekuwa likitengeneza timu bora ya mwaka tangu mwaka 2005, wakiwapigia kura wachezaji wakulipwa kutoka kila sehemu duniani. Timu hiyo inaitwa FIFPro World XI (11 bora ya dunia ya mwaka) ikiwajumuisha wachezaji bora kutoka sehemu mbalimbali duniani, akiwamo golikipa mmoja, walinzi watatu, viungo watatu na washambuliaji watatu. Tangu kuanzishwa kwake, wachezaji wawili wameweka rekodi ya kutwaa mara nyingi zaidi kwenye kikosi hicho. Messi na Ronaldo wamejumusishwa kwenye kikosi hicho mara 13.

Muaregntina na Mreno huyo wote kwa mara ya kwanza waliorodheshwa kwenye FIFPro World XI mwaka 2007, hata hivyo, wakati Messi alichaguliwa kama mshambuliaji, Ronaldo alitajwa kama kiungo. Mwaka uliofuata, walitajwa wote wawili mbele kwa mara ya kwanza na hawajakosa tangu wakati huo.

Ronaldo ameziwakilisha Manchester United, Real Madrid na Juventus kwenye tuzo hiyo; ambapo yeye na Dani Alves ni wachezaji wawili pekee kutajwa kwenye tuzo hiyo wakiwa kwenye klabu tatu tofauti. Wakati Messi mara zote amekuwa na Barcelona.

### 2. HAT-TRICK NYINGI UEFA

Kwa sababu kufunga ndio kazi yao kubwa, si jambo la kushangaza Messi na Ronaldo wana rekodi sawa ya kufunga hat-trick nyingine kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Raia hao wa Argentina na Ureno wote wamefunga hat-trick nane kila mmoja. Wachezaji pekee waliojaribu kuwakaribia ni Robert Lewandowski, Mario Gomez na Luiz Adriano na wote kila mmoja ana hat-trick tatu kwa majina yao.

Messi alifunga hat-trick yake ya kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Aprili mwaka 2010 dhidi ya Arsenal na tangu hapo, amefunga hat-trick dhidi ya Viktoria Plzen, Bayer Leverkusen, Ajax, Apoel, Celtic, Manchester City na PSV Eindhoven.

Ronaldo alifunga hat-trick ya kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa mchezaji wa Real Madrid dhidi ya Ajax mwaka 2012. Halafu akaendelea kufunga hat-trick zaidi dhidi ya Galatasaray, Shakhtar Donetsk, Malmo FF, Wolfsburg, Bayern Munich na Atletico Madrid.

Hat-trick ya hivi karibuni ya Messi alifunga dhidi ya PSV Eindhoven kwenye msimu wa 2018/19, wakati Ronaldo alifunga hat-trick yake ya mwisho dhidi ya Atletico Madrid msimu uliopita, pia ikiwa ni ya kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa akiwa mchezaji wa Juventus.

Ronaldo ni mchezaji pekee kufunga hat-trick tatu kwa msimu mmoja, ambapo alifunga wakati anaichezea Real Madrid msimu wa 2015/16. Kwa upande mwingine, Messi amefunga hat-trick mbili kwa msimu mmoja msimu wa 2011/12 na 16/17.

### 1. TATU BORA YA BALLON D'OR

Wakati tuzo ya Ballon d'Or ikiwa inachukuliwa na wachezaji bora tangu kuanzisha kwake mwaka 1956, Messi na Ronaldo ndio wenye mafanikio makubwa zaidi kwenye tuzo hiyo.

Wote wawili walitokea kwenye 3-bora ya Ballon d'Or mwaka 2007, wakati Messi alipomaliza akiwa watatu na Ronaldo akiwa wa pili nyuma ya Kaka.

Messi na Ronaldo wametokea kwenye 3-bora ya Ballon d'Or mara 12, ikiwa ni mara nyingi zaidi kuliko mchezaji yoyote katika historia. Wote watatu wamemaliza nafasi ya tatu mara moja, lakini wakati Ronaldo amemaliza nafasi ya pili mara sita, Messi amefanya hivyo mara tano. Hata hivyo, Messi amemzidi Ronaldo kwa kutwaa mara nyingi zaidi Ballon d'Or, akiwa amebeba mara sita na Ronaldo mara tano.

Tangu mwaka 2007, Ronaldo hajakuwapo kwenye tatu-bora ikiwa ni mwaka 2010 pekee, huku Messi hajawa kwenye 3-bora mwaka 2018, ambapo ilibebwa na Luka Modric.

**JE, WAJUA?**



KIPIGO ilichokipata Liverpool cha mabao 3-2 dhidi ya Atletico Madrid, ni mara ya kwanza kwa timu hiyo kupoteza mechi ya michuano ya Ulaya katika uwanja wa nyumbani chini ya Kocha Jurgen Klopp, lakini kikiwa cha kwanza kwao kupoteza Ulaya hapo kwenye dimba la Anfield tangu Oktoba 2014.



Beki wa Yanga, Lamine Moro (kulia), akimiliki mpira dhidi ya mshambuliaji wa KMC, Sadala Lipangile, kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam wiki iliyopita na KMC kushinda 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KMC INAVYOCHOMOZA KUWA MSHINDANI WA YANGA BARA

**Na Adam Fungamwango**

ALIKUWA ni Salim Aiyee, ambaye msimu uliopita alishika nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji bora akimaliza na mabao 18, nyuma ya Meddie Kagere aliyecheka na nyavu mara 23, akifunga bao pekee Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam na kuipa ushindi timu yake ya KMC wa bao 1-0 dhidi ya Yanga.

**Aiyee ambaye msimu uliopita alikuwa akiichezea Mwadui FC, hakuwa na msimu mzuri, lakini bao lake hilo pekee limemwezesha kuanza kuonekana tena kwenye kurasa za magazeti na kuwa gumzo kwenye redio, TV na mitandao ya kijamii.**

Ushindi wa KMC una maana, timu hiyo imeendeleza rekodi yake ya kuisumbua Yanga kwenye Ligi Kuu tangu ilipopanda na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu uliopita wa 2018/19.

KMC, inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni, msimu uliopita ilicheza michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na ikawa kwenye msimu mzuri, msimu huu pamoja na kwamba ipo kwenye nafasi za chini, ikipigania kutoshuka daraja, lakini haijafungwa na Yanga.

Kwenye Ligi Kuu, kuna baadhi ya timu zimekuwa na tabia ya kutokubali kufungwa kirahisi na baadhi ya timu, na KMC imekuwa ni moja kati ya timu ambazo huwa ni mwiba mchungu kwa Yanga tangu ilipopanda na hata kama ikifungwa, lakini panachimbika.

Mfano Simba inavyopata ugumu mno kwa Kagera Sugar na Prisons, lakini si kwa Mbeya City, Coastal Union, huku Yanga ikiwa ni rahisi sana kuzifunga timu nyingi za majeshi kama Ruvu Shooting, Prisons, JKT Tanzania, lakini si kwa Coastal Union, Polisi Tanzania, Mbeya City na pia KMC.

Mfano ni kwamba KMC imekuwa ni nyanya kwa Simba, ikifungwa mechi zote nne za msimu uliopita na msimu huu pia, lakini kwa Yanga imekuwa ikikomaa kweli kweli.

Desemba 19, 2018, Simba iliichapa KMC mabao 2-1 mechi za mzunguko wa kwanza msimu uliopita na wa pili, iliifunga pia mabao 2-1, Aprili 25 mwaka jana.

Msimu huu, Simba iliifunga KMC mabao 2-0, Desemba 28, mwaka jana mechi ya mzunguko wa kwanza na hivi majuzi, Machi Mosi mwaka huu, pia ikashinda mabao 2-0, yaliyofungwa na Luis Miquissone.

Kesheshe inakuja KMC inapopambana na Yanga, ndipo panapotokea patashika nguo kuchanika.

**1. KMC 0-1 YANGA (2018/19)**

Ni mechi ya mzunguko wa kwanza msimu uliopita, ikiwa ni ya kwanza kwa timu hizo kukutana baada ya KMC kupanda Ligi Kuu. Yanga ilishinda kwa mbinde bao 1-0, Oktoba 25, 2018.

Lilikuwa ni bao la mkwaju wa faulo uliopigwa na Feisal Salum, dakika moja kabla mechi kumalizika, huku mashabiki wa Yanga wakiwa wamekata tamaa kwa kuamini mechi hiyo ingeisha kwa sare tasa.

**2. KMC 1-2 YANGA (2018/19)**

Machi 10, mwaka jana, ilichezwa mechi ya mzunguko wa pili Yanga dhidi KMC. Kwenye mechi hiyo Yanga kwa mara nyingine ilishinda kwa mbinde mabao 2-1.

Mohamed Rashid akiwa kwa mkopo kutokea Simba aliipatia KMC bao, lakini Papy Yshishimbi alisawazisha. Yanga ilipata ushindi kwa bao la kujifunga la beki wa KMC Ally Ally dakika ya 66. Na baadaye mchezaji huyo akasajiliwa Yanga.

**3. KMC 1-1 YANGA (2019/20)**

Ilikuwa ni mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu msimu huu, ikichezwa Desemba 2, mwaka jana.

Jitihada za KMC kuikazia Yanga tangu msimu uliopita zilionekana kwa sare ya bao 1-1. Yanga ilipata bao dakika ya 72 lililofungwa na Mrisho Ngassa, lakini kwenye dakika tatu za nyongeza, KMC ilipata penalti iliyowekwa wavuni na Abdul Hillary.

**4. KMC 1-0 YANGA (2019/20)**

Hii ndiyo mechi iliyochezwa Alhamisi iliyopita, KMC ilipoitungua Yanga bao 1-0, likiwekwa wavuni na Salim Aiyee na kuendelea kuwa ni timu ambayo ni sumbufu mno kila inapokutana na Yanga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**NJE YA UWANJA**

MABAO manne yaliyofungwa katika muda wa nyongeza katika mechi ya mkondo wa pili ya hatua ya 16-bora Ligi ya Mabingwa Ulaya katika Uwanja wa Anfield wakati Atletico Madrid ikishinda 3-2 dhidi ya Liverpool, ni mara ya kwanza katika michuano hiyo idadi kubwa ya mabao kama hiyo kufungwa muda wa nyongeza. Liverpool ilishinda 1-0 ndani ya dakika 90 na kufanya matokeo ya jumla kuwa 1-1, hivyo kulazimika kuongezwa muda wa nyongeza na Atletico kuibuka na ushindi wa 3-2.

UEFA CHAMPIONS LEAGUE

## Extra Time

# MAMBO MA5 MUHIMU MBIO ZA 4-BORA EPL




**LONDON,** England

NI moja kati ya vitu vya kuvutia zaidi katika kila msimu kuona klabu zikiwania nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. Huku Manchester City ikitarajiwa kutumikia adhabu ya kutoshiriki michuano hiyo ya Ulaya msimu ujao, hiyo imetoa nafasi kwa timu nyigine kuiwania nafasi hiyo.

**Hapa ni mambo muhimu yanayochangia kwenye mbio za klabu katika kufuzu kucheza michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Ulaya, twende pamoja...**

### 1. MORALI YA VIJANA WA CHELSEA

Frank Lampard alikabiliwa na changamoto kubwa wakati alipochukua nafasi ya kuinoa Chelsea kipindi cha majira ya joto kilichopita. Akiwa na msimu mmoja tu wa uzoefu kwenye nafasi ya ukocha, maamuzi yake ya kukubali kazi ambayo ingeweza kumthibitisha uwezo wake kwenye maisha yake ya kisoka kulionyesha namna gani kiungo huyo wa zamani wa England alivyo na uwezo wa kukabiliana na changamoto mpya.

Adhabu ya kuzuia kutofanya usajili ulikuwa wakati mgumu na wa mpito kwa klabu hiyo, na wakati hali hiyo ilibainisha kwamba Lampard hangeweza kupoteza, pia kulizua maswali kama angeweza kupata mafanikio kwenye hali hiyo. Hata hivyo, yeye mwenyewe kama mchezaji, Lampard aliaminiwa wakati akianza maisha ya soka pale West Ham United akiwa bado kijana, na uzoefu wake huo ukamfanya aamue kuwaamini wachezaji wake vijana kama Callum Hudson-Odoi, Tammy Abraham, Reece James, Mason Mount na Billy Gilmour.

Uaminifu aliouonyesha kwa vijana wake ilitoa taswira tofauti na utamaduni wa zama za Roman Abramovich, na ameweka uwekezaji wa kikosi chake kwa siku za usoni na kwa uhakika vijana hao hawajamwangusha. Kwa miaka mingi Chelsea ilikuwa ikizalisha vijana wengi kwenye timu za Ulaya, lakini ilishindwa kuwapa nafasi kwenye kikosi chao cha wakubwa.

### 2. UJIO WA BRUNO FERNANDES

Manchester United imetengeneza vichwa vingi vya habari kwa sababu ya maamuzi kadhaa yaliyoonekana kutokuwa sawa katika miaka ya hivi karibuni, na huku Ole Gunnar Solskjær akiingia kwenye mwaka wake wa pili kama kocha wa klabu hiyo, anaonekana amedumu kwa muda mrefu zaidi tofauti na wengi walivyoamini. Mchango mkubwa kwa 'kufufuka' kwao hivi karibuni ni usajili wa Bruno Fernandes. Kiungo huyo wa kimataifa wa Ureno ameleta ujasiri wa kujiamini kwenye vyumba vya kubadilishia nguo pale Old Trafford, na anaweza kuwa sehemu ya mchango mkubwa wa kupata nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Yalikuwa ni matokeo ya kushangaza ya ushindi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain msimu uliopita ambayo yalimhakikishia Solskjær kupata mkataba wa kudumu, huku pia alikuwa mchezaji shujaa wakati wa mafanikio ya klabu hiyo kwenye mashindano hayo mwaka 1999.

Fernandes amejiimarisha maisha yake pale Manchester United tangu siku ya kwanza kabisa kuwasili. Alionekana kubeba mzigo kwenye safu ya kiungo na hata shutuma hasi zlizokuwa akizipata kiungo mwenzake, Paul Pogba sasa zimekuwa chanya kwenye nafasi hiyo.

Kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya utakuwa wakati bora zaidi kwa maisha ya ukocha ya Solskjær kwani kwa sasa si tu ameonyesha kukimudu kikosi chake, lakini pia uwezo wake umeimarika kama kocha.

### 3. USHUJAA WA BRENDAN

Kushindwa kutwaa taji la Ligi Kuu ya England akiwa na Liverpool unaweza kuwa wakati mbaya zaidi kwake, lakini Brendan Rodgers yupo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuirudisha Leicester City kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Timu yake ilionyesha kiwango cha kuvutia zaidi kwenye ushindi wa 4-0 dhidi ya Aston Villa katika mchezo wa Jumatatu iliyopita, na ujasiri ambao Rodgers ameuingiza kwa wachezaji wake unaonyesha mafanikio makubwa pale kwenye Uwanja wa King Power.

Kama ilivyokuwa wakati wakitwaa taji la Ligi Kuu ya England mwaka 2016, mtu wake muhimu hadi sasa hapo Leicester City ni mshambuliaji wao, Jamie Vardy.

Kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya pili itakuwa hamasa kubwa zaidi kwa Vardy. Kocha wa zamani Claudio Ranieri alishindwa kufuzu kwa msimu wa pili huku pia klabu hiyo ikijikuta ikipitia wakati mgumu baada ya kifo cha mmiliki wake, Vichai Srivaddhanaprabha. Baada ya misimu kadhaa, Leicester City inaonekana ina nafasi nyingine ya kurudi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### 4. BAHATI NASIBU KWA TIMU NYINGINE

Sheffield United ilirudi kwenye Ligi Kuu ya England huku ikionekana kuwa itashuka daraja, lakini kocha, Chris Wilder amebadilisha kabisa mambo na kuiweka kwenye nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kufuzu kucheza Ligi ya Europa inaweza kuwa ndoto ambayo hawakuwahi kuiota, lakini kwa kiwango kinachoonyeshwa na timu hiyo kwa uhakika chochote kinaweza kutokea kwao.

Wanaweza wasifuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini tayari wameonyesha msimu huu kila kitu kinawezekana kwa klabu hii.

Wakati huo huo, Wolverhampton Wanderers wanaendelea kupata uzoefu wa changamoto ya kuwania taji la Ligi Kuu na Ligi ya Europa. Kocha Nuno Espirito Santo ameonyesha ujio wa changamoto mpya kwenye mbio za Ligi Kuu tangu alipoipandisha Wolves na malengo yake ni kuendelea kuisukumiza kwenye mafanikio zaidi. Huku wakipata sapoti kubwa ya kifedha nyuma yao, Wolves wanaweza kupata mafanikio makubwa zaidi chini ya kocha wao huyu na kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya ni hatua inayofuata kwao.

Ili kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, Wolves inahitaji kumaliza msimu ikiwa juu ya timu kama Tottenham Hotspur na Arsenal, na wachambuzi kadhaa wameshaona jinsi picha linavyokwenda.

### 5. MAJANGA ZAIDI KWA MOURINHO

Ukichukulia namna Tottenham Hotspur ilivyoonyesha udhaifu wakati wakitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Red Bull Leipzig Jumanne iliyopita, kufuzu kwa mashindano hayo msimu ujao ni wazi wakati mwingine mgumu kwa Jose Mourinho. Majeruhi ya wachezaji muhimu kumefanya kiwango cha Spurs kushuka zaidi kwa wiki za hivi karibuni, lakini matokeo yao ya hivi karibuni hayaonyeshi kama wanaweza kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

Michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ndiyo iliyomjengea jina Mourinho katika maisha yake ya ukocha hadi sasa. Tangu kuanzia kule Porto alikobeba taji hilo mwaka 2004 na baadaye Inter Milan mwaka 2010. Lakini mafanikio hayo kwa sasa yanamwonyesha Mourinho wa tofauti kabisa. Tangu achukue mikoba ya kuinoa Spurs kutoka kwa Mauricio Pochettino, Tottenham bado haijaonyesha ubora

## Nukuu

"Tuna golikipa ambaye ni bora duniani, bila shaka yoyote, nimekuwa nikisema hivyo kwa muda mwingi, ni kama Barcelona ambayo ina Messi. Anaamua matokeo ya mchezo kwa staili yake ya uchezaji; Oblak yeye anaamua matokeo kwa kuokoa," **Kocha wa Atletico Madrid, Diego Simeone baada ya timu yake kuichapa Liverpool mabao 3-2 na kuitoa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.**



"Kwanza kabisa mawazo yetu yapo na Mikel Arteta na tunamtakia kupona haraka. Ni muhimu kabisa kwa afya na ustawi wa watu binafsi inachukua kipaumbele na kwa kuzingatia kwamba mechi ya Jumamosi [juzi] imeahirishwa, tunaomba radhi kwa mashabiki wote kwa usumbufu utakaojitokeza, lakini amini kila mmoja ataelewa kuwa tunakabiliwa na hali isiyokuwa ya kawaida," **Mkurugenzi Mkuu wa Brighhton, Paul Barber baada ya mechi dhidi ya Arsenal kuahirishwa kutokana na Arteta kukutwa na maambukizi ya virusi vya corona wiki iliyopita.**



"Ni ngumu kuzungumzia kuhusu majeruhi, lakini unataka nizungumze kuhusu vitu ambavyo vipo wazi? Vipi kama Leipzig wangekuwa hawana Sabitzer (Patrik), Schick (Timo) , Werner, unafikiri wangeshinda kama hivi? Ingewezekana Liverpool ikafanya vizuri bila (Mohamed) Salah, (Sadio) Mane, (Jordan) Henderson au Barcelona bila (Antoine) Griezmann, (Lionel) Messi, (Luis) Suarez na (Gerard) Pique," **Kocha wa Spurs, Jose Mourinho akijitetea wingi wa majeruhi baada ya kupigwa 3-0 na RB Leipzig kwenye mchezo wa pili wa hatua ya 16-bora.**



## Michezo



Mshambuliaji wa Simba, John Bocco, akimtoka beki wa kati wa Yanga, Lamine Moro kwenye mechi ya Ligi Kuu, Machi 8, mwaka huu katika Uwanja wa Taifa. **PICHA: MAKTABA**

# MECHI SIMBA, YANGA ILIVYOSOMEKA KINAMBA

**Adam Fungamwango**

BAO la dakika ya 44 la Bernard Morrison liliifanya Yanga kumaliza uteja wa misimu mitatu mfululizo kwa Simba, ilipoibuka na ushindi wa bao 1-0 Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Ulikuwa ni ushindi uliosubiriwa na wanachama na mashabiki wa Yanga kwa miaka mitatu, kwani mara ya mwisho Yanga kuifunga Simba ilikuwa ni mwaka 2016, na tangu wakati huo ilikuwa haijaifunga tena.**

Ilikuwa ni Februari 20, 2016, Ligi Kuu msimu wa 2015/16, Yanga ilipoichapa Simba mabao 2-0, yaliyofungwa na Donald Ngoma ambaye kwa sasa yupo Azam FC na Amissi Tambwe ambaye hayupo tena na timu hiyo.

Baada ya hapo ikaja misimu mitatu ya Yanga kuteseka kwani, Oktoba Mosi 2016, Ligi Kuu ya msimu wa 2016/17, zilitoka sare ya bao 1-1, ya Amissi Tambwe kwa Yanga na Shiza Kichuya kwa upande wa Simba, na mzunguko wa pili Simba ikaichapa Yanga mabao 2-1, yaliyofungwa na Kichuya na Laudit Mavugo, la Yanga likiwekwa wavuni na Simon Msuva, Februari 25, mwaka 2017.

Msimu uliofuata 2017/18 pia haukuwa mzuri kwa Yanga kwani Oktoba 28, 2017, ilitoka sare ya bao 1-1 na Simba, mabao ya Kichuya na Obrey Chirwa kwa Yanga ambaye kwa sasa yupo Azam FC na mechi iliyofuata mzunguko wa pili, ilifungwa bao 1-0 Aprili 29, 2018 bao la Erasto Nyoni.

Msimu uliopita 2018/19, timu hizo pia zilitoka sare ya bila kufungana kwenye mechi ya kwanza, ikipigwa Septemba 30, 2018, lakini mechi iliyofuata ya msimu huo, Simba ilishinda bao 1-0 likiwekwa wavuni na Meddie Kagere, pambano likichezwa Februari 16, mwaka 2019.

Kwenye mechi ya kwanza msimu huu Januari 4, timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2 kabla ya Yanga kushinda mechi ya Jumamosi iliyopita bao 1-0 na kumaliza uteja wa kutoifunga Simba kwa misimu mitatu mfululizo.

Mwandishi wa makala haya anakuletea takwimu na matukio ya mechi hiyo katika namba...

**MIL. 545/-** Ni idadi ya mapato halisi yaliyopatikana kwenye mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga zilizocheza Machi 8 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na kuingiza Sh. milioni 545.

**57-** Ni asilimia ya umiliki wa mpira iliyokuwa nao timu ya Simba kwenye mechi hiyo ambayo wapinzani wao walishinda bao 1-0.

**43-** Yanga ilimiliki asilimia hizi kwenye pambano hilo ambalo pamoja na kuzidiwa umiliki wa mpira na wapinzani wao, lakini iliondoka na ushindi wa bao 1-0.

**25-** Ni umbali wa mita ambazo zinakadiriwa mpigaji wa faulo ya Morrison alipoachia mkwaju ukaenda moja kwa moja wavuni na kumuacha kipa Aishi Manula wa Simba asijue la kufanya.

**18-** Ni idadi ya faulo zilizochezwa na wachezaji wa Yanga kwenye mechi hiyo.

**10-** Ni idadi ya faulo zilizochezwa na wachezaji wa Simba kwenye mechi hiyo.

**6-** Simba ilipiga idadi hii ya mashuti ambayo hayakulenga lango la wapinzani wao, Yanga.

**5-** Ni idadi ya kona ilizopata Simba kwenye mechi hiyo ya watani wa jadi, lakini pia ni idadi ya mashuti ya wachezaji wa timu hiyo yaliyolenga golini mwa Yanga.

**4-** Yanga ilipiga idadi hii ya mashuti ambayo hayakulenga lango la wapinzani wao kwenye mechi hiyo.

**3-** Namba hii inasimama kuwa ni idadi ya kona Yanga ilizopiga kwenye mechi hiyo, lakini pia ni idadi ya kadi za njano ambazo wachezaji wake walizawadiwa kwa kucheza faulo.

**2-** Namba hii ni idadi ya mashuti yaliyolenga lango la Simba. Na katika haya, moja lilidakwa na moja liliingia wavuni na kuwa ndiyo bao lililowalaza mapema Simba siku hiyo. Hata hivyo, namba hii hii inasimama pia kwa idadi ya kadi za njano ambazo wachezaji wa Simba walizipata kwenye mechi hiyo.

**1-** Ndiyo goli pekee kwenye mechi hiyo lililofungwa na Benard Morrison wa Yanga, lakini pia Yanga iliotea mara moja tu kwenye mechi hiyo.

**0-** Hakukuwa na kadi nyekundu kwenye mechi hiyo iliyohudhuriwa na maelfu ya watu wakiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

**NAJUA WAJUA**



HAKUNA klabu ya Ligi Kuu England iliyoshuhudia wapinzani wao wakionyeshwa kadi nyekundu mara nyingi zaidi katika michuano yote kama Wolves (mara sita - ikiwa sawa na Aston Villa).

SOKA



Madaktari wakimtibu mgonjwa mwenye maambukizi ya coronavirus katika Hospitali ya Zhongnan, Wuhan nchini China, mji ambao virusi hivyo vilianzia. **PICHA: MTANDAO**

# CORONA INAVYODIDIMIZA UCHUMI SOKA LA ULAYA, DUNIA

**LONDON,** England

SOKA na matukio mengine ya michezo yameendelea kuathiriwa na mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa corona, COVID-19 ambavyo hadi jana imeripotiwa kuwa na wagonjwa 156,000 huku vifo vilivyotokana na janga hilo vikiwa zaidi ya 5,800.

**Ilianza Italia kusimamisha Ligi Kuu ya soka ya Serie A hadi Aprili 3 na kuna uwezekano mkubwa tarehe hiyo ikasogezwa mbele zaidi.**

Maamuzi ya Italia kusimamisha ligi na matukio mengine kimichezo na burudani pamoja na mikusanyiko yote ni baada ya nchi hiyo kuathirika zaidi barani Ulaya.

Hadi jana nchini Italia wachezaji takriban watano wametajwa kuwa na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, huku klabu ya Juventus ndiyo iliyoathirika zaidi.

Pia janga kama hilo limeikumba Ligi Kuu ya England, ambapo nayo imesimamisha mechi za ligi hiyo hadi Aprili 3 baada ya baadhi ya wachezaji wa ligi hiyo kupatikana na maambukizi ya virusi vya corona akiwamo winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi na Kocha Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta.

Mashindano yote ligi ya soka ya Ulaya, ikiwamo Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi ya Europa pia yameahirishwa.

Hadi sasa zaidi ya watu 156,000 wamepatikana na virusi vya corona katika nchi 123 kote duniani, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO). Idadi kamili ya vifo vya watu vikielezwa kufikia 5,800.

Kutokana na hilo makala haya yanaangalia namna corona inavyodidimiza uchumi wa soka barani Ulaya, twende sasa...

**3. KUPOTEZA MAPATO KWA KLABU**

Mauzo ya teketi yanachangia kutoka asilimia nne hadi 18.75 katika mapato ya mwaka ya klabu, na hilo huzifanya klabu kuiingiza kiasi kikubwa cha fedha.

Wakati mapato ya siku ya mechi kwa timu ndogo kama Bournemouth, yanaweza kulingana na mshahara wa mchezaji mmoja mkubwa kwa wiki, klabu kubwa kama Manchester United zinaingiza kiasi kama cha pauni milioni nne kwa mechi.

Wakati kiasi cha mapato hayo kinaonekana kidogo ukilinganisha na kile kinachopatikana kwenye matangazo, udhamini na mikataba, kusimamishwa kwa ligi hiyo au kucheza huku milango ikiwa imefungwa kunaweza kuziathiri klabu kwa miezi mingi ijayo.

**2. KAMPUNI ZA BIMA KUPOTEZA FEDHA**

Kusimamishwa kwa soka pia kunaweza kuwa na athari kubwa kwa mapato yanayotokana na utangazaji wa mechi kwenye televisheni. Bahati nzuri mikataba ya kutangaza mechi kwa mashirika makubwa ya utangazaji kama BBC, yanawawezesha kuingiza kipato kikubwa, sasa kusimamishwa huko kutawaathiri zaidi.

Wakati kampuni za bima zinaweza kuingiza fedha nyingi kutokana na ada ya kujiunga kulinda haki zao za matangazo, lakini sasa yanaweza kujikuta kwenye wakati mgumu zaidi wakati yatakapojikuta yakidaiwa fidia. Klabu zitalazimika kudai fidia kutokana na kupotea kwa mapato yao na kutoka kwenye kampuni za bima na hilo litasababisha kampuni nyingi za bima kujikuta kwenye wakati mgumu.

**1. ATHARI YA KIFEDHA KLABU ZINAZOPANDA, KUSHUKA**

Matokeo kwa klabu kushuka daraja na nyingine kupanda, bado msimu wake haujamalizika na kwa uhakika mwisho wake unaonekana ni wa kutisha. Kuna fedha nyingi ambazo klabu inazipata kutokana na bonasi ya kushinda mataji au kupanda daraja au kushuka.

Kwa mujibu wa ripoti ya Consultancy.uk, klabu zinazopanda Ligi Kuu thamani ya bonasi yao ni pauni milioni 170. Hii inamaana inaweza kubadilika kwa klabu ndogo ambazo hutumia fedha hizo kwa ajili ya kupanua timu zao dimbani kwa kununua wachezaji au uwekezaji mwingine.

Kwa upande mwingine, Deloitte Sports Business Group inakadiria kwamba klabu kushuka daraja kunazigharimu kwa kiwango cha juu cha pauni milioni 50 kwenye Ligi Kuu pekee. Klabu za Ligi Kuu kwa haraka zinaingiza kama pauni milioni 90 kwa msimu mmoja wa ligi kutoka kwenye fedha wanazozipata kutokana na mapato yatokanayo na haki za televisheni za ndani na masoko ya nje. Wakati timu zinazoshuka daraja zinapata fedha za kujikimu kama pauni milioni 40. Hivyo kusimamishwa kwa ligi hiyo kutaleta athari kubwa zaidi ya fedha kwa klabu.

BAO alilofunga Mason Greenwood dhidi ya LASK ya Austria wiki iliyopita, ni la tano kwake kwenye michuano ya Europa League msimu huu, hivyo kumfanya kuwa kinda wa kwanza Manchester United kuweza kufunga idadi kubwa ya mabao kama hiyo kwenye msimu mmoja wa michuano ya Ulaya.



NDANI YA 18

Nipashe
Spotika



NI moja kati ya vitu vya kuvutia zaidi katika kila msimu kuona klabu zikiwania nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. Huku Manchester City ikitarajiwa kutumikia adhabu ya kutoshiriki michuano hiyo ya Ulaya msimu ujao, hiyo imetoa nafasi kwa timu nyigine...

Uk. 16&17

# 4-BORA USAJILI WA JANUARI EPL 2020



**LONDON,** England

NI zaidi ya miezi kadhaa sasa tangu kufungwa kwa dirisha la usajili la Januari, na wachezaji wote walionunuliwa kwenye klabu za Ligi Kuu ya England wamekuwa na wakati mzuri kwenye timu zao mpya. Wengine wameonyesha matokeo mazuri, na wengine wakiwa kwenye wakati mgumu.

Endapo wachezaji hao wanaweza kuwa bora zaidi kwa usajili wa Januari kama ilivyokuwa kwa wachezaji kama Virgil Van Dijk, Pierre-Emerick Aubameyang, Luis Suarez na Nemanja Vidic - ni suala la muda.

Makala haya yanakuchambulia 4-bora ya usajili bora wa Januari 2020, shuka nayo...

**1. BRUNO FERNANDES**

Usajili wa Januari wa mchezaji huyu wa kimataifa wa Ureno, Bruno Fernandes pale Manchester United unaonekana kuwa mtamu sana kwao. Kiungo huyu mshambuliaji, ambaye alikuwa anawaniwa na 'Mashetani Wekundu' kwa muda, aliwagharimu kiasi cha pauni milioni 47 kutoka kule Sporting Lisbon, lakini tayari inaonyesha kwamba ada yao imezaa matunda.

Fernandes alianza kucheza kwenye mchezo ambao United walitoka sare ya bila kufungana na Wolves, Februari Mosi, na tangu hapo United imefanya vizuri zaidi kwenye mechi zake, na tayari kiungo huyo ana mabao matatu na pasi za mwisho tatu kwenye mechi zake nane za kwanza na klabu hiyo.

Zaidi ya hapo ni kwamba Fernandes anaonekana kukipa nguvu zaidi kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer na kuanza kuonyesha sasa wanakipata kile walichokuwa wakipata wakati wa utawala wa Sir Alex Ferguson. Na huu unaonekana unaweza kuwa usajili bora zaidi wa Januari kwa United.

**2. STEVEN BERGWIJN**

Alisajiliwa na Tottenham kwa pauni milioni 26.7 akitokea PSV Eindhoven, na winga huyu wa kimataifa wa Uholanzi, Steven Bergwijn ameonyesha ubora wake tangu kuanza kucheza chini ya Jose Mourinho na alikuwa shujaa kwa miamba hao wa London Kaskazini kwa kufunga bao wakati Spurs wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Manchester City na ni kiwango bora zaidi kwa klabu hiyo chini ya Mourinho.

Tangu hapo, Bergwijn ameonyesha kiwango cha kuvutia zaidi na kuisaidia Tottenham, ambao kwa sasa wanakabiliwa na majeruhi kadhaa akiwamo mshambuliaji wao Harry Kane na Son Heung Min.

**3. PEPE REINA**

Ulikuwa usajili wa kushangaza wa Januari wakati golikipa mkongwe Pepe Reina ambaye ameshinda mataji kadhaa kama vile Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Kombe la FA, Kombe la Dunia na lile la Ulaya akiwa na Hispania, alihamia Aston Villa kwa mkopo akitokea AC Milan. Usajili huo uliwashangaza mashabiki wengi, hasa kutokana na umri wa Reina mwenye miaka 37 akiwa amecheza mechi 12 tu katika msimu wa 2018-19.

Lakini sasa Reina anaonekana kuwa muhimu kwa kikosi hicho cha kocha, Dean Smith wakati timu hiyo ikipigania kutoshuka daraja pale Villa Park. Mchezo wake wa kwanza ulimfanya kuwa na kiwango bora zaidi wakati akiokoa hatari nyingi timu yake ikitoka sare ya kufungana bao 1-1 na Brighton na mchezo wa pili Villa walishinda 2-1 dhidi ya Watford ambao nao wanapigania kutoshuka daraja.

Reina pia alionesha kiwango cha kuvutia wakati Villa ikifungwa 2-3 na Tottenham huku yeye akiokoa hatari saba, lakini ingawa matokeo ya Villa hayavutii, yeye amekuwa na kiwango bora zaidi.


**4. JARROD BOWEN**

Baada ya kufunga mabao ya kuvutia kwenye mashindano ya EFL akiwa na Hull City, ambapo alifunga mabao 16 katika mechi 20 msimu huu lilikuwa jambo la lini Jarrod Bowen atacheza kwenye Ligi Kuu ya England. Wanaojikongoja West Ham ndio ilikuwa klabu iliyoamua kumsajili mshambuliaji huyo kwa pauni milioni 18.

Hadi sasa Bowen amefunga bao moja katika mechi zake nne alizocheza, lakini ameonyesha makubwa zaidi uwanjani na mashabiki wa 'Wagonga Nyundo' hao wa London wana matumaini naye makubwa sana.

Kikosi hicho cha kocha, David Moyes kwa sasa kinaonekana kuwa kwenye nafasi ya kupigana kutoshuka daraja, huku Bowen ndiye anayeonekana kubeba dhamana ya timu hiyo.

**USILOLIJUA**



MARCOS Llorente ni mchezaji wa pili Atletico Madrid kufunga mara mbili kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya Sergio Aguero kufanya hivyo dhidi ya Chelsea Novemba 2009, wakati akiichezea miamba hiyo ya Hispania.



## HABARI MBEYA




Mafundi wakiendelea na ujenzi wa stendi ya mabasi ya Tarafani katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya ambayo ilikuwa imetelekezwa muda mrefu na kusababisha adha kwa watumiaji kutokana na kujaa maji mara kwa mara. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waandishi habari wakumbushwa kiwango elimu kabla muda kuisha

**Na Grace Mwakalinga**

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, amewakumbusha waandishi wa habari ambao hawana elimu ya diploma kurudi shule kabla ya muda uliotolewa na serikali kumalizika.

Mtunguja alitoa kauli hiyo jana wakati wa sherehe za maadhimisho ya miaka 25 tangu kuanzishwa kwa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya (MBPC).

Alisema muda uliobakia ni vyema ukatumiwa vizuri kwa wanahabari ambao hawajakidhi matakwa ya kisheria yanayotaka kila mwandishi awe na kiwango cha elimu kuanzia diploma na kwamba msisitizo huo una lengo la kuboresha mazingira na maslahi ya wanahabari nchini.

"Nawaomba wanahabari wa Mkoa wa Mbeya wasiokuwa na sifa kwa mujibu wa sheria ya huduma ya vyombo vya habari warudi shule kabla panga halijapita, mkumbuke pia sheria mpya ya huduma ya vyombo vya habari ina lengo la kuwatetea ikiwamo kupata stahiki zenu, mikataba kwa waajiri na uhuru wa kupata taarifa," alisema Mtunguja.

Aliishauri klabu hiyo kuanzisha utaratibu wa kuomba fedha kwa wadau ili kuwasomesha wanachama.

Katika hatua nyingine, Mtunguja aliwashauri waandishi wa habari kujiingiza kwenye shughuli za ujasiriamali na kilimo ili kuwa na kipato cha uhakika badala ya kutegemea fedha za wahisani.

Katibu wa klabu hiyo, Godfrey Kahango, aliwaomba wadau na serikali kuwapatia eneo la kujenga ofisi ili kutekeleza majukumu yake bila vikwazo, huku akiwasisitiza pia kutoa ushirikiano wanapohitaji kupata taarifa.

Mdau wa Maendeleo mkoani Mbeya, Ndele Mwaselela aliwaahidi wanahabari kuchangia fedha na matofali kwenye ujenzi wa ofisi ya klabu hiyo.

Aliwashauri wanahabari kuacha kutumikia wanasiasa ambao wanatumia rushwa kupata madaraka na badala yake wajikite zaidi kuandika habari zinazozingatia misingi ya taaluma.

Baadhi ya waanzilishi wa klabu hiyo, Ulimboka Mwakilili, aliwaomba waandishi wenye uwezo wa kuongoza wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi mkuu ujao.

# TRA yaonya wafanyabiashara magendo mpakani

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imewataka wafanyabiashara na mawakala wanaofanya shughuli zao kwenye mpaka wa Kasumulu, wilayani Kyela ambao unazitenganisha nchi za Tanzania na Malawi, kuachana na biashara ya magendo kwa kuwa inaathiri uchumi wa nchi.

Meneja wa Elimu kwa Mlipakodi nchini, Diana Masalla, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akitoa elimu ya athari za biashara za magendo kwenye mipaka ya nchi.

Masalla alisema biashara za magendo kwenye mipaka ya nchi inachangia kuathiri uchumi wa nchi kwa sababu bidhaa zinazosafirishwa na kutumiwa zinakuwa hazijathibitishwa ubora wala kulipiwa kodi.

"Moja ya kazi kubwa ambayo TRA tumeivalia njuga kwa sasa ni kutoa elimu mipakani kwa wafanyabiashara na mawakala wa forodha kuwaeleza athari zitokanazo na biashara ya magendo kiuchumi na kiafya pia nawaomba wafuate taratibu zote ambazo zimewekwa kwa mujibu wa sheria za nchi," alisema Masalla.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa mlipakodi katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya lengo likiwa ni kuongeza uelewa wa masuala ya kodi na kutambua umuhimu wa kulipa kwa wakati.

Ofisa Elimu kwa Mlipakodi Mkoa wa Mbeya, Serapio Luanda, aliwataka mawakala wa forodha wanaojishughulisha na biashara ya kuondoa mizigo katika mpaka wa Kasumulu kutoa taarifa ya mapato yanayotokana na biashara zao.

Alisema utoaji wa taarifa mapema utaondoa usumbufu wa kila wakati kufuatiliwa na TRA ambao wanahimiza utoaji sahihi wa taarifa za mizigo na ulipaji wa kodi.

Miongoni mwa wafanyabiashara waliopatiwa elimu kwa mlipakodi, Ramadhani Msangi, alisema elimu hiyo, imesaidia kuongeza ari ya ulipaji kodi na kuwaomba TRA kuwatembelea mara kwa mara.

Alisema TRA wanapaswa kuwa karibu na wafanyabiashara ili wawaeleze vikwazo wanavyokutana navyo badala ya kuwatembelea wanapodai madeni.

## Waomba vifaa tiba hospitali ya wilaya

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WANANCHI wa Kata ya Mpuguso, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, wameiomba serikali kusaidia vifaa tiba katika kituo chao cha afya ili kuepukana na adha ya kutembea umbali wa kilometa 14 kufuata huduma za matibabu kwenye hospitali ya wilaya.

Wananchi hao walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakizungumza na Nipashe, walisema walitumia nguvu kazi zao pamoja na fedha ili kujenga kituo cha afya kwa lengo la kuondokana na adha ya kufuata huduma za matibabu kwenye Hospitali ya Makandana.

Walisema licha ya jitihada hizo za kukamilisha jengo, hitaji lao kwa sasa ni vitendea kazi vya kutolea huduma za matibabu pamoja na watumishi.

Miongoni mwa wananchi hao, Queen Ndile, alisema waliamua kuchangishana fedha kwa kila mwananchi ili kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya na kwamba hakuna kiwango maalumu walichokuwa wameweka ili kumfanya kila mmoja ashiriki.

"Tuliamua kuanza ujenzi wa kituo cha afya kwa nguvu zetu wenyewe baada ya kuchoka kutembea umbali mrefu wa kilometa 14 kufuata huduma za matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Makandani hapa tulipofikia sasa tunaomba serikali itusaidie kumalizia maana ni suala la kitaalamu," alisema Ndile.

Diwani wa Kata ya Mpuguso, Jarald Bakize, alisema Sh. milioni 140 ambazo zilichangwa na wananchi zimetumika katika ujenzi wa kituo hicho cha afya.

Alisema mfuko wa jimbo kwa kushirikiana na wadau wengine walichangia fedha katika ujenzi huo.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Challya, alipongeza jitihada za wananchi kujenga kituo cha afya bila kusubiri mchango wa serikali na kwamba katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 kuna fedha imetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi vya kutolea huduma.



# Mavunde arejesha furaha kwa wenye ulemavu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, amefungua kambi maalumu ya upimaji vifaa tiba saidizi na utengenezaji wa miguu bandia yenye lengo la kurejesha furaha na matumaini kwa watu wenye ulemavu.

Kambi hiyo inaendeshwa na Ofisi ya Mbunge kwa kushirikiana na Taasisi ya People Empowerment Foundation, iliyo chini ya Kampuni ya Kamal Group.

Akizungumza katika uzinduzi wa kambi hiyo, Mavunde ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, alisema hakuna sababu ya watu wenye ulemavu kukata tamaa na maisha kwa kuwa vipo vifaa saidizi vinavyoweza kuwasaidia kufikia ndoto zao.

Alisema kuna watu wamepoteza furaha na tumaini kutokana na kukosa vifaa saidizi, hivyo kupitia huduma hiyo wengi watarejesha furaha na kufikia ndoto zao.

"Niwaombe mhimizane watu waje kupata vipimo na kutengenezewa huduma hii ni bure hakuna atakayedaiwa hata senti moja, tumeleta huduma hii kwa sababu serikali ya awamu ya tano inawajali watu wenye ulemavu na wenye mahitaji na njia pekee ni kurejesha furaha, na mimi moja ya kazi ninazopenda kuzifanya ni kurejesha matumaini kwa watu," alisema.

Alisema angetamani kuona furaha hiyo inakuwa kwa Watanzania na wananchi wa mikoa mingine wachangamkie fursa hiyo.

"Watu wanafikiri kupata ulemavu ni mwisho wa maisha na wanakata tamaa, kama yule mtu aliweza kupanda mlima mrefu duniani na nyie hamuwezi kushindwa kufikia mafanikio mnayoyataka kuyafikia, huduma hii ni ya mkoa mzima na wananchi wa mikoa mingine lengo ni kuhudumia watu bila kuangalia wanapotoka," alisisitiza.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Kamal Sameer Santoji, alisema, kampuni yake iliamua kupeleka huduma hiyo kwa wahitaji baada ya kupokea ombi kutoka kwa Mavunde akihitaji kusaidia miguu bandia kwa ajili ya wananchi wa jimbo lake.

Alisema kutokana na uhitaji wa watu wengi, kampuni hiyo imejiandaa kutoa huduma hiyo kwa watakaojitokeza kwenye kambi hiyo bila kujali mkoa anaotoka.

"Hakuna haja ya kukata tamaa watu wengi wenye ulemavu wamepata mafanikio makubwa kama yule aliyepanda mlima mrefu duniani hakuna kitu kinachoshindikana ukihitaji mafanikio," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Dodoma, Dk. Ernest Ibenzi, alisema viungo saidizi vinawawezesha watu wenye ulemavu kufanya kazi zaidi ya wenye viungo vyote.

"Mguu bandia unamsaidia mtu kutoka eneo moja kwenda eneo jingine kwa urahisi kuliko kama angetumia magongo na wakati mwingine mwenye viungo saidizi anafanya kazi kuliko mtu ambaye hana ulemavu wowote," alisema.



Wananchi wakiangalia gari namba za usajili T.821 DSY iliyopata ajali na kutumbukia kwenye mtaro wa maji nje ya Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) eneo la Makole jijini Dodoma jana. Hata hivyo, hakuna aliyefariki dunia. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wenye maduka ya nyama waonywa utumiaji magogo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BODI ya Nyama imewaonya wafanyabiashara wa soko la Majengo jijini Dodoma kuacha kutumia magogo kwenye ukataji wa nyama ili kulinda afya za walaji.

Akizungumza katika ziara ya kushtukiza kwenye soko hilo, Kaimu Msajili wa Bodi hiyo, Iman Sichalwe, alisema imebainika bado kuna wafanyabiashara wanaotumia magogo na kuwataka kuacha mara moja.

"Tuliagiza Septemba 9, mwaka 2019 wafanyabiashara kuacha kutumia magogo na badala yake watumie mashine za umeme au kifaa malumu katika kukata nyama," alisema.

Alisema katika ukaguzi huo wamebaini magogo hayo yanahifadhi uchafu kwa muda mrefu jambo linalohatarisha afya za walaji.

"Inaweza kutengeneza vijidudu vinavyo sababisha magonjwa ya kuhara hivyo ni hatari kwa afya za walaji," alisema.

Alisema utumiaji wa panga na shoka katika kukata nyama sio salama kutokana na chembe za mifupa kubaki kwenye nyama na kuhatarisha afya za walaji.

Naye Mshauri wa mifugo mkoa, Goodluck Ndaweka, aliwataka wafanyabiashara kuzingatia kanuni za usafi.

"Mkifuata taratibu na sheria hakutakuwa na tatizo lolote kwenu na pia mtafanyakazi kwa uhuru na wateja watapata huduma inayostahili kwa vigezo vyote," alisema Ndaweka.

Akizungumza kwa niaba ya wamiliki wa bucha, Charles Laiza, alisema mashine haziwezi kukata nyama kubwa na kuomba vitafutwe vifaa mbadala ya magogo.

"Nyama zingine ni kubwa sana haziwezi kukatwa kwa mashine na kama kuna mbadala basi iweze kukata nyama na iwe na uwezo kama wa gogo," alisema.

# Watumishi wa Lita wapewa somo

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

SERIKALI imetaka watumishi wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA), kutatua kero zinazowakabili wafugaji ili kuwa na ufugaji wa kisasa.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, alipokuwa akifungua baraza la saba la wafanyakazi wa LITA, jijini hapa. Alisema watumishi wa sekta ya mifugo ni moja ya chachu kubwa katika kutatua kero za mfugaji nchini.

"Ninyi ni fursa muhimu sana katika kushauri programu na kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya mifugo, hivyo baraza ndiyo chimbuko la fikra kwa kuleta mapinduzi makubwa katika sekta hii ya mifugo na kuwa chachu muhimu zaidi kutatua kero za mifugo nchini," alisema.

Alisema watumishi katika sekta ya mifugo walio na ngazi ya astashahada na stashahada wanafanya bidii katika kuwahudumia wafugaji ikilinganishwa na watumishi wenye shahada kwa kuwa baadhi ya watumishi wenye elimu ya juu wanajiona wako hadhi ya juu kumhudumia mfugaji wa kawaida.

"Wakati umefika kwa watumishi bila kujali elimu waliyo nayo kubadilika na kuwa karibu katika kumhudumia mwananchi wa kawaida," alisema.

Kadhalika, aliwataka wafugaji na Watanzania kuwa na desturi ya kugharamia na kuhudhuria kozi ya muda mfupi namna ya ufugaji bora ili kuwa na ufugaji wenye tija.

Awali, Mwenyekiti wa Baraza hilo, Dk. Pius Mwambene, alisema kuna kero mbalimbali hasa za miundombinu pamoja na upungufu wa wakufunzi takribani 34 wa afya ya mifugo.

"Juhudi zinafanyika ikiwa ni pamoja na ukarabati wa miundombinu na kubuni biashara, mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji katika kukabiliana," alisema.

Mkurugenzi wa utafiti, mafunzo na ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Angello Mwillawa, alisema utafiti una mchango mkubwa katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya sekta ya mifugo, husaidia kuweka mikakati ya kukabiliana na kero zinazoweza kujitokeza.





Meneja wa kitengo cha kudhibiti maradhi kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Asha Ussi Khamis, akitoa mada kuhusu ugonjwa wa corona katika mafunzo ya siku moja kwa waandishi wa habari kuhusu ugonjwa huo na hatua zinazochukuliwa. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ kuzindua kiwanda kila mwezi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, amesema wizara hiyo itahakikisha kila mwezi inazindua kiwanda kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na kukuza uchumi wa nchi.

Alisema nguvu mpya ya serikali ni kuhakikisha Zanzibar inakuwa nchi ya viwanda ambavyo vinaongeza thamani ya mazao yanayozalishwa nchini.

Hayo aliyaeleza alipokuwa akizindua biashara ya chumvi chapa ya ZALT inayotengenezwa Pemba chini ya Kampuni ya Swahili Coast Salt Company (SCSC), hafla iliyofanyika Shangani mjini Unguja jana.

Alisema sera ya wizara hiyo inaangalia viwanda ambavyo vinawagusa watu wengi na vinavyoongeza thamani ya bidhaa lengo likiwa ni kila mwananchi awe anafaidika na uchumi katika eneo lake.

Alisema, sera hiyo iliyotolewa hivi karibuni ya mwaka 2020/2030 inaeleza wazi juu ya azma hiyo ya serikali katika kuhakikisha maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

"Kama hii chumvi imeingia kwenye mzunguko mzima wa thamani, imetiwa viungo na ipo kwenye ubora wa kushindana kwenye soko la kimataifa," alisema. Alieleza kiwanda hicho pia kitasaidia ajira kwa wazalendo ambapo tayari kuna makundi 20 yanayolima chumvi kwa ajili ya kiwanda hicho cha kisasa.

"Yapo makundi karibu 56 yanayolima chumvi Unguja na Pemba, sasa utaona namna ajira itakavyowezwa kutengenezwa baada ya kiwanda hichi kujengewa njia bora," alisema.

Balozi Amina alisema umefanyika utafiti na kubaini kuwa chumvi ya Pemba ina soko kubwa, hivyo kuanzishwa viwanda vya kusindika kuiongezea thamani iuzwe kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi, ni tija kwa taifa. "Mtazamo wetu hivi sasa ni kuipeleka chumvi ya Zanzibar kwenye soko la kimataifa, lakini itakuwa fursa iliyopo katika viungo vinavyopatikana ikiwamo hiliki, karafuu na mdalasini."

Hivyo, Waziri Amina alisema ikiwa wananchi watatumia vyema fursa za upatikanaji wa viungo nchini wanaweza kutajirika kutokana na uhitaji wake mkubwa katika masoko ya kimataifa.

Aidha, Waziri Amina aliwahakikishia wawekezaji kwamba serikali itaendelea kuwaunga mkono na kuwa nao pamoja katika kuhakikishia malengo yao ya kiuwekezaji yanafikiwa.

Naye kiongozi wa kampuni hiyo ya uwekezaji, Stephanie Said, alisema, mradi huo unafanyakazi kwa karibu jamii ya Zanzibar, ukiwapa zaidi nguvu na fursa vikundi vya wajasiriamali wa Pemba ili kuboresha viwanda vya chumvi kisiwani humo.

Alisema, wakifanyakazi na wazalishaji wa chumvi wa Pemba na wataalamu wa kuvuna chumvi duniani, SCSC inarudisha uhai wa tamaduni za zamani na mbinu za kuvuna chumvi kiasili kwa kutumia jua.

"Chumvi yetu inatengenezwa katika hali ya kipekee na hajatiwa kemikali za aina yoyote...pia chumvi hii huvunwa moja kwa moja kutoka baharini na kuandaliwa kwa mikono. Uandaaji huu unahifadhi ladha halisi na virutubisho vyake," alisema.

Alieleza kuwa lengo lao kuu ni kuunda mfumo wa ukuzaji wa ujasiriamali na biashara endelevu na kwamba kampuni hiyo inatoa fursa kwa wazalishaji kupata soka la kuuza chumvi ili kujenga maendeleo.

Mkurugenzi wa Uwezeshaji wa Mamalaka ya Vitega Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Shariff Ali Shariff, alisema ni jambo la faraja kuzindua biashara hiyo ambapo sera ya serikali ni kuwa na viwanda vya kutosha kutokana na umuhimu wa uchumi.

# Vibali kusafirisha mazao vyahimizwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kufuata taratibu za kukata kibali cha kusafirisha mazao wanapoyasafirisha kwenda sokoni.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kati Unguja, Mohammed Salum Mohammed, baada ya kukamatwa kwa mazao ya biashara yanayosafirishwa kinyume na taratibu za kisheria kutoka maeneo mbalimbali.

Alisema hali hiyo imekuwa inakosesha mapato serikali ambapo mapato hayo husaidia katika shughuli mbalimbali za kijamii kwa ajili ya maendeleo.

Alisema taratibu za kukata vyeti cha mazao kwa mwananchi anayesafirisha mazao hayo zipo kisheria na zinapelekea kuongezeka kwa pato la serikali na kusaidia kudhibiti wizi wa mazao yanayoibiwa mashambani na kusafirishwa kupelekwa sokoni.

Naye Sheha wa Shehia ya Bambi, Amour Pandu Mkombe, alisema serikali haina lengo la kuwaonea wananchi wake bali taratibu hizo zimewekwa kwa maslahi ya wananchi na mazao yao kutokana na kuwapo kwa ongezeko la kesi za kuibiwa mazao na kusafirishwa kupelekwa sokoni.

Kwa upande wao wananchi waliokamatwa kwa kusafirisha mazao bila ya kibali wameiomba serikali kuwapunguzia gharama za ukataji wa kibali cha kusafirisha mazao.

# Serikali yatoa neno wanufaika Tasaf

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI wanaonufaika na mpango wa kaya maskini kupitia Mfumo wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) wametakiwa kuiunga mkono serikali kutokana na mchango mkubwa inaoutoa kwa wananchi wake ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kupunguza umaskini nchini.

Wameelezwa kuwa kufanya hivyo kutasababisha serikali ya Zanzibar na Tanzania kuongeza jitihada zaidi katika suala zima la kuwawezesha wananchi katika kuwaunganisha pamoja ili kushirikiana katika kuibua miradi itakayowasaidia kujiongezea kipato na kuimarisha maisha yao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hudumu ya Baraza la Wawakilishi inayoshughulikia ofisi za viongozi wakuu, Panya Ali Abdalla, alieleza hayo katika ziara maalum iliofanywa na kamati hiyo kuangalia na kukagua miradi iliyobuniwa na walengwa wanaonufaika na mpango wa kaya maskini kwa upande wa Mkoa wa Kusini Unguja. Alisema mpango wa kunusuru kaya maskini umesaidia kwa kiasi kikubwa kuuleta umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi wengi Tanzania. Hali inayopelekea urahisi wa utekelezaji wa mipango ya serikali. Panya aliwataka viongozi wanaosimamia Mfuko wa Tasaf Zanzibar kuongeza umakini kuhakikisha fedha zinazotolewa zinawafikia walengwa na kusimamia matumizi ili lengo la serikali la kuondosha changamoto zinazowakabili wananchi wake lifikiwe. Alieleza kuwa mpango wa kunusuru kaya maskini umekuja kuleta ukombozi kwa wananchi wa Tanzania, na kuna mafanikio makubwa yaliopatikana kwa walengwa hususani kinamama baadhi yao wamefikia hatua ya kujenga nyumba pamoja na kusomesha watoto pamoja na kukidhi mahitaji yao madogo.

Naye mjumbe wa kamati hiyo ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mihayo Juma N'hunga, aliwashauri walengwa wanaonufaika na mpango huo pamoja na miradi walioianzisha ikiwamo mradi wa upandaji wa miti, kuna haja sasa ya kuangalia uwezekano wa kuanzisha miradi ya mazao ya matunda.

Mihayo alieleza endapo walengwa watajikita katika uzalishaji wa mazao ya matunda wataweza kupata mavuno na mafanikio makubwa ndani ya muda mfupi kutokana na uzalishaji wa mazao hayo kuchukua kipindi kifupi.

Aliwahakikishia viongozi wa shehia kwamba kupitia utekelezaji wa Tasaf awamu ya tatu kipindi cha pili serikali itaangalia uwezekano wa kuwaorodhesha wananchi wengine ili nao waweze kunufaika na mpango huo kama waliovyonufaika wananchi wengine. Mratibu wa Tasaf Unguja, Makame Ali Haji, alisema kufuatia ziara, yapo mapendekezo ya kufanywa kwa tathmini ya utekelezaji wa mpango huo.

# Wanusurika kifo kwa kukatwa mapanga

**Na Ndalike Sonda,**
KAHAMA

WAKAZI watatu wa Kijiji Cha Nyandekwa katika Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, wamenusurika kuuawa kwa kukatwa mapanga, baada ya kuvamiwa na watu wanaodhaniwa ni majambazi.

Imeelezwa kuwa mmoja wa majeruhi hao hali yake ni mbaya.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi, na kwamba kati ya waliojeruhiwa, wawili ni wanandoa ambao ni Magema Magazi (66), na Limi Ntabo (62) na Kubyula Joseph (32).

Shuhuda wa tukio hilo, Msibu Magema ambaye ni mtoto wa Magema, alisema watuhumiwa hao ambao hawajafahamika idadi wala majina, walianzia kumshambulia kwa mapanga mama yake mzazi kisha baba yake mzazi, na kwamba baada ya kukosa fedha walikwenda nyumba jirani ya Joseph.

"Majambazi yalipiga mlango ukafunguka, yakaanza kumpiga kwanza mama na kumwambia atoe pesa na baadaye yakaanza kumpiga baba na kumkata mapanga kichwani, na sehemu zingine za mwili za begani, jicho la kushoto, baba alianguka na kuzimia na yalipokosa pesa yakaenda nyumba jirani kwa Joseph nako yakagonga mlango na kumvamia," alisema Msibu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, Dk. George Masasi, alisema walipokea majeruhi watatu alfajiri ya juzi wanaume wawili na mwanamke mmoja, lakini kati yao wawili wameruhusiwa baada ya hali zao kuendelea vizuri, na kuwa Magema Magazi anaendelea na matibabu kutokana na kujeruhiwa vibaya.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Deborah Magiligimba, akizungumza kwa njia ya simu na Nipashe, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema kuwa atatoa taarifa kamili baadaye.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azzan Zungu (kulia), akizungumza na wafanyabiashara wa chuma chakavu (hawapo pichani) jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuwapo kwa mfumo mpya wa utoaji vibali kwa njia ya mtandao. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka: **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# Wachakataji dagaa walia ugumu vibali

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

WACHAKATAJI wa zao la dagaa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki Tanzania, Uganda, Kenya na Burundi wameomba kurahisishiwa upatikanaji vibali vya kusafirisha bidhaa hiyo kutoka ndani ya nchi kwenda nje.

Aidha, wameomba kutafutiwa vitendea kazi vya kisasa pamoja na kujengewa kiwanda kimoja cha vifungashio kitachokuwa cha jumuiya ili waweze kupata vifungashio kwa bei nafuu.

Mwenyekiti wa Mtandao wa wanawake wanaochakata dagaa, Beatrice Mbaga wa Tanzania na Gabriel Butoyi kutoka Burundi wakizungumza baada ya mafunzo ya kwa kinamama na vijana ya namna bora ya uchakataji wa samaki aina ya dagaa ili kuongeza thamani ya bidhaa hiyo, walisema matatizo yaliopo kwa wachakataji yanafanana kwa nchi zote, hivyo wanahitaji vitendea kazi vya kisasa pamoja na kiwanda cha kutengeneza vifungashio vinavyokidhi vigezo kwa nchi zote na upatikanaji wake uwe wa bei nafuu.

Walisema utitiri wa ushuru sehemu mbalimbali pamoja na upatikanaji wa vibali kutokuwa sehemu moja ni changamoto kubwa ambayo wakati mwingine huchangia kuwa nje ya muda dagaa kuharibika, hasara, mitaji kukatika na upandishaji wa bei kwa walaji.

"Hii ni sekta moja ni vyema vibali vyote vikapatikana sehemu moja sio kama ilivyo sasa, ukienda kwenye mwalo kulangua samaki jinsi ya kupata vibali ndio changamoto kimoja unachukua hapa vingine sehemu nyingine," alisema Butoyi.

Dk. Shigela Mahongo, Mtendaji Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inayohusika na uvuvi endelevu, aliwaomba wachakataji hao wa dagaa kulipa thamani zao hilo linalilopatikana kwa asilimia 60 kwa mazao yote ya samaki wanaovuliwa Ziwa Victoria ili kuongeza kipato chao.

Naye Katibu Mtendaji Bonde la Ziwa Victoria, Dk. Saidi Matano, akizungumzia taarifa mbalimbali zinazotoka zikieleza Ziwa Victoria ni chafu, alisema maziwa yote duniani yanakabiliwa na changamoto ya uchafuzi wa ziwa na kueleza kuwa maji ya Ziwa Victoria ni safi na mazingira yake wanawezesha samaki na dagaa kukua kwenye mazingira safi.

Akifunga mafunzo hayo Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, aliwataka wachakataji hao wa dagaa kutumia vizuri mbinu walizopewa ili dagaa waweze kuuzika katika masoko ya kimataifa.

# Mipakani waonywa magendo mifuko plastiki

**Na Mwandishi Wetu,** TUNDUMA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewaomba wananchi wanaoishi maeneo ya mipakani kuchukia kuingizwa kwa njia ya magendo mifuko na vifungashio vya plastiki ambavyo serikali imepiga marufuku ili kulinda mazingira na viwanda vinavyotengeneza nchini mifuko na vifungashio vilivyoruhusiwa.

Akizungumza mjini hapa, wakati wa ziara ya siku ya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa amri ya serikali ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko na vifungashio vya plastiki na ustawi wa biashara ya mifuko mbadala, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema Sheria ya Mazingira ya 2004 na Kanuni zake lazima zifuatwe ili kulinda mazingira ya Tanzania.

"Ulinzi wa mipakani ni muhimu uimarishwe ili kuzuia kuingiza kwa magendo wa mifuko kutoka nje. Tunatarajia wananchi washio maeneo ya mpakani mchukie biashara ya magendo ya aina hii na mfichue wanaofanya biashara hii kwa mamlaka husika, maana mifuko ya plastiki na vifungashio vinavyoingizwa nchini kwa njia ya magendo vitayadhuru mazingira na kuua soko la wazalishaji wa ndani," alisema.

Alisema wananchi washirikiane na vikosi kazi vya mazingira vilivyopo katika kila mkoa kuzuia mifuko ya plastiki kuingia na kutumika nchini, na kuviuomba vikosi kazi kuendeleza elimu juu ya umuhimu wa kutumia mifuko mbadala katika utunzaji wa mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadaye. "Matumizi ya mifuko mbadala yenye kiwango cha GSM70 yanahimizwa kwa sababu yanalenga kulinda wazalishaji wa ndani na pia kwenda sambamba na azma ya serikali ya awamu ya tano ya ujenzi wa uchumi wakati na viwanda. Hivyo ni lazima tuilinde mipaka yetu na kuzuia biashara ya magendo ya mifuko ya plastiki kwani biashara hiyo itazorotesha soko la ndani la mifuko mbadala," alieleza.

Akigusia azma ya NEMC ya kuhakikisha utekelezaji wa katazo la serikali unafanyika kwa utaratibu mzuri, alisema baraza limetoa mwezi mmoja kuhakikisha matumizi, uzalishaji na usambazaji wa vifungashio vya plastiki vinasitishwa ili vifungashio mbadala vitumike kwa lengo la kulinda mazingira.

Jestina Mwalupengo, mkazi wa Tunduma, alisema matumizi ya mifuko ya plastiki bado yapo katika eneo lao na kudai kwamba mifuko hiyo inatoka nchi jirani.

"Tutaendelea kuhamasishana wenyewe ili kuzuia mifuko isiingizwe nchini. Matokeo ya mifuko iliyopigwa marufuku tunayaona hapa. Ni mazuri kwani yamefanya mazingira kuwa salama tofauti na hali ilivyokuwa kabla ya katazo," alisema Mwalupengo.

Lasmos Muyinga, mfanyabiashara ndogo Tunduma mjini, aliipongeza serikali kwa kukataza matumizi ya mifuko ya plastiki nchini na kueleza kwamba hali ya mazingira ilikuwa mbaya sana kutokana na mifuko hiyo kuzagaa ovyo.

# Rwanda yafunga shule, makanisa, misikiti kudhibiti corona

**KIGALI,** Rwanda

SERIKALI ya Rwanda imetangaza kuchukua hatua kadhaa za dharura kukabiliana na janga la ugonjwa virusi vya corona ikiwamo kufunga shule zote kwa muda wa siku 14.

Hatua hiyo imekuja baada ya kutangaza kwamba raia mmoja wa India aliyewasili nchini humo Machi 8, kuthibitishwa kuwa na virusi vya ugonjwa wa corona.

Katika mahojiano na Radio Rwanda, Mawaziri Anastase Shyaka wa Mambo ya Ndani na Dk. Ngamije Daniel wa Afya, walisema kuwa hatua hizo ni pamoja na kufungwa kwa shule zote za umma na za kibinafsi, maeneo ya kuabudu na sehemu zote za umma.

Hatua hiyo inaanza kutekelezwa kuanzia jana.

Shyaka (pichani) alisema kwamba pia makasisi wanaelewa ukubwa wa janga hilo ambalo Rwanda na dunia nzima inakabiliana nalo.

Miongoni mwa hatua hizo, Shyaka alisema kwamba matukio kama vile mikusanyiko ya watu katika maeneo ya michezo na harusini ambayo yameahirishwa na kwamba wale waliopoteza wapendwa wao watazikwa kwa namna ya kipekee.

Shirikisho la Soka la Rwanda (FERWAFA), pia limetangaza kwamba michuano yote kwa sasa itafanyika bila kuhudhuriwa na mashabiki katika viwanja vya michezo, huku shirikisho la mpira wa mkono nchini humo likiahirisha michezo yake yote.



Waziri Shyaka pia alitoa wito kwa raia kuepuka mikusanyiko katika maeneo ya migahawani na masokoni.

Katika usafiri wa umma, Shyaka alisema kwamba hakuna abiria atakayeruhusiwa kusimama na kutoa wito kwa watu wa eneo na vikosi vya usalama kusaidia kuhakikisha hatua hizo zinatekelezwa.

Kwa upande wake Dk. Ngamije, alisema kwamba hatua hizo zitasaidia katika kukabiliana na ugonjwa wa virusi vya corona na kutoa mfano wa maeneo mengine kama vile Hong Kong na Singapore ambako zimezaa matunda. **BBC**

# Sherehe za Pasaka Vatican kutohudhuriwa na waumini

**VATICAN,** Italy

TAARIFA iliyotolewa jana na makao makuu ya Kanisa Katoliki mjini Vatican imesema sherehe za kitamaduni za Wiki ya Pasaka hazitohudhuriwa na waamini kutokana na tishio la virusi vya corona.

**Italia ndiyo taifa lililoathiriwa vibaya barani Ulaya na mlipuko wa corona.**

Idara katika ofisi ya kiongozi mkuu wa Kanisa Katoliki ilieleza kuwa kutokana na dharura ya kiafya duniani, sherehe zinazofahamika pia kama Liturujia ya Wiki Takatifu ya Pasaka itafanyika bila ya kuwapo makundi ya watu.

Vatican pia imesema mikusanyiko ya watu na sala ya Malaika wa Bwana ambayo huongozwa na Papa Francis itafanyika kwa njia ya mtandao hadi Aprili 12.

Kulingana na takwimu zilizotolewa hadi jana watu 1,441 wamekufa nchini Italia kutokana na maradhi ya ugonjwa wa virusi vya corona huku wengine 21,000 wameambukiwa virusi hivyo.

Italia ndiyo taifa lililoathiriwa vibaya barani Ulaya na mlipuko wa virusi vya corona, huku taifa la China likiwa la kwanza. **DW**



Waziri Mkuu wa Canada, Justin Trudeau (kulia) na mkewe, Sophie Grégoire ambaye ameugua ugonjwa a virusi vya corona wakiwa pamoja. **PICHA: REUTERS**

# Mahakama yafunga shughuli kisa corona

**NAIROBI,** Kenya

SEKTA ya mahakama nchini Kenya imechukua hatua ya kufunga baadhi ya shughuli zake kufuatia taarifa ya kupatikana na mtu wa kwanza mwenye virusi vya corona nchini humo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Jaji Mkuu nchini humo David Maraga alisema kuwa mahakama inasitisha uendeshaji wa kesi ndogo kwa muda wa siku 14.

Aidha, alisema kuwa wafungwa waliopo lumande hawatafikishwa mahakamani na badala yake wenye makosa madogo, Kamishna Mkuu wa Polisi atawatoza faini katika kituo cha polisi, kulingana na mwongozo utakaotolewa.

Alisema kuwa majaji hawatapewa mafunzo kwa kipindi cha siku 14 na safari za nje ya nchi zimesitishwa.

Wakati huo huo, makazi ambayo aliishi mtu aliyepatikana na ugonjwa wa virusi vya corona yamekuwa yakinyunyiziwa dawa ya kuua wadudu na wale waliobainika kuwa wametangamana na mgonjwa huyo wametengwa kwa ajili ya uchunguzi.

Hali ya wasiwasi imetanda nchini humo kufuatia kutangazwa kwa kisa cha kwanza cha mlipuko wa ugonjwa wa vurusi vya corona huku baadhi ya wakazi wa Jiji la Nairobi wakionekana kununua bidhaa kwa wingi kwa hofu ya kuzikosa baadaye iwapo mlipuko utaendelea kusambaa.

Upande wa kesi kubwa mahakama imesema kuwa zitahudhuriwa na wahusika wa kesi pamoja na mawakili wao, na usalimianaji wa mikono na kukumbatiana vimepigwa marufuku katika maeneo ya mahakama.

Siku ya Alhamisi Waziri wa Afya nchini humo, Mutahi Kagwe, alitangaza kwamba mtu mwenye maambikizi ya virusi vya corona alithibitishwa kuwa ana maambukizi hayo Alhamisi usiku.

Kisa hicho ni cha raia wa Kenya aliyewasili nchini humo kutoka Marekani kupitia mjini London nchini Uingereza Machi 5, mwaka huu. Mtu huyo aligunduliwa kuwa na virusi hivyo katika maabara ya Wizara ya Afya nchini Kenya.

Hata hivyo, waziri huyo wa afya alisema kwamba mgonjwa huyo ambaye ni mwanamke yuko katika hali njema na kwamba viwango vyake vya joto vimeshuka na kuwa vya kawaida.

Aliwahakikishia Wakenya kwamba serikali imejiandaa vilivyo kukabiliana na virusi hivyo tangu kisa cha kwanza kitangazwe nchini China, akiongezea kuwa watatumia raslimali zake zote kukabiliana na janga hilo. **BBC**

# Marekani yalipa kisasi dhidi ya wanamgambo

**BAGHDAD,** Iraq

MAREKANI imefanya mfululizo wa mashambulizi ya kulipiza kisasi dhidi ya wanamgambo wa Iran ikijibu shambulizi la roketi lililogharimu maisha ya askari wake wawili na mmoja wa Uingereza katika kambi ya jeshi Kaskazini mwa Baghdad.

Mapema jana mchana, Pentagon iliwanyooshea kidole cha lawama wanamgambo wanaounga mkono serikali ya Iran kwamba walihusika katika shambulio hilo dhidi ya kambi ya Jeshi ya Taji, shambulio ambalo pia lilijeruhi watu 14.

"Marekani imefanya mashambulizi ya kujihami dhidi ya mitambo ya kundi la Kataib Hezbollah kote nchini," ilisema taarifa ya Pentagon na kuongeza kuwa:

"Mashambulizi hayo ni jibu la moja kwa moja kwa tishio lilifanywa na wanamgambo wa Kishia wanaoungwa mkono na Iran".

Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Mark Esper, alinukuliwa katika taarifa hiyo, akiionya kwamba Marekani itachukua hatua muhimu kulinda vikosi vyake nchini Iraq na katika ukanda wa Mashariki ya Kati. **RFI**

# Kairuki avuta wawekezaji wa Sweden

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, ameyaainisha maeneo na sekta mbalimbali zenye fursa lukuki wa uwekezaji nchini na kuwataka wafanyabiashara na wewekezaji kutoka Sweden kuja na kuchangamkia fursa hizo.

Mbali ya kuwapo kwa fursa hizo, Waziri Kairuki ameitaja miradi mikubwa mitatu ambayo serikali inatekeleza katika juhudi yake ya kuweka miundombinu imara na wezeshi katika ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

Akizungumza katika Kongamano la Biashara na Uwekezaji la Afrika Mashariki na kuhudhuriwa na wafanyabiashara na wewekezaji kutoka Sweden jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki ambapo Waziri Kairuki alimwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliwahakikishia wawekezaji hao kuwa serikali imeshachukua hatua mbalimbali muhumu ikiwemo kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji wakiwamo wa Sweden.

"Serikali inatekeleza miradi mikubwa mitatu ambayo ni ujenzi wa reli ya kisasa, ujezi wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa maji wa Julius Nyerere na upanuzi wa viwanja vya ndege hapa nchini sambamba na kuendelea kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na kuwekeza," alisema Kairuki.

Alisema serikali ipo katika hatua za mwisho kurekebisha Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 1996 na Sheria ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 1997 ili ziendane na mabadiliko ya kidunia ya uwekezaji.

Waziri Kairuki alisema Tanzania imejaliwa kuwa na fursa na vivutio vya utalii duniani na hivyo kuwaomba waje kuwekeza katika maeneo hayo mbapo alisema kuna maeneo yaliyotengwa maalum kwa uwekezaji.

Alisema sekta ya utalii inakuwa kwa kasi kubwa na inachangia asilimia 17.2 katika pato la taifa kwa sasa. Tanzania ina mbuga za wanyama 16, maeneo tengefu 28, maeneo maalum ya uhifadhi 44, maeneo ya hifadhi ya bahari mbili.

Alisema zipo fursa nyingi za kuweza katika sekta za usafiri majini, uvumbuzi na uchimbaji wa gesi asilia katika kina kirefu cha baharini, utalii wa maeneo ya pwani, uvuvi katika bahari na katika maji baridi yaani kwenye maziwa na mito.

Waziri Kairuki aliwakaribisha wawekezaji kuja pia kuwekeza kwenye viwanda vya kuchakata na kuzindika mazao kwani alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na ardhi kubwa na yenye rutuba kwa mazao ya aina mbalimbali.

Kongamano hilo liliwaleta wawekezaji kutoka Sweden ambao walikutana na wenzao wa Tanzania, ambapo walipata fursa ya kipekee kusikiliza mada mbalimbali zilizoainisha maeneo na sekta mbalimbali zenye fursa za kuwekeza hapa nchini




Mkuu wa Mtandao wa Matawi wa Benki ya Absa Tanzania, John Beda (wa pili kulia), akisoma jina la mmoja wa washindi wa droo ya kwanza ya promosheni ya akaunti ya mshahara ya benki hiyo iliyopewa jina la 'Ongeza Mshahara wako' jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine kutoka kushoto ni Mkuu wa Bidhaa kwa Wateja Rejareja, Heristraton Genesis, Mkaguzi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Rasuli Masudi, na Meneja Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Beda Biswalo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ocode yakabidhi shule madawati, darasa

**Na Julieth Mkireri**

SHULE ya Msingi Kibwegere inakabiliwa na upungufu wa miundombinu ya vyumba vya madarasa na ofisi za walimu.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Charles Kulemba, alisema mwishoni mwa wiki wakati wa makabidhiano ya madawati na darasa lililojengwa na Organization Community Development (Ocode).

Alisema, kwa muda mrefu wanakabiliana na ukosefu wa ofisi za walimu na vyumba vya madarasa, wakati mwingine inawalazimu walimu kufanyia kazi zao wakiwa wamekaa chini ya miti.

Kulemba alisema, msaada huo ulitolewa na Ocode utawasaidia kupunguza uhaba huo na kuomba wadau wa maendeleo kuendelea kusaidia kutatua changamoto za elimu. Mkurugenzi wa Ocode, Joseph Jackson, alisema wametoa msaada wa madawati 39, viti 13 vya walimu na kukabidhi chumba kimoja cha darasa kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya awali katika shule hiyo.

Akizungumzia msaada huo Jackson alisema, upo katika utekelezaji wa mradi wa elimu, ambao utakuwa wa kipindi cha miaka mitano.

Alisema, mradi huo ulioanza kutekelezwa mwaka 2019 unatarajia kumalizika 2023 na kwamba lengo ni kuwasaidia watoto wa shule za awali na msingi katika kuwawekea mazingira mazuri ya elimu.

Pia, alisema katika chumba hicho cha darasa kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya awali, mpaka kukamilika kwake kimegharimu kiasi cha Sh. milioni 26.

"Ocode kwa sasa tunautekeleza mradi wa elimu ambao utakuwa unazigusa baadhi ya shule za msingi ambazo zipo katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, lengo letu kuwasaidia watoto hawa kuanzia elimu ya awali, la pili na la tatu ili waweze kupata elimu katika mazingira mazuri," alisema.

Katika utekelezajj wa mradi huo wameahidi kushirikiana na serikali na wadau wengine wa maendeleo ili kuleta mabadiliko chanya ya kimaendeleo kupitia elimu kuanzia ngazi za chini na kuendelea.

Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Ubungo, Beatrice Dominic, alisema, pamoja na juhuzi zinazofanywa na serikali, kuna changamoto kubwa ya miundombinu ya madarasa kwa shule za msingi na sekondari na anatambua walimu wanafanya kazi zao katika mazingira magumu.

Alilipongeza Shirika la Ocode kwa kuamua kushirikiana na serikali kuboresha sekta ya elimu kuanzia ngazi ya awali.

Shule ya Kibwegere iliyopo katika Manispaa ya Ubungo nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, kwa sasa ina jumla ya wanafunzi 1,741 ambao wanakabiliwa na upungufu wa walimu, uhaba wa miundombinu ya madarasa, ofisi za walimu, pamoja na matundu ya vyoo.

# Tulia azishukuru nchi za Francophone

**Na Salome Kitomari**

NAIBU Spika, Dk. Tulia Ackson, amesema kuwa serikali inatambua na kuthamini mchango wa nchi zinazozungumza Kifaransa kwenye maendeleo ya nchi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wa wakati wa hafla ya maonyesho ya vyakula vya nchi zinazongumza lugha ya Kifaransa (Francophone) zenye balozi zake Tanzania, alisema amefurahi kuwa muungano huo siyo wa suala la lugha pekee bali maendeleo ya nchi nyingine.

"Tunatambua na kuthamini mchango wa Francophone kwa kuhakikisha Tanzania haifanyi vizuri tu kiuchumi bali kijamii, na tumehakikisha masuala ya haki za binadamu na demokrasia, tunafurahi kuwa muungano wenu siyo kwa suala la lugha pekee, bali maendeleo na kuzisaidia nchi ambazo hazizungumza lugha hiyo," alisema.

"Tunaamini mtaendelea kushirikiana vyema kuhakikisha nasi (Tanzania) tunapiga hatua kubwa kama baadhi ya nchi zenu zilikofikia," alisema Dk. Ackson.

Awali Balozi wa Ufaransa nchini, Fredric Clavier, alisema miaka kumi ijayo idadi ya wanaozungumza Kifaransa itafikia milioni 5, na kwamba lugha hiyo ni ya nne kutumiwa kwenye 'internet', na kwamba watu milioni 132 duniani hujifunza lugha hiyo kila mwaka.

"Asilimia 59 ya watumiaji wa lugha hiyo wanaishi Bara la Afrika, na kuna nchi 88 zinazoshirikiana kwenye tamaduni, vyakula, lugha, sera za kisiasa na maendeleo yanayolenga kuinua lugha hiyo na maendeleo endelevu," alisema.

Kwa mujibu wa balozi huyo, nchi hizo zinalenda kuinua lugha hiyo, kuimarisha utafiti na kilimo cha umwagiliaji, uchumi, sayansi, maendeleo endelevu, utulivu na amani pamoja na hali za binadamu.

**HABARI KITAIFA**

# Ewura yazungumzia mlipuko gesi Morogoro

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imesema eneo palipolipuka mitungi ya gesi na kusababisha watu watano wakiwamo waandishi wa habari wanne kujeruhiwa wakati wakichukua matukio, palikuwa pakifanyika biashara isiyo halali.

Imesema ni sehemu ya kutunza mitungi mingi ya saizi na kampuni tofauti kwenye nyumba ya makazi sambamba na wapangaji, na uchunguzi wa awali umebaini mmiliki alikuwa akichanganya na kupunguza gesi.

Akizungumza na Nipashe katika eneo ilipoungua nyumba iliyokuwa na mitungi hiyo ya gesi, Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, alisema isingewezekana kwa mmiliki huyo kuwa na mitungi zaidi ya 30 katika chumba kidogo cha kupanga pamoja na wapangaji wengine.

Alisema mitungi hiyo imebainika kuwa ni ya kampuni mchanganyiko na baadhi ya mitungi hiyo inauzito wa kilo hadi 38, ambayo huuzwa hadi Sh.120,000 kwa jijini Dar es Salaam, jambo ambalo pia sio rahisi kuuzika katika mazingira hayo, ilipolipuka nyumba hiyo.

"Mmiliki wa mitungi hii alikuwa akitumia chumba kimoja kati ya vyumba vitano vilivyopo katika nyumba hii. Kwa hiyo chumba kilijibana na kusababisha joto, hivyo kutokea mlipuko, na ukizungumza na majirani wanasema hapa ilikuwa hata ukihitaji gesi ya Sh. 40,000 unapata, kwa hiyo kuna uchanganyaji na upunguzaji wa gesi ulikuwa ukiendelea," alisema Kaguo.

Kaguo aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa mamlaka mbalimbali ikiwamo Polisi na EWURA wenyewe watakapobaini mazingira kama hayo ya uhifadhi au uuzaji usio halali wa gesi, na kwamba wanaendelea kushirikiana na Polisi kumsaka mmiliki huyo.

# Waziri Zungu: NEMC kusajili vibali kwa njia ya mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amesema serikali kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) imejipanga kutoa huduma ya vibali vya biashara ya taka hatarishi kwa njia ya mtandao ili kuondoa usumbufu na kurahisisha mchakato wa upatikanaji wa vibali.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, baada ya mkutano wake na wafanyabiashara wa taka hatarishi, Waziri Zungu alisema serikali ina nia ya dhati ya kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na kuleta tija kwa wafanyabiashara na wawekezaji.

"Mpaka sasa kumekuwa na zuio la kutoa nje na kuingiza taka hatarishi na hivyo katika kipindi hiki cha zuio serikali inaendelea kuangazia changamoto ambazo zilipelekea zuio hilo kama vile kulinda malighafi kwa viwanda vya ndani, ucheleweshaji wa vibali na uharibifu wa miundombinu ya reli na madaraja," alisema.

Waziri Zungu alisema wizara yake ipo katika mazungumzo na wizara na taasisi zingine ili kuweka mfumo wa utoaji wa vibali kwa njia ya mtandao ili kurahisisha upatikanaji wa vibali hivyo kwa wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara hiyo.

"Serikali ipo katika majadiliano kuona namna nzuri ya utoaji vibali kwa njia ya mtandao na tunaamini kukamilika kwa mchakato huo kutasaidia kuondoa urasimu, kupunguza muda wa upatikanaji wake pamoja na usumbufu ambao umekuwa ukijitokeza," alisema.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara hao kuendelea kuwa wavumilivu wakati huu serikali ikiendelea kufanyia kazi changamoto mbalimbali ambazo zilijitokeza katika ufanyaji wa biashara hiyo ya taka hatarishi kwa kuwa hata serikali imeendelea kukosa mapato yanayotokana na kodi.

"Walioathirika na zuio siyo nyinyi peke yenu hata kwa upande wa serikali inakosa mapato kupitia biashara hii. Hata hivyo hatuwezi kuruhusu biashara ambayo inakiuka mikataba ya kimataifa na kuharibu mazingira yetu kwa lengo la kujipatia kodi," alisema na kuongeza kuwa serikali inafanyia kazi kabla ya kurudisha mrejesho.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, aliwaondoa wasiwasi wafanyabiashara ambao wamekuwa wakitumia vibali vya Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa upande wa Zanzibar (ZEMA) kuingiza mizigo yao Tanzania Bara.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Stop One & Company, Yusuph Ally amepongeza utaratibu mpya wa utoaji wa vibali kwa njia ya mtandao na kuongeza kuwa utaongeza tija na ufanisi kwa pande zote mbili.



Mbunge wa Musoma Vijijini mkoani Mara, Profesa Sospeter Muhongo (mwenye kofia) na baadhi ya wakazi wa Halmashauri ya Musoma, wakiwa na moja magunia ya mahindi yaliyotolewa na Mbunge huyo kwa ajili ya chakula kwa shule za msingi Sokoine na Chirorwe, kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, yaliyofanyika katika kijiji cha Chirorwe juzi. **NA MPIGAPIGA WETU**

# Wanawake mjini wapewa changamoto

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WANAWAKE wenye maendeleo waishio mjini, wametakiwa kuwashika mkono wanawake waishio vijijini katika kujikwamua kiuchumi kwa kupeleka elimu ya ujasiriamali na uthubutu kwenye ngazi za vijiji.

Meneja wa Benki ya Azania tawi la Geita, Roda Baluya, ameyasema hayo wakati wa kongamano la 'Fahari ya Mwanamke Geita' lililokuwa na lengo la kuwajengea uwezo wa kujiamini na kuchangamkia fursa za kiuchumi ili kuleta maendeleo ya pamoja badala ya kubaki kuwa wategemezi kwenye familia.

Baluya alisema wanawake wanapaswa kutambua maendeleo yao yatapatikana endapo wao watakuwa na umoja, kushirikiana na kubebana katika sekta za kiuchumi badala ya kutumia nafasi zao kuwakandamiza wanawake wenzao ili wasifanikiwe.

"Wanawake wenzangu tufanye kazi, kuweni na ndoto ya mambo makubwa usikubali kukaa na kusubiri huu mwaka wa 2020 uwe wetu kujikwamua kiuchumi na usijiangalie wewe mwenyewe mfuate na aliyeko kijijini mwezeshe anyanyuke," alisema Baluya.

Mtoa elimu katika kongamano hilo, Maza Sinari, alisema endapo elimu ya kujitambua na ujasiriamali itapelekwa vijijini itaondoa mgawanyo kati ya wanawake wa mjini na vijijini ili kufikia uchumi wa viwanda.

Sinari alisema amekuwa mfanyabiashara wa muda mrefu, lakini anaendelea kujifunza na kuwataka wanawake kutoridhika na hali waliyonayo na badala yake wanapaswa kuanza kidogo kidogo ili kufikia malengo makubwa badaye.

Alisema kilio cha wanawake cha kukosa mtaji na kuwafanya washindwe kufanya biashara sio cha kweli kwani mtaji mkubwa kwa mfanyabiashara ni fikra na mtazamo unaomuwezesha kuziangalia fursa za kiuchumi zinazomzunguka.

"Mimi huwa nawaambia wanawake waheshimu pesa ndogo iwape heshima kubwa," alisema Sinari.

Mwandaaji wa kongamano hilo, Gathi Joseph, alisema lengo la kuandaa kongamano hilo ni ili kupata walimu watakaowasaidia wanawake kujiamini kusimama hata pale watakapokutana na changamoto za kibiashara.

Gath aliwataka wanawake kutobweteka na uwezo wa waume zao, badala yake waanze kujisimamia wenyewe ili hata pindi inapotokea mume ameondoka waweze kusimamia familia kwenye nyanja zote za kiuchumi.

Mbunge wa Busanda, Lorensia Bukwimba, alisema asilimia 52 ya watu nchini ni wanawake, lakini katika nafasi mbalimbali za maamuzi wanawake nafasi zao ni ndogo ambapo ndani ya bunge wanawake ni asilimia 37 pekee.

Bukwimba aliwataka wanawake kutumia maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kujitathmini kisha kuthubutu ili kuleta mabadiliko katika ngazi za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

# BARCELONA YASHUSHA BEI YA COUTINHO



**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich imefurahishwa na uamuzi wa Barcelona wa kupunguza bei ya kiungo wake, Philippe Coutinho kutoka euro milioni 120 hadi euro milioni 80 na sasa wanafikiria kumsajili kipindi cha majira ya joto.

Coutinho anacheza pale Bayern Munich kwa mkopo wa misimu miwili akitokea Barcelona, lakini mkataba huo unatarajiwa kuisha mwishoni mwa msimu huu na miamba hiyo ya Allianz Arena inataka kumchukua jumla, lakini tatizo lilikuwa bei yake kuwa kubwa mno.

Awali Barcelona ilikuwa inataka euro milioni 120 ili kumuachia raia huyo wa Brazil ili atue moja kwa moja Bayern Munich, lakini baada ya mvutano wa muda mrefu timu hiyo ya Nou Camp imeamua kushusha dau lake hadi kufikia euro milioni 80.

Uamuzi huu wa Barcelona unaonekana kupokewa kwa mikono miwili na Bayern Munich ambayo sasa inajiandaa kumchukua jumla staa huyo wa zamani wa Liverpool ambaye ameshindwa kujihakikishia namba pale Nou Camp. Coutinho alinunuliwa kutoka Liverpool na Barca kwa pauni milioni 142.

# Solskjaer amtaka jumla Ighalo

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ameonyesha nia ya kutaka kumsajili kwa mkataba wa kudumu, Odion Ighalo anayecheza kwa mkopo pale Old Trafford akitokea Shanghai Greenland Shenhua ya China.

Nyota huyo tangu atue pale Old Trafford amefunga mabao manne katika mechi nane.


Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Nigeria, aliiongoza Man United kwa kupachika bao moja katika mchezo wa Ligi ya Europa dhidi ya LASK ya Austria waliyoifumua mabao 5-0, Alhamisi.

"Odion amekuwa akifanya vizuri tangu alipojiunga na timu, amekuwa akiimarika kadri siku zinavyosonga mbele, ameonyesha kiwango ambacho natamani kuendelea kukiona kwenye timu," amesema Ole na kuongeza;

"Ana uwezo mzuri wa kufunga na anajua kushambulia, ameonyesha kutokuwa na hofu na lolote."

Kocha Ole amemsifia Ighalo kwa kusema; "Anatambua majukumu yake katika timu, ni mzuri pia kwenye kuzuia, amekuwa akijitahidi kuwa na maelewano mazuri na wachezaji wenzake uwanjani."

Mabao mengine ya Manchester United katika mchezo dhidi ya LASK ambao walicheza ugenini nchini Austria, yalifungwa na Daniel James, Juan Mata, Mason Greenwood na Andreas Pereira kila mmoja akipachika bao moja.





# *Werner apiga hesabu pakwenda*

**DORTMUND,** Ujerumani

NYOTA wa Klabu ya RB Leipzig, Timo Werner amebainisha kwamba anafanya uchambuzi wa klabu gani anayoweza kujiunga nayo kipindi cha majira ya joto kijacho.

Mshambuliaji huyo wa Ujerumani, kwa sasa amekuwa ndiye anayetajwa zaidi kutakiwa na klabu kadhaa za Ulaya.

Werner amekuwa na msimu wa kuvutia pale RB Leipzig, akifunga mabao 27 na kutoa pasi za mwisho 12 katika mechi 36 kwenye mashindano yote msimu huu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, amekuwa akitolewa macho na klabu kadhaa, kutaka saini yake, lakini mwenyewe amesema bado anafikiria wapi pakwenda.

Liverpool, Barcelona, Manchester United na Real Madrid zimetajwa mara kadhaa kuisaka saini yake.

"Bado sijajua nini kitatokea. Klabu gani nitakwenda? Sijui," alisema Werner akinukuliwa na gazeti la Bild la Ujerumani.

"Ninafanya kwanza uchambuzi na kuangalia klabu gani naweza kujiunga nayo, lakini kwa sasa tusubiri kwanza, maana bado nipo hapa RB Leipzig, nitatoa msimamo baadaye."

# Bruno: Sikufikiria mara mbili kutua Man United

**MANCHESTER,** England

BRUNO Fernandes amefichua kwamba, hakujiuliza mara mbili wakati alipopata ofa ya kujiunga na klabu ya Manchester United, kwani ilikuwa chaguo lake la kwanza.

Bruno amesema hakuweza kujiuliza mara mbili ilipokuja ofa ya kutakiwa kujiunga na United kwani alifanya maamuzi mepesi tu mara moja.

"Kujiunga na United lilikuwa kwangu kila siku, lilipokuja tu kwangu wala sikufikiria maamuzi mara mbili zaidi ya kujiunga nao," alisema.

Alisema alizungumza na klabu yake ya zamani (Sporting Lisbon) ambao tayari walikuwa na maongezi ya awali na United kabla ya yeye mwenyewe kufanya maamuzi.

"Niliwaambia kabisa Sporting kwamba chaguo langu la kwanza ni United, kwa hiyo hata wakati wanafanya mazungumzo walikuwa wanajua kabisa msimamo wangu," alisema.

Kiungo huyu amejiunga na United katika dirisha la usajili wa Januari akitokea Sporting Lisbon, akiichezea mechi tisa za mashindano yote na kufunga mabao matatu mpaka sasa.





# WHO YAWASHUKURU RONALDO, POGBA MAPAMBANO CORONA

**MANCHESTER,** England

JURGEN Klopp, Cristiano Ronaldo na Paul Pogba wamepata ujumbe wa shukrani kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tedros Adhanom Ghebreyesus kwa "kuhamasisha afya na kuwalinda watu kutokana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona".

Mwanasiasa na msomi huyo wa Ethiopian aliwashukuru nyota hao pamoja na wengine kutoka katika michezo mingine ambao walibeba majukuu binafsi ya kuhamasisha kutoenea kwa ugonjwa huo.

Ronaldo aliposti ujumbe kwenye ukurasa wake wa Twitter na kuwaambia wafuasi wake "kufuata ushauri wa WHO", huku Klopp akiwaambia mashabiki wa Liverpool "kufikiria njia nzuri kwenye jamii na kuchukua maamuzi haraka pale wanapohisi kunaweza kusababisha maambukizi".

Pogba aliwaambia wafuasi wake milioni 39.7 kwenye mtandao wa Instagram "kupambana na corona" - kwa kujilinda wakati wa kukohoa, kupiga chafya kwa kutumia kitambaa badala ya mikono - kama WHO inavyoshauri.

"Asante Jurgen Klopp na Liverpool FC kwa ujumbe wako mzuri kwa dunia," aliandika Ghebreyesus kwenye ukurasa wake wa Twitter.

"Wafanyeni watu wajali kwanza afya, wapunguze hatari, kujali mazingira na kujilinda: Na hivyo ndivyo WHO inavyotaka.

"Tutashinda mapambano dhidi ya COVID-19 kama tutafanya kazi kwa pamoja.

"WHO inawashukuru sana Jurgen Klopp na Liverpool FC, Alisson Becker, Cristiano Ronaldo, Paul Pogba, Fifa, Peter Schmeichel, Andrea Radrizzani, Romain Grosjean na nyota wengine kwenye michezo duniani."

# *Mahrez afunguliwa mlango wa kutokea*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imemfungulia mlango wa kutokea kiungo wake, Riyad Mahrez ambaye ameripotiwa kutakiwa na miamba wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Paris Saint-Germain.

Mahrez alijiunga na Man City mwaka 2018, lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England wameripotiwa kuwa tayari kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Algeria.

Huku Man City ikiwa imepewa adhabu ya kufungiwa kutoshiriki mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya, (Uefa) kwa misimu miwili, wanaona kwamba Mahrez anaweza kuondoka hapo kwenye dimba la Etihad.

Na sehemu pekee anayoonekana yeye kutaka kwenda ni Paris Saint-Germain.

Kwa mujibu wa Calciomercato, Mahrez mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kuondoka hapo ili aweze kupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Man City haina tatizo la kumuuza Mahrez kwenda PSG, mlango uko wazi kwake kama akitaka kuondoka, kilidokeza chanzo kimoja kutoka Man City kikinukuliwa na gazeti la Daily Mail.

Mahrez, msimu huu ameanza katika mechi 15 kati ya 23 za Ligi Kuu ya England.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA KUSITISHA NIA KWA AUBAMEYANG

## Miamba hiyo ya LaLiga imemwambia straika huyo wa Arsenal kwamba yeye si kipaumbele...

**LONDON,** England

ARSENAL ipo tayari kumuuza Pierre-Emerick Aubameyang kama hawatafikia makubaliano naye, lakini Barcelona ipo tayari kusitisha mpango wake wa kutaka kumsajili kipindi cha majira ya joto.

**Barcelona ilikuwa inawania kumsajili Aubameyang wakati wa kipindi cha majira ya joto kinachokuja kwa ajili ya kuimarisha safu yake ya ushambuliaji.**

Na walimwona nahodha huyo wa Arsenal ambaye amefunga mabao 20 katika mechi 32 alizocheza kwenye mashindano yote msimu huu kuwa ndiye suluhisho kwao.

'Washikabunduki' hao mkataba wao na Aubameyang mwenye umri wa miaka 30, unamalizika mwishoni mwa msimu ujao na amekuwa akuhusishwa na kutakiwa Barcelona na Inter Milan.

Na ingawa wameimarika chini ya Mikel Arteta, klabu hiyo inaweza kukosa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa wa Ulaya na hilo ni pigo kwao kwa upande wa kuingiza fedha.

Aubameyang anataka mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki ikiwa ni ongezeko la asilimia 30 kutoka kwenye mkataba wake wa sasa na hilo limechangia mazungumzo ya mkataba mpya kusimama na sasa wataangalia uwezekano wa kumuuza.

Lakini Barca imemwambia Aubameyang kwamba yeye si kipaumbele chao kwa sababu wanawania kumsajili nyota wa Inter Milan, Lautaro Martinez na kumrudisha Neymar kutoka Paris Saint-Germain.

Inter imeendelea kuonyesha nia yake ya kutaka kumsajili kwani wanajua wakimuuza Martinez watakuwa na fedha ya kumnunulia Aubameyang kama akishindwa kufikia makubaliano na Arsenal.

Uwezekano wa kuondoka kwa mshambuliaji huyo ni mkubwa kwa sababu Arsenal wanaonyesha hawana uwezo wa kumbakisha, lakini Ian Wright anaona kwamba hakuna kitakachomzuia Aubameyang kuondoka klabuni hapo.

"Kama ukimfikiria kwenye timu bora, angeweza kushinda taji la Ligi Kuu na kupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya na nafikiri anastahili hilo," alisema Wright ambaye ni mshambuliaji wa zamani wa Arsenal.

"Huwezi kumuona mara nyingi akizungumza uwanjani, hanyooshei mtu kidole wala kupiga kelele, lakini anafanya kile kinachotakiwa kuwaheshimu viongozi wake kwa kufunga mabao.

"Kama ukiyatoa mabao yake, timu ingekuwa kwenye wakati mgumu zaidi kwa sasa. "Arsenal inahitaji wachezaji wapya ili kuweza kucheza naye na kumsaidia.

"Tunamzungumzia mfungaji wa mabao ambaye anafunga kwa kiwango cha mchezaji wa Ligi ya Mabingwa Ulaya au daraja la juu kabisa duniani.

"Tunazungumzia kuhusu mkataba wake mkubwa wa mwisho katika maisha yake ya soka.

"Natumaini kwamba mapenzi aliyonayo kwa klabu na mashabiki yanatosha, lakini anataka kuwa kwenye nafasi yake."

Aubameyang amekuwa na msimu mwingine wa kuvutia baada ya kufunga mabao 20 katika mashindano yote msimu huu.

## ZISIKUPITE

### UEFA KUIAHIRISHA EURO 2020

SHIRIKISHO la Vyama vya Soka Ulaya, Uefa, linafikiri kuihamishia michuano ya Euro 2020 Desemba ili kutoa muda wa kutosha kwa Ligi Kuu ya England na mashindano mengine kumaliza ratiba zao wakati wa kipindi cha majira ya joto, baada ya kusimamishwa kwa muda kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. ***(Sunday Telegraph)***

### MAHREZ KWENDA PSG

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Riyad Mahrez, 29, anafikiria kwenda Paris St-Germain, ambayo imeonyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Algeria kipindi cha majira ya joto. ***(Express)***

### NEYMAR KURUDI BARCELONA

KLABU ya PSG inatarajia mshambuliaji wao raia wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 28, ataondoka wakati wa kipindi cha majira ya joto na kurudi katika klabu yake ya zamani, Barcelona kwa euro milioni 150. ***(Marca)***

### MANE CHAGUO LA KWANZA REAL

MIAMBA wa Ligi Kuu ya Hispania, Real Madrid imemtaja mshambuliaji wa Liverpool na timu ya Taifa ya Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 27, kuwa ndiye chaguo lao la kwanza kwenye usajili wa kipindi cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### CHELSEA YAMPA OFA BAILEY

CHELSEA inajiandaa kutoa ofa ya pauni milioni 85 kwa winga wa Bayer Leverkusen na timu ya Taifa ya Jamaica, Leon Bailey mwenye umri wa miaka 22, baada ya kumwangalia akicheza kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga na Ligi ya Europa. ***(Sunday Express)***

### JUVE YAMKATIA TAMAA POGBA

KLABU ya Juventus inatafuta kiungo, na wamewekeza nguvu zao kumwania nyota wa kimataifa wa Italia, Sandro Tonali mwenye umri wa miaka 19, anayecheza pale Brescia pamoja na mchezaji wa Ufaransa, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 21 anayekipiga kule Lyon, wakati matumaini yao ya kumrudisha, Paul Pogba, 27, kutoka Manchester United yakianza kudidimia. ***(Tuttosport)***

### CHELSEA MACHO KODO BARCA

KLABU ya Chelsea imeingia kwenye mbio moja na Napoli za kumuwania nyota wa Barcelona, Marc Cucurella mwenye umri wa miaka 21, ambaye anacheza kule Getafe. Pia klabu za Borussia Monchengladbach na Bayer Leverkusen zinamtolea macho beki huyo wa kushoto wa kimataifa wa Hispania. ***(Mail on Sunday)***

### KONDOGBI AMKUNA MOURINHO

KIUNGO mkabaji wa Valencia, Geoffrey Kondogbia mwenye umri wa miaka 27, anawaniwa na Tottenham, baada ya kiwango cha mchezaji huyo wa kimataifa wa Jamhuri ya Kati kumvutia kocha, Jose Mourinho. ***(Goal)***

### MAN UNITED YAMTAKA JIMENEZ

MSHAMBULIAJI wa Mexico, Raul Jimenez mwenye umri wa miaka 28, amefungua mlango wa kutaka kuondoka Wolves, huku Manchester United ikitajwa kuwa ndio inayomwania. ***(Manchester Evening News)***

### JONES ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inapambana kutaka kumsajili beki wa Manchester United na timu ya Taifa ya England, Phil Jones mwenye umri wa miaka 28. ***(Sunday Mirror)***

## Corona yapeperusha Umisseta, Umitashumta

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameahirisha mashindano ya michezo kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na yale ya Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) kwa mwaka 2020, kutokana na tishio la kusambaa kwa virusi vya corona.

Jafo alitoa kauli hiyo jana, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema mashindano hayo yaliyotarajiwa kufanyika hivi karibuni yameahirishwa hadi watakapotangaza tena.

"Hivyo wanafunzi wote wanaohusika na michezo hii kuanzia ngazi ya msingi mpaka sekondari wanatakiwa kubaki kwenye shule zao na kuendelea na masomo yao kama kawaida," alisema.

## Cioaba alia umakini mastraika Azam

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Arstica Cioaba, amesema kutokuwa makini kwa washambuliaji wake ni sababu kubwa ya kushindwa kupata idadi kubwa ya mabao katika mechi za Ligi Kuu Bara msimu huu.

Safu yake ya ushambuliaji ushindi mkubwa iliyopata msimu huu ni dhidi ya Alliance FC ilipofunga mabao 5-0.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Cioaba alisema wachezaji wake wanashindwa kutumia nafasi wanazozipata jambo linalowapa ugumu kuondoka na pointi tatu.

Alisema washambuliaji wake wanapoteza nafasi nyingi wakiwa ndani ya 18 jambo linalowafanya washinde kwa mabao machache kwenye mechi zao nyingi za ligi walizocheza.

"Ukiangalia mechi na Ruvu Shooting, tumepata ushindi wa mabao 2-1, yote akifunga Nevere Tegere, lakini pia tumekosa nafasi nyingi za wazi huku Obrey Chirwa na Shaban Chilunda wakigongesha mwamba na kipa kudaka," alisema Cioaba.

Hadi sasa wakati huu Azam FC ikiwa na pointi zake 54 baada ya kushuka dimbani mara 28 msimu huu, imefunga mabao 37 na kuruhusu nyavu zake kutingishwa mara 20.

# TFF YAIENDEA FIFA UGANDA KUCHEZESHA VIJEBA U-17

**Na Somoe Ng'itu,** KAMPALA

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limewasilisha rufani Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), likilalamikia Uganda kutumia wachezaji waliozidi umri wa miaka 17 'vijeba' katika mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa wachezaji wa U-17.

**TFF iliwasilisha rufani hiyo saa chache kabla ya kikosi chake hakijakumbana na kichapo cha mabao 5-0 katika mechi ya marudiano iliyochezwa juzi jijini hapa.**

Matokeo hayo yaliifanya Tanzania kuondolewa katika mashindano hayo kwa kufungwa jumla ya mabao 6-2.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa, Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Oscar Milambo, alisema uamuzi wa kukata rufani ulifanyika baada ya kupata taarifa muhimu za wachezaji watano wa Uganda ambao ni wakubwa kitu ambacho ni kinyume na kanuni za mashindano hayo.

Milambo aliwataja wachezaji hao ambao walizidi umri kuwa ni pamoja na Namusisi Joan, Fauzia Najjemba, Nalugya Shamira na nahodha Juliet Nalukenge.

Kiongozi huyo alisema baada ya kujiridhisha, Tanzania ilifikia kuandika rufani hiyo na inaamini Fifa itatenda haki.

"Baada ya kujiridhisha, na kupata vielelezo vyote vya kuonyesha kuwa wachezaji hao hawakustahili kucheza mechi ya U-17 kwani wana umri mkubwa zaidi na hawapaswi hata kucheza mechi za U-20, na wengine walionge-zwa katika mechi ya leo (juzi)," alisema Milambo.

Naye Kocha Mkuu wa timu ya Tanzania, Bakari Shime, alianza kwa kupongeza Uganda kwa ushindi, lakini akasema matokeo hayo ni ya kujifurahisha kwao kwani wamefanya udanganyifu ambao katika michezo hauruhusiwi na una athari kubwa kwa maendeleo ya soka.

Shime alisema matokeo ya mchezo huo hayajamuumiza sana kwa sababu wapinzani wao walichezesha wachezaji ambao hawakustahili.

"Hii ilikuwa ni kampeni ya kitaifa, Waganda wenyewe wanaujua ukweli, kwa upande wetu sisi tunaendelea kujenga timu, tunaendelea kuwajenga wachezaji wetu," alisema Shime.

Kikosi cha Tanzania kilirejea nchini jana mchana na wachezaji watarudi katika klabu zao kuendelea na mechi za Ligi Kuu ya Wanawake baada ya mchezo ujao wa kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia kwa vijana wa umri chini ya miaka 20 dhidi ya Senegal uliotarajiwa kuchezwa Machi 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kuahirishwa kutokana na kuenea kwa virusi vya corona duniani.




Mkurugenzi wa Uendeshaji na Udhibiti wa SportPesa, Tarimba Abbas (kulia), akimkabidhi mipira Katibu wa timu ya Sungura FC, Said Namaona, katika hafla fupi ya ugawaji wa vifaa vya michezo mkoani Lindi mwishoni mwa wiki, huku wakitumia miguu kusalimiana ikiwa ni njia ya kuepuka maambukizi ya virusi vya corona, ambavyo hata hivyo havijabisha hodi nchini. **PICHA: SPORTPESA**

# *SportPesa yamwaga vifaa vya michezo Ruangwa*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo ya Kubashiri ya SportPesa Tanzania, imeunga mkono juhudi za Waziri Mkuu na Mbunge wa Ruangwa, Kassim Majaliwa za kuendeleza michezo kwenye Wilaya ya Ruangwa baada ya jana kugawa vifaa vya michezo wilayani hapo.

Vifaa vilivyotolewa na SportPesa ni kutoka kwa timu mbalimbali ambazo inazidhamini Ulaya kwa ajili ya kuisaidia michezo Afrika kupitia Kampeni ya SportPesa inayojulikana kama Kits For Afrika.

SportPesa ambayo inaidhamini pia timu ya Namungo FC ya Ruangwa ilipata nafasi ya kutembelea mkoa wa Lindi na kuzungumza na baadhi ya viongozi wa timu mbalimbali katika kuunga mkono juhudi za Majaliwa ya kuhakikisha soka linakua.

Akizungumza na timu hizo, Tarimba alisema katika kutambua umuhimu wa michezo, SportPesa imeona ni vema ikatoa vifaa vya michezo ikiwamo mipira na lengo ni kuona vijana wanapata mafanikio kama ilivyokuwa kwa Mbwana Samatta anayeichezea Aston Villa ya Uingereza.

Tarimba alisema wamevutiwa na mwenendo wa Namungo inayoshika nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu Bara na kushawishika kumwaga vifaa Ruangwa.

Aliongeza kuwa, huo ni mwanzo kwa timu nane za Ruangwa walizozipatia zawadi za vifaa vya michezo huku wakipanga kuzipa timu nyingine wilayani hapo kwa baadaye zikiwamo jezi mpya.

"SportPesa kama kampuni ya ubashiri hapa nchini, imeona vema kuunga mkono juhudi za Waziri Mkuu na Mbunge wa Ruangwa, Majaliwa katika kuendeleza michezo katika wilaya yake.

"Kwa kuanza, tumeanza na timu nane kubwa za wilayani hapa Ruangwa na baadaye tutatoa tena vifaa vingine vya michezo zikiwamo jezi kama ilivyokuwa Namungo inayofanya vizuri katika ligi.

"SportPesa imekuwa sehemu ya kuunga michezo hapa nchini na ikumbukwe kuwa SportPesa iliwahi kuzileta klabu kubwa za kutoka Ulaya ikiwamo Everton inayoshiriki Ligi Kuu ya Uingereza na Sevilla inayocheza LaLiga ya huko Hispania," alisema Tarimba.

**Michezo**

Jumatatu Machi 16, 2020

Nipashe



Barca kusitisha nia kwa Aubameyang UKURASA 30

**HAKUNA KULALA...**



Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi katika Uwanja wao wa Mo Simba Arena uliopo Bunju, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam. Timu hiyo inajiandaa na mechi yao ijayo ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ruvu Shooting. NA PICHA: MTANDAO

# YANGA YASOGEZA UBINGWA SIMBA

## ● ● ● Namungo yaing'ang'ania Uwanja wa Majaliwa, huku KMC ikiendeleza ushindi kwa...

**Na Adam Fungamwango**

SARE ya bao 1-1 iliyoitoa Yanga jana kwenye Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi dhidi ya wenyeji Namungo FC, imeendelea kutoa nafasi kwa watani zao, Simba kuukaribia ubingwa wa Tanzania Bara msimu huu.

**Kwa matokeo ya mechi ya jana, Simba inahitaji pointi 14 tu iweze kutangazwa kuwa mabingwa wa Tanzania kwa mara ya tatu mfululizo.**

Ni pointi zinazoweza kupatikana kama ikishinda mechi tano kati ya 10 ilizosalia au mechi nne na sare mbili ili kufikisha alama 85 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote katika msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Yanga ambayo katika mechi ya jana ilitandaza kandanda safi tofauti na mechi yake dhidi ya KMC, ilipata bao la mapema tu lililofungwa na Tariq Seif dakika ya tano, baada ya krosi ndefu iliyochongwa na Juma Abdul.

Straika huyo alimfunga kipa Nurdin Balora ambaye walicheza naye kwenye klabu ya Biashara ya Mara, kabla ya kila mmoja kutimka kivyake.

Baada ya bao hilo, wachezaji wa Namungo walionekana kupoteana na kuwaruhusu Yanga kufanya mashambulizi mengi langoni mwa wapinzani hao, lakini wachezaji wake wakakosa umakini.

Bernard Morrison, akicheza kwa mara ya kwanza baada ya mechi dhidi ya Simba ambayo alifunga bao pekee, alikosa bao la wazi dakika ya 31, alipobaki yeye na kipa Balora, lakini shuti lake lilipanguliwa na kipa huyo.

Shambulio pekee la hatari kwa Namungo lilikuwa kwenye dakika ya 35, wakati straika wake hatari, Bigirimana Blaise alipopiga kichwa safi akiunganisha krosi iliyochongwa na Lucas Kikoti, lakini mpira ukatoka nje kidogo ya lango.

Kipindi cha pili Namungo ilionekana kuamka, wachezaji wake wakilishambulia kama nyuki lango la Yanga.

Jitihada zao zilizaa matunda dakika ya 61 waliposawazisha bao lililofungwa na Mrundi Bigirimana kwa kichwa, akiunganisha mpira wa faulo uliopigwa na Kikoti.

Pamoja na timu zote kupambana kutaka kuibuka na ushindi na hasa Yanga, ikipeleka mashambulizi dakika za mwisho, lakini mechi hiyo iliisha kwa sare ya bao 1-1.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga kuendelea kukamata nafasi ya tatu, sasa ikifikisha pointi 51, nyuma ya Azam yenye pointi 54 na Simba yenye pointi 71, lakini kikosi hicho cha Mbelgiji Luc Eymael kikiwa na mechi moja mkononi.

Kwa upande wa Namungo inasalia nafasi ya nne na kushindwa kuishusha Yanga, ikiwa imejiongezea alama moja na kufikisha pointi 50.

Baada ya mechi hiyo, hesabu zinaonyesha iwapo Yanga itashinda mechi zote 11 zilizosalia na Azam zote 10 zilizosalia, kila mmoja itafikisha pointi 84, kwa maana hiyo Simba sasa inahitaji kufikisha pointi 85 ili iweze kutwaa ubingwa.

Katika mechi nyingine iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, KMC imeendeleza wimbi lake la ushindi kwa kuifunga Alliance FC mabao 2-1, ikifikisha pointi 33 kwenye nafasi ya 14 na kuiacha Alliance kwenye nafasi ya 18, ikiwa na pointi 29.

# Simba, Yanga zinaibiwa - Serikali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

LICHA ya mechi ya Simba na Yanga iliyopigwa Uwanja wa Taifa Machi 8, mwaka huu kuingiza kiasi cha Sh. milioni 545, kiasi kikubwa cha fedha kimepotea kwa njia za 'panya' huku wapigaji wakibainika, serikali imeelezwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Hassan Abbas ndiye aliyeanika hadharani suala hilo huku akitishia kuwataja hadharani wale wote wanaohusika na upotevu huo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Dk. Abbas ambaye ni Msemaji Mkuu wa Serikali, alisema imebainika katika upotevu huo kuna tiketi feki zilikamatwa na baadhi ya magari ya taasisi kutumika kuingiza watu uwanjani kwa njia za panya.

"Rais John Magufuli aliungana na Watanzania katika kushuhudia mchezo huo wa Simba na Yanga, ambayo ilivunja rekodi ya mapato kwa kuingiza Sh. milioni 545.4, ni fedha ambazo tangu Simba na Yanga ziumbwe haijawahi kupatikana.

"Kwa mfano kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita mwaka 2016 mapato yalikuwa Sh. milioni 357, mwaka 2017 Sh. milioni 324, Agosti, 23 mwaka 2017 Sh. milioni 381, Oktoba 28 mwaka 2017 Sh. milioni 113, Aprili 29 mwaka 2018 Sh. milioni 376," alisema.

Alieleza kuwa Septemba 28, mwaka 2018 Sh. milioni 404, Februari 16, mwaka 2019 Sh. milioni 342 na Januari 4, mwaka huu Sh. milioni 539.

"Nimekuwa Katibu Mkuu kwa kipindi cha mwezi mmoja na nusu uliopita nilichokibaini kuna upotevu mkubwa wa mapato na kuna mianya mbalimbali, kwenye mechi hii siri moja ambayo hamjui mimi mwenyewe nilienda geti kwa geti nilishinda uwanjani," alisema.

Alisema watu wamekuwa wakiingia bure kwenye mechi na kusababisha klabu kuendelea kuwa maskini kwa kutokana na kufanya hujuma za upotevu wa mapato.

"Watanzania tuache njia za panya kuingia uwanjani, kuna ubabaishaji upotevu wa mapato kwenye mechi watu waliingia 59,000 wakati iliyopita ni 58,000 na huenda waliofika uwanjani ni 70,000," alisema.

Msemaji huyo alisema amebaini kona zote za panya, na kwamba wapo wadau wa soka ikiwamo taasisi ambao wanashiriki kuingiza watu uwanjani.

"Juzi tumekamata tiketi feki nyingi na tunafuatilia mtandao, nawapa angalizo katika mechi ijayo nitataja taasisi na mtu mmoja mmoja anayehusika kwenye upotevu wa mapato kwa kuanzia viwanja vya Dar es Salaam," alisema.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042